# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KISAUNI CONSTITUENCY, MLALEO SCHOOL.

**ON**

**6TH MAY 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KISAUNI CONSTITUENCY HELD AT MLALEO SCHOOL ON 6TH MAY 2002.**

**Present:**

1. Com. Prof. H.W. Okoth-Ogendo
2. Com. Salome Muigai
3. Com. Pastor Zablon Ayonga
4. Com. Paul M. Wambua

**Secretariat Staff in Attendance:**

1. Eunice Gichangi - Programme Officer
2. Phillip Mollo - Asst. Programme Officer
3. Regina Obara - Verbatim Recorder
4. Milka Mahindu - Sign Language Interpreter

**Meeting was called to order with a word of prayer.**

**Najib K:** Ningeomba tuanze na maombi jambo (inaudible).

**Maombi:** Ee Mwenyezi Mungu mwenye kuneemesha neema zote hapa ulimwenguni, mwenye kuneemesha wema hapa ulimwenguni, na mwenye kuneemesha wema wa (inaudible) kesho athera. Kwa kweli nakuabudu na kwa kweli ninataka msaada. Ee Mwenyezi Mungu tuongeze katika shughuli hizi na mambo haya tutakayoyafanya hapa. Kwake wewe ndio

tunaweza pata msaada, na kwako wewe tunaweza fanikiwa. Ee Mwenyezi Mungu, tusaidie.

**Najib K:** Tungepata mwingine wa thehebu la Kikristu atuombee tafadhali. Ni nani atajitolea?

**Maombi:** Baba katika jina la Yesu Kristu tunakushukuru (inaudible). Tunasema ni asante kwa sababu ya siku hii njema ambayo umetupa tuweze kusherehekea na tuweze kushukuru katika ndani yake. Baba tunakushukuru kwa wakati huu ambao umeweza kutufanya tukakusanyika hapa ili tukapate kutoa maoni katika hiki kikao ambacho ni cha Kenya mzima. Baba tunaomba ya kuwa maoni ambayo tutatoa hapa, yataweza kusaidia kizazi hiki hata kizazi (inaudible) Baba tunaomba ukaweze mwenyewe na wale viongozi wako hapa na wale ambao wamekusanyika hapa, hekima ili yale ambayo watatoa itaweza kuwasaidia hao wenyewe na hata kizazi kijacho. Baba tunaomba utupe hekima kwa haya yote. Tunaomba hayo machache katika jina la Yesu Kristu aliye Mwokozi wetu. Amen.

**Najib K:** Kuna thehebu lingine lolote? Kuna thehebu lingine lolote? Hamna. Kwa jina naitwa Najib K. Mimi ni constitution committee wa Kisauni na hata hivyo nitampisha dada yangu (inaudible) Ndodo ambaye ni (inaudible aweze ku-introduce ma-commissioners na mpangilio ambao yuko nayo.

**Ndodo:** Hamjambo mabibi na mabwana?

**Wananchi:** Hatujambo.

**Ndodo:** Kwanza kabisa ningelitoa fursa hii kwa kuwashukuru nyote, ma-commissioners wetu, na nyote mliofika na wote waliotuongaza kwa maombi ya leo. (inaudible) tuko na commissioners watatu ambao ndio watatuongoza katika kikao chetu cha leo, kwanza kabisa nitaanza na Commissioner Paul Wambua, Commissioner Pastor Zablon Ayonga na watatu ni Com. Prof. Okoth-Ogendo. Sasa hao ndio commissioners wetu ambao tutakuwa nao siku ya leo na bila kupoteza wakati nitampisha Professor Pastor Zablon Ayonga atuanzie kikao chetu.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Nawakaribisha nyote kwa niaba ya ma-commissioner wenzangu tuliomo hapa mbele. Tumetaka tuanze kikao hiki na ningependa wale ambao tuna maoni ambayo yameandikwa, tutawapa dakika kidogo ya kuweza kutumulikia machache makubwa yaliomo katika hayo maandishe. Hamji kutusomea neno kwa neno kwa maana tutaenda kusoma ofisini. Na kwa hivyo wale wengine ambao mtatoa maoni yenu ambayo ya kwandikwa, nitaanza kuwapa dakika tano na ninapokuambia dakika zako zimekwisha, zimekwisha kwa sababu tunataka kumpisha mwingine naye apate nafasi ya kuweza kutoa maoni yake. Na kama hukuja una maoni umekuja kusikiza, sikiza tu, usijilazimishe kuanza kusema na mimi nataka kuongea na hali la kuongea huna. Kwa hivyo ikiwa una simu ya mkono tafadhali uzime. Uzime simu yako, nitaanza kuzima yangu. Kwa maana hatutaki hiyo simu iingie katika record. Maneno yenu yote mtakayosema yanachukuliwa kwa hivyo mtu asije afikiri, mbona naona yule hata aandiki, maneno yangu haya ni kama ni bure. Maneno yako yote utakayoyasema hata

ukikohoa, kihozi lako litaingia kule kwa hicho ki-machine. Kwa hivyo tungependa kila mmoja wenu ambaye aliyejitayarisha kuja kutoa maoni, utoe maoni. Hukuja hapa kutuuliza maswali. Leo hatukuja kuwafunza, leo tumekuja utupe maoni yako na maoni yako yatakuwa kwa namna ya kutupa suluhisho kwa yale unayo yataka, kwamba hivi na hivi ndivyo ningelitaka. Si kutuuliza kwamba na sasa hio tufanye je? La. Lazima ujue mtafanya aje. Kwa hivyo nitaanza na nitafwata orodha ya karatasi hii. Jinsi mlivyokuja mtu alipo register kule nje, nikikuita kama umekuja tu kusikiza, sema tu mimi nimekuja kusikiza, sina maoni. Mtu wa kwanza hapa ni James Olopono Oleminis. Ambavyo hatuna machini hii ya kutumika, tunataka ukiongea inua sauti yako juu ili hao wote walioko hapa waweze kukusikiza.

**James Olopono:** Asante Bwana Commissioner na commissioners wale wengine. Jina langu ni James Olopono Oleminis mimi ni mwanachama katika Kisauni Land Lobby Group. Nilitumia kitabu kile cha Tume ya Kurekebisha Katiba kutoa maoni kadha wa kadha. Yote nimeandika katika memorandum yangu, nitapeana kwa commissioners.

Kuhusu chanzo cha Katiba yetu au preamble, nitasoma kwa Kingereza. This Constitution is being enacted to merge our diversity in color, creed, religion, language and persuasion into one nation of brotherhood forging forward for the benefit of all. Every Kenyan must be able to read the reviewed Constitution and discover himself or herself inside it to the point of declaring that the Constitution is his own. Tungependa Katiba mpya iwe Katiba ya kila Mkenya. Akisoma anajisikia yeye yumo ndani.

Principles of state policy: We need to clarify our national philosophy and guiding principles. Kenya is a democratic republic which while agreeing to the views of the majority, also takes into consideration the views of the minority as they are part and parcel of our beloved nation. Kenyans are deeply religious and the Constitution must set each one free to practice his or her own beliefs as best as he thinks fit. Kenyans are endowed with a traditional and cultural heritage which must never be compromised or exchanged with foreign cultures being pedaled via the internet, television, video shows, radio and other news media. Any information that is unpalatable to the Kenyans must be rejected out right. There is no point in letting in poison in the name of liberization of trade which will end up poisoning ourselves as well as our young generation. The Constitution must clearly spell out what we can tolerate and what we cannot.

On constitutional supremacy: The current parliamentarians are selfish group. They are ego centric, they are self seeking legislators. Therefore the need to amend the Constitution must never be placed in their hands ever again, thus, the Constitution must protect itself from unwarranted amendments and any future amendments can only be carried out through Constitution of Kenya Review Commission so that every Kenyan has an opportunity to contribute and to participate. The present process we are adopting is an excellent example for the future. Marekebisho ya Katiba kila mmoja wetu aruhusiwe kushiriki na kutoa maoni sio tu katika bunge. Kila Mkenya ashiriki.

Citizenship: All Kenyans born in Kenya after 12th December, 1963 should become automatic citizens. Any child whose parent is a Kenya citizen should also become a citizen automatically. Any foreigner who declares he wishes or she wishes to become a

Kenyan, must be allowed to do so as long as he fulfills the required conditions. The conditions should be reduced to the minimum in order to encourage as many immigrants or refugees or aliens who would like to become Kenyans. Once a person is married to a Kenyan, he or she should automatically become a Kenyan regardless of the sex. In this regard I am considering our immediate people of Somalia, Ethiopia, Sudan, Uganda, Tanzania and the Indian Ocean Island where there is a lot of cross border marriages. Every citizen is entitled to basic rights, food, clothes, health, shelter, education, life, livelihood or employment, freedom of association and of expression. A citizen must obey the Constitution and all other laws being enacted from time to time.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Hebu muulika maoni yale makubwa makubwa.

**James Olopono:** Haya, asante. Maoni mengine yamo ndani ya karatasi ambayo nitapeana kwa hivyo nitafanya kwa ufupisho. Kuhusu uzalendo au citizenship, nimependekeza kila Mkenya awe Mkenya bila kuulizwa maswali mengi. Haya, kwa kuzaliwa, kwa ajili ya mzazi kuwa Mkenya na kwa ajili ya kupenda kuwa Mkenya. Unahamia kutoka nchi ingine, umependa kuishi Kenya na unataka kuwa Mkenya halisi, uruhusiwe, usizuiliwe kwa njia yeyote.

Kuhusu mambo ya vitambulishe: Ingewezekana tunapendelea kila Mkenya amezaliwa Kenya apewe kitambulisho, apewe passport, apewe cardi ya kura mradi tu akigonga miaka kumi na nane, tangu siku yake ya kuzaliwa. Na hiyo yote inawezekana kwa ajili Kenya sasa ni computerized, watoto wakizaliwa majina yao na siku ya kuzaliwa iwekwe ndani ya computer. Miaka ya kumi na nane ikifika, apewe vitu hivyo bila kuulizwa maswali zaidi.

Kuhusu defence and national security, usalama wa nchi: Rais haitajiki kuwa mkuu ya majeshi, haitajiki kusimamia kila sehemu, kila kituo, askari polisi, askari jeshi, hapana. Rais apeana vyeo vyingine kwa Wakenya na awaamini ya kuwa watasimamia jukumu yao bila wasiwasi. Kwa hivyo kuwezekane kuwe na Minister for Defence na aachwe afanye kazi yake kikamilifu. Kuwe na Commander of the Armed Forces tofauti na Rais na asimamie wanajeshi sawa sawa. Hapana changanya na si vizuri mtu mmoja kuwa na viti vyote ya Kenya. Igawanywe gawanywe, kila mwingine apewe.

Kuhusu vyama vya kisiasa: Ninapendekeza vyama viwe vitatu. Chama kimoja ambacho kina majority, chama ya pili ambacho kina majority ya pili na chama cha tatu, kiitwe independent party. Chama ambacho kitasomba Wakenya wengine ambao hawataki chama ya kwanza, na hawataki chama cha pili. Lakini kuwa na mlolongo ya chama arubaini, sitini haifai. Zipunguzwe, zifanyiwe screening, uchuji, zichujwe kabisa zibaki tu tatu pekee yake. Halafu sisi tunajiandikisha kwa hivyo vitatu.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** James saa yako imekwisha.

**James Olopono:** Asante sana Bwana mwenye kiti. Kuna mengine mengi ningesema lakini kwa vile nitapeana ikiwa kwenye kitabu, ninaamini ma-commissioners watashughulikia vilivyo. Asante sana.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Na ujiandikishe, ni lazima uweke kidole. Wapili anayemfuata James ni Omar Hussein Maktar. Mzee unamaandishi au,

**Hussein Omar:** Nina maandishi. Nitayazungumzia kidogo.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Ndio tafadhali ufanye kwa ufupi. Tunataka kila mtu apate nafasi.

**Hussein Omar:** Asalaam Alyeikum

**Wananchi:** Alyeikum salaam

**Hussein Omar:** Picture ya kwanza mimi, jina naitwa Hussein Omar Maktar na mimi ni mmoja katika waalimu na nashukuru sana hii referendum ya Constitution kuja kuletwa hapa maanake wakati sisi Wakenya tulikuwa hatuzijui sheria za Kenya, wala hatujui haki zetu. Sasa mimi nitagusia kwa ufupi juu ya wakfu commission.

Wakfu commission ilikuwa ni British Protectorate ambaye ilikuwa kuunganishwa ikawa amalgamated na nchi ya Kenya kutoka Zanzibar na ikaandikwa wakfu commission ambaye ndio itakuwa right na interests za watu walikuwa wakiishi katika upwa huu wa pwani. Sasa katika Cap. 109 iliyoandikwa Langata, utakuta kwamba Wazungu wamekosea kidogo katika ile defination ya waislamu. Wakasema kwamba muislamu ni mwarabu, mwislamu ni mmoja katika makabila kumi na mbili ya waswahili, muislamu ni mkomoro, muislamu ni mwafrika ambaye ana imani ya kiislamu. Sasa hii defination inawatoa waislamu katika nchi hii inawafanya kama wageni na ndio unatarajia mabadiliko yafanyike katika hii defination ambaye nitaitoa baadaye hapa nyuma. Haya makabila ya kiswahili yamekuwa yakiishi katika upwa huu tangu mwaka wa mia nane. Nimeingia hapa kutoka Shugwaya, wameishi wamejenga miji yao wakiendelea na dini yao ya kiislamu. Halafu baadaye, waswahili hawa hawa ambao ndio utamaduni wao 80% ni uislamu. Sasa wakaja watu wengine ambao majirani wa mijikenda pia wakaingia pia katika uislamu. Wanapoingia katika uislamu, ile mila inaonekana ni moja. Sasa ile identification ya waswahili inakuwa inakosekana. Watu wanaona kama hakuna waswahili, na waswahili wako. Pia ile lugha ya Kiswahili ndio lugha imekuwa ikitumika katika Madrasa kama ya kusomeshea hapa Kenya na Central Africa pia. Na waswahili wenyewe katika ile safari zao za biashara, wamekuwa wakieneza hii lugha. Baada ya hii lugha kuenea, wazungu walipokuja, wakaichukua hii lugha, wakaifanya ndio chombo chao cha kutumia katika maslaha yao. Sasa hii haimaanishi kwamba waswahili hawako. Waswahili wenyewe wako na mradi waseme wamekuwa ni wengi, na lugha imekuwa ya kitaifa na waislamu wengi pia hii lugha imekuwa ndio yao wanaitumia. Na hawawezi kukatazwa. Na kwa vile mila ya kiislamu ni universal ni ya kila mtu, huwezi kumzuia mtu mwingine kwamba usitumie mila hii. Sasa wazungu waliona kama uislamu ni kitu kama civilization sio jina. Sasa ndio wakataja waswahili, wakomoro, na watu wengine. Na kwa hivyo hii defination ya kiislamu, hapa mimi uislamu kwanza kwa kingereza ni submission to the will of Allah. Yaani mtu yeyote ni kujitolea kuamini sheria za Mwenyezi Mungu, ndio maana ya uislamu. Yaani

kushuhudia kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu pekee yake. Na pia kuamini vitabu ambvyo Mwenyezi Mungu aliviteremsha kama zaburi, taurashi na injili na mitume wote wa Mwenyezi Mungu ambao walitumwa kuja kuleta ujumbe, huu ndio uislamu. Na muislamu ni mtu yeyote awe mkikuyu, awe mnandi, awe mjaluo, awe mzungu au ni mtu gani, ndio uislamu. Lakini sio hii defination iliyotolewa hapa.

Na kwa hivyo wakati wa kufanya drafting ndio mimi nasema haya makabila kwa sababu yalikuwa under British Protectorate, makabila haya ya kiswahili yaorodheshwe pamoja na makabila mengine arubaine na mbili ya Kenya ambayo yalikuwa yanahesabiwa bila ya upendeleo.

Sasa katika proposal yangu katika hii wakfu commission pia, nasema Chief Kadhi achaguliwe mtu ambaye ana elimu ya secondary school. Na katika elimu ya dini awe amesoma ni graduate, awe na masters degree katika elimu ya dini. Halafu ofisi hii hii ya Chief Kadhi, iwe extended mpaka katika High Court, appeal zozote za kislamu zisikizwe na Maula wa Kislamu wawe ndio wanasimamia katika hizo appeal. Na vile vile nikirudi katika mambo ya vitambulisho, majina ya waislamu kama Omari, Abdala ni majina yameridhiwa tangu zamani. Kwa hivyo isiwe ndio sababu ya watu kukataa kupewa vitambulisho kwa sababu hawana majina mengine kama Katana sijui nani nani. Haya pia ndio tunapendekeza yasifwatwe haya, maana yake haya majina yame-exist hapa tangu katika karne ya miaka mia mbili hasa ukristo ulikuwa haujaingia haya majina yalikuweko. Kwa hivyo sasa ndio tunasema pendekezo hili waisilamu tu-set tukisumbulia. Kwa mfano mswahili ikienda kwa vetting hapa katika kuchukua kitambulisho, anakuaamba haya makabila hayako, na haya makabila yalitajwa katika wakfu commission. Makosa ni ile serikali haikuchukua makabila haya yakawaweka pamoja na makabila mengine kwa sababu walitoka katika nchi nyingine ambayo ilikuwa ni British Protectorate.

Na katika mambo ya uraia mimi nimependekeza pia kama mwenzangu alivyo tangulia kusema mtu yeyote aliye zaliwa katika nchi hii, apewe kitambulisho bila ya kuambiwa aandamane na mama yake na baba yake. Hili jambo ni ukoloni wa kisasa ambao unaletwa ambao hatuutaki. Mtoto yeyote akiwa na birth certificate, apewe kitambulisho bila ya kuulizwa baba wala mama. Kwa hivyo mimi yangu ni mengi nilioandika sitaki kuchukua mda na karatasi zangu ndio hizi hapa ninapeana.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Mzee ujiandikishe kule halafu utupe (inaudible) Dominic Omidi Awuor.

**Dominic Abwuor:** Asanteni sana macommissioner na wananchi wenzangu. Asubuhi ya leo imekuwa ni fursa nzuri.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Sema majina yako.

**Dominic Abwuor:** Majina yangu ni Dominic Ongundi Abwuor ambapo kidogo yamesomwa kwa makosa kidogo, nitarekebisha pale.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Ndio maana yake tunataka uyasema wewe mwenyewe.

**Dominic Abwuor:** Ni kweli. Asante sana kwa marekebisho hayo. Basi nafikiri kwa sababu fursa tumepewa, tutabidi tutumie vilivyo ili tupate kutoa maoni yetu ikiwezekana yajumlishwe katika Katiba ambayo inakuja kutolewa, iwe ni Katiba yetu. Kwa kuanzia naona kwamba, ningepende kusema kwamba kuna vipengele fulani ambavyo vitatolewa hapa ambvyo labda havilingani na mambo ambayo yameandikwa kwenye kile kijitabu cheusi kile, ambacho kina maswali pale. Lakini ma-commissioner wenyewe nafikiri wanajua mahali pakuielekeza. Labda wengi wetu hatujasoma, sasa hatujui ni sehemu gani ya Constitution, basi inatakiwa kurekebishwa lakini wao wataweka mahali inafaa. Nikisema chief…(*sentence incomplete)*

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Bwana Abwuor umekuja kutoa maoni. Toa yale maoni ambayo unayo sasa kutoa. Bila maelezo hayo mengine ya (inaudible)

**Dominic Abwuor:** Basi sawa sawa nafikiri tumeeleweka hapo. Katika utangulizi, preamble ningependa kusema kwamba Katiba ni kitu muhimu sana ambacho lazima kiwe kinalindwa kabisa. Lakini lazima ionyeshe ni mahali gani tumetoka na ni mahali gani tunaelekea ili iwe in bora kwetu, tuwe na hali ya kawaida vizuri sisi kuweza kuzalisha mambo ambayo yatatusaidia katika maisha yetu. Tena naona kwamba iwe tunaweka policy ambayo itatuelekeze katika ku-achieve haya mambo ambayo tunaweka ili iwe inatusaidia baadaye katika maisha yetu. Basi kuhusu Constitution yenyewe ningependekeza kwamba, Constitution ama Katiba ni kitu ambacho ni cha muhimu kisiguswe kila mara mtu akipenda aguse ili ajunufaishe mwenyewe. Iwe ni kwamba Constitution maana yake mambo yanaendelea kuchipuka na kuzidi kuenda mbele, Constitution iwe reviewed ama inaweza kuangaliwa tena kwa mara nyingine baada ya miake ishirini na mitano. Hapo itakuwa ni referendum tena vile tumekuwa hivi, tuulizwe ikiwezekana tutoe ni sehemu gani tunaweza kurekebisha kulingana na mageni yatakuwa yametokea.

Kuhusu uraia, citizenship: Mimi naona kwamba kila mtu aliyoko Kenya ni Mkenya, ni citizen. Lakini ikiwa kuna wale ambao labda wamepata kutoka nchi kwa ajili ya kuoa na kuolewa, basi iwe ni kwamba wanaweza kuoana lakini wapewe cheti ambacho kinasema kwamba hao wako Wakenya kwa wakati huo. Ikiwa labda watatengana na yule ambaye wamepata kumuoa, hiyo contract iishe, yeye arudi kwao kama ni mzungu aliyeoa Mkenya yeye ni Mkenya anapoishi hapa lakini ikiwa kuna divorce kati yao, na arudi kwao, hata ikiwa ni mwanamke arudi kwao. Lakini isemekane kwamba kuna document ya kuonyesha kwamba yeye ni Mkenya ndio lakini as long as hiyo contract bado iko. Na mtoto ambaye amezaliwa hapa awe ni Mkenya na afikishe 18 years ndio aamue kama yeye atataka kuwa Mkenya ama namna gani. Lakini ikiwa baadaye, basi tusiwe na dual citizenship. Mtu ni Mkenya leo halafu at the same time yeye ni Yemen huku. Ah Ah. Uwe ni Mkenya ukitaka kutoka, upewe idhini utoke na vikaratasi vyako vitengenezwe uwache kuwa Mkenya. Ni wewe unatoa maoni.

Halafu kuhusu defense: Naona kwamba Rais awe ni Commander-in-Chief of the Armed Forces kwa sababu haya ni mambo muhimu kabisa ya ulevi. Lakini wale ambao ni wanajeshi wakikosea, wawe disciplined vile wanafanya sasa hivi.

Na kuhusu vyama vya kisiasa: Mimi naona kwa sababu, mimi niko chama fulani bibi yangu yuko chama fulani tunagombana kwa nyumba. Tusiwe na vyama. Let us be party less country. Kusiwe na chama. Hivi kwamba ukabila utatokea, hivi kwamba pingamizi zitatokea katika jamii kwamba huyu ni huku na huku na vita vinapiganwa kila wakati kwa sababu utofauti wa kisiasa. Kusiwe na vyama nchini Kenya. Na hata ikiwa kuna vyama, tusiwe tuna, serikali inasimamia mipango yao kifedha, hapana. Kwamba shirikisho inapewa pesa na serikali, DP inapewa pesa na serikali na hizo ni pesa zetu wananchi sisi. Itumike kutengeneza barabara itusaidie. Vyama haitusaidii popote, haileti chakula kwa nyumba yangu.

Halafu kuenda kwa executive: Naona kwamba executive iwe kuna President ambaye ni ceremonial ambaye atasimamia mambo ya ku, taalima mbali mbali ya kitaifa. Ikiwa kuna sherehe fulani, yeye anaenda kuongoza pale. Halafu awe ni Commander-in-Chief of the Armed Forces. Aongoze army ya Kenya lakini mambo mengine awache. Halafu kutakuwa na yeye awe elected asiwe mbunge, asiwe Member of Parliament kwa sababu hiyo itakuwa ni shida atawakilishaje Wakenya wote na tena constituency yake pale? Halafu Prime Minister pia awe ambaye anachaguliwa not appointed, anachaguliwa na raia. Halafu Deputy Prime Ministers wawe wawili, pia wanachaguliwa. Halafu Vice President pia awe anachaguliwa, makamu wa Rais isiwe kwamba mtu anakuwa appointed, kidogo wanafanya kuzungusha kwa sababu nimeku-appoint kwa hivyo lazima utaimba nyimbo zangu mimi. Halafu ukiingia kwenye executive yenyewe, President hatutaki mtoto awe ni President. President awe ni kuanzia 45 years to 70. Isiwe chini ya hio ama mbele ya hio. Maana yake ukiwa umechukua mtu ambaye ni miaka thelathini, sasa itakuwaje? Wanashughuli nyingi nyumbani, mtoto wake mdogo bado analia anataka maziwa, tunataka mtu ambaye amekomaa. Amewacha mambo ya kulisha watoto. Hata kama ni mama, asiendelee anaenda maternity leave, mama President itakuwa namna gani sasa? Basi iwe ni miaka 45 kwenda na mbele, asha funga kuzaa tayari maana yake tunatarajia siku moja labda mtu akakuwa mama President, si ndio? Sasa nyinyi itakuwaje President ameenda leave halafu legislator ni wale ambao mbwa bunge. Iwe inanguvu kabisa wawe wanakuwa elected for only 5 years, President 5 years, Prime Minister 5 years, miaka mitano, mitano, mitano. Isiwe mtu anatokomea katika uongozi.

Halafu judiciary iwe kwamba kuna wale wanakuwa appointed na Parliament baada ya ku-vet na President ana-endorse. Sasa Prime Minister awe yeye mwenyewe anachagua Cabinet Ministers ambao wasiwe kwamba wanakaa hapo miaka nenda, miaka rudi. Baada ya miaka miwili, re-shuffle, unapelekwa ministry ingine. Lakini after 5 years umekuwa ume-serve kuwa minister, usichaguliwe tena kuwa minister. Uwaachia wengine pia kazi wapate nafasi, tutapata maoni tofauti tofauti, new ideas itapatikana.

Halafu katika local authorities pia kwamba, yule wa kumsaidia Mayor halafu council chairman na deputy wawe wanachaguliwa na raia. Wale wanapata miaka mitano, mitano, pekee yake. Ukisha kuwa Mayor, usichaguliwe tena usisimame tena unataka umayor tena.

Halafu katika basic rights ni kwamba kila mtu ana haki yake ya kuishi vizuri, kuishi mahali popote bila kuhangaishwa. Mtu akipewa kitambulisho hiyo inaonyesha kwamba yeye anaishi mahali fulani asiwe anasumbuliwa kila wakati. Na hiyo

Constitution iwe inatoa ana rights gani, kuabudu, ku-assemble, hata kufanya mambo yoyote bora tu asivunje sheria.

Halafu kwa electrol commission iwe kwamba hawa watu ni watu wenye hekima. Wale ambao wamekua watu wakujulikana ni watu wazuri. Commissioners wawer 14 (kumi na nne) na chairman wao. Wasiwe ni watu wengi ishirini na sita, hamsini na kitu, hao tosha. Halafu wawe ofisini tena miaka mitano. Halafu electrol commission pia iwe kwamba hao katika miaka mitano isewe kwamba wako very active wakati elections inakuja. Wazungushe kila wakati, waangalie boundaries zinakuwa namna gani, mambo mengine pia inakuwa namna gani. Halafu vulnerable groups zile kama wale hawajiwezi, wamelemaa, the disabled wawe wanaweza kuakilishwa vilivyo. At least kwenye kikao fulani cha ku-make decisions, hao wawe wanawakilishwa na a third of the people. Kama kuna watu sitini wakuamua mambo ya kuendeleza nchi, wawe ambao wamelemaa, wale ambao akina mama, wale ambao akina mama, wale ambao labda wanaambiwa ni marginal groups wawe pale a third, watu ishirini wako pale wa kutuwakilisha.

Halafu tena tunasema kwamba resources ambazo ni zetu, ziwe zinalindwa vizuri. Hatutaki forests zetu ziharibiwe kwamba zinapewa watu fulani. Forest ni forest, ikiwa watu wanataka kuishi, waishi umbali wa mita mia moja kutoka forest na hata chemi chemi za maji.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** (inaudible) si una maandishi ambayo utatupa?

**Dominic Abwuor:** Itakuwa baadaye.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Ndio lakini dakika zako zimekwisha.

**Dominic Abwuor:** Haya basi. Wale civil servants, wawe wanaweza kulipwa vizuri lakini kiwango cha tofauti za job groups na mishahara isiwe iko juu ili tu-avoid ma-strikes. Migomo migomo ya kila wakati, iwe ni fair. Halafu constitutional commissioners ni wale watu ambao wanakua pale for 5 years only. Baada ya hapo tukitaka ku-review Constitution after 25 years pia, wawe wanachaguliwa tena. Transfer of power mtu akisha chaguliwa President iwe ni two weeks after matokeo kutolewa a assume ofisi. Yule wa kwanza alikuwa ametoa tayari vitu ametumea vya serikali ametoa miezi miwili kabla ya elections kufanywa. Asante sana kwa kunisikiza.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Jiandikishe kule na utuachaie maadishi na uwache kidole. Tafadhali ningali-time na ningewaomba kwamba, mtumie mda mchachae. Nikikuamba mda wako umekwisha, umekwisha. Ningalipenda mkija hapa (inaudible)wakati tu. Ikiwa wewe unamaandishi sisi tutasoma. Mulika tu maneno makubwa makubwa. Na kama fulani amesha sema juu ya neno fulani, wacha na wewe kulirudia rudia, ni kitu ambacho tumesema na tumeelewa. Anayefwata ni Antony Karisa. Antony unamaandishi? Kwa hivyo tumulikie mawili matatu. Kwanza useme majina yako na uanze mara moja.

**Antony Karisa:** Mimi kwa majina naitwa Antony Charo Karisa kutoka (inaudible) Youth Group. Nilikuwa na maoni kidogo hapa kama manne hivi. Ya kwanza ni kuhusu employment, ya pili ni human rights, mtanisamehe kidogo kwa sababu niko na mafua.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** (inaudible) kuna wengi wanao ongea ongea ongea. Ikiwa unaneno na mwenzako utoke nje muongee. (inaudible)

**Antony Karisa:** Ya kwanza kabisa ni kuhusu employment, na ya pili ni human rights, la tatu ni water and power supply. La nne nikuhusu education. Sitasema kwa urefu kwa sababu mengi nimeandika hapa. Nitafanya kugusia.

Kuhusiana na elimu: Ningependekeza ya kwamba serikali iwe inaweza kutoa elimu ya bure kuanzia nursery mpaka darasa la nane. Jukumu la wazazi liwe ni kalamu na uniform pekee yake. Vitabu na elimu iwe bure ili kwa wale pia hawajiwezi, waweze kupata elimu.

Lingine ni kuhusiana na employment: Nafikiri serikali ingetoa sheria thabiti kuhusiana na mambo ya uwajiri. Kama ku-retrench watu wangekuwa wanapunguzwa kazi ambao labda amehudumia kampuni hio ama shirika hiyo kwa zaidi ya miaka kumi na mitano kuendelea. Sio mtu amefanya kazi miaka miwili na anafukuzwa kazi ikiwa kuna watu ambao wako na service ya over 30 years.

Lingine pia wapewe sheria kwa sababu siku hizi ni kampuni chache ambao wana-employ watu permanent. Siku hizi ni contract, ikiisha contract una-renew na mwishowe unatoka kitupu. Hata kama umefanya miaka arubaini, hakuna lolote utapata. Kwa hivyo pia wapewe sheria ya kwamba kama wanaajiri, waajiri watu permanent wakisha-serve zaidi ya miezi sita na kuendelea.

Lingine ni kuhusu human rights. Kuhusiana na swala la vitambulisho, ni wengi wamejishugulisha kutafuta vitambulisho na wameshindwa kupata kulingana na sheria zilizowekwa ambazo zimefinya watu wengi. Kwa sababu, tuchukulie kwa mfano inasemekana mtu kupata kitambulisho lazima awe na birth certificate au school leaving certificae au baptisimal certificate. Na awe na kitambulisho cha mzazi mmoja either mama au baba ambapo ni ngumu kwa wengineo kwa sababu wengine waliachwa wakiwa bado ni wadogo, na hawakuweza kuona vitambulisho hizo, na wala hakupata elimu, na kuna wengine ambao kufikia sasa hawajui dini ni nini. Hawajafika kanisani wala msikitini. Hawezi kuwa na makaratasi kama hayo. Kwa hivyo baadhi ya sheria zile zimewekwa ili mtu apate kitambulisho zipunguzwe. Mtu akifikisha miaka kumi na minane apate kitambulisho bila maswali mengine.

Kuhusianan na swala la moto na maji: Ningependa serikali iangalie hili swala sana kwa sababu kusema ukweli, kuna vijiji vingine ambavyo ukitaja kuhusu maji ya mfereji ni kama ndoto. Una zaidi ya miaka ishirini bado hajaona maji ya mfereji. Kuna kwingine ambapo stima pia ni kama ndoto kwa sababu wengine wamesomea kazi hizi za jua kali na wametegemea kitu kama

stima. Sasa kama hakuna stima hiyo ni kumaanisha ya kwamba nafasi za kazi zimepungua. Sina mengi ni hayo machache.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante kijana. Unaweza toa makaratasi yako kule na ujiandikishe. Anayefuata ni Bwana (inaudible) Sisi tutaendelea. Anwar (inaudible) Anwar unamaandishi?

**Anuwar Abaye:** Ndio.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Nataka tu umulike, nakupa dakika tano za kumulika yaliyomo.

**Anuwar Abaye:** Asante sana.

**Com. Salome Muigai:** Sema majina yako.

**Anuwar Abaye:** Majina yangu ni Anuwar Abaye wa kikundi cha Kisauni Youth for Development. Ingawaje kuna maandishi, lakini naomba uniwachie hizo dakaka tano nifafanua kitu hapa Bwana Commissioner.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** (inaudible)

**Anuwar Abaye:** Kuna kitu Katiba. Kuna kitu act of Parliament. Kuna kitu Presidential directive, policies finally tunakuja law and order. Katiba yetu ya Kenya ambayo ni hii, nilisoma vizuri na nikaielewa, hii hapa. Halafu kuna hiki kijichabu ambacho commissioners wamekitoa, mwongozo ili tujaribu kutoa maoni. Lakini at the end of the day, nilikuja nikakuta ya kwamba, things get distorted where the implementations, wakati wa kutekeleza, kwa sababu nikisema hivi tukisoma (inaudible) Katiba, act of Parliament na kila kitu, law and order, the police force, the judiciary ndio mara nyingi wana-fail the community.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Wewe toa maoni.

**Anuwar Abaye:** Natoa maoni. Bwana commissioner itakuwa unatoa centiment halafu maoni because maoni inategemeana na what is there. Okay. Kwa mfano nikija katika, kwanza wacha nianze na ardhi halafu ndio nifikie hapo. Ardhi ya Kenya, tunaomba Katiba ambayo tutatengeneza leo impatie kila mwananchi hata kama ni kipande kidogo cha ardhi ya Kenya.

Mbili, natural resources: Tungependekeza ya kwamba natural resources zitumiwe kikamilifu na wananchi kuliko kuyapeana natural resources kwa government. Na tukifika where ambapo kwamba sasa implimentation inakuwa shida na wakati wa kwamba, wakati wa police force anatekeleza sheria inakuwa kwamba mwananchi wa kawaida hapewi nafasi ya kujitetea. Kwa hivyo tunapenda police force iwe strengthened kwa viwango kama, yaani wapewe mafundisho zaidi wasome mambo ya human rights, wawe trained kujua mambo ya treatment of women suspects and women victims, torture of suspects by police officers to be taken as a crime, Section 387 one of the criminal procedure code states that any police officer who kills should be

suspended pending investigation. Tunaomba hiyo katika Katiba yetu pia itiliwe mkazo sana. The use of maximum force to the community. Katiba yetu pia isaidie fafanua hiyo. Childrens act. Katika Childrens Act juzi imepitishwa kwamba watoto wapewe elimu ya bure na mambo kama hayo. Mtoto kuwa na raha, ni mzazi wake awe na raha. Mzazi ana raha, mtoto atawezaje kupata security? Kwa hivyo first of all tunaenda kwa mti kabla hatujafika kwa tunda. Bwana Chairman, katika historia ya Kenya, kuna mambo ambayo hatujazingatia ambapo katika Katiba sijui hayakuweko kwa sababu gani. Kuna wale waliopigania uhuru wa nchi hii. Bwana Chairman, ni aibu ya kwamba wengine wao mpaka sasa, maisha yao ni magumu sana. Wale ambao hawana ardhi, hawana maisha mazuri ya kwamba wanaweza kuishi. Kwa hivyo tunapendekeza ya kwamba, wale ambao walipigania uhuru wawe honoured. Singependa kuendelea sana kama vile ulivyonishauri kwa sababu hii article imeandika kila kitu. Thank you very much.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Nakushukuru ndugu Anuwar. Unaweza kuleta hayo maandishi yako hapa na pia uweke kidole. Na (inaudible) keti hapo, unamaandishi? Tumulikie pia (inaudible)

**Bwana Nzori:** Jina langu naitwa Bwana Nzori mwakilishi katika kisauni lands lobby group. Mimi nitazungumzia kuhusu mambo ya wakfu. Kwanza nitaanza na interpretation. Ningependelea iwe katika interpretation iwe muislamu, a muslim should be, it should read, a believer of islam faith ndie awe ni muislamu sio itaje muislamu kwa kabila. Vile iko muislamu. (*sentence incomplete)*

Adminstration nasema every work made by for any muslim should be administered by muslim. Hii administration nataka iwe na waislamu wenyewe wakiihudumia you know work. Halafu si nazungumzia kuhusu Constitution work commission ambayo huwa iko na members wanane. Ningependelea katika hawa members wanane, ikiwa kama member wa kwanza ni PC basi badala akuwe awe ni automatically awe in PC, awe ni lazima PC huyo awe ni muislamu ama kama si muislamu, awe ni DC lakini awe hapa kuwe na muislamu vile vile. Ya pili awe ni Chief Kadhi ambaye chief kadhi mwenyewe amekuwa appointed tena na waislamu. Mtu wa watatu awe ni scholar, msomi wa kiislamu vile vile. Na watano wengine ambao wamebaki kukamilisha wanane, nataka wawe wanachaguliwe na panel ya scholors ya wasomi wa kiisalmu wapitishe hawa watu wanane kuwa hawana hitilafu yeyote. Halafu D, nazungumzia period of office, mda wa hawa watu kukaa kwenye wakfu. Napendelea iwe miaka mitatu lakini anapotoka nje, asionyeshe uadilifu katika hayo mambo, awe aweza kukatizwa wakati wowote.

Halafu E. power, uwezo: Nazungumzia wapewe uwezo wa kuweza kushtaki na wao pia waweze kushtakiwa. F. Nazungumzia kuhusu register of property. Zile wakfu ambazo zimeandikishwa kule (inaudible) na nafasi mtu yeyote anapokwenda kule anaweza kupata ile file na kuona ni vitu gani viko kwenye wakfu. Isiwe vitu vile vinakuwa confidential. Viwe katika kila areas ambapo wakfu inasimamia iwe watu wanaweza kufika na kuona vile vitu viko. Kwa hapa naona niko na haya a mpaka f.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** (inaudible)

**Alice Malanga:** Kwa jina naitwa Alice Malanga natoka Maendeleo ya Wanawake.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Maranga, Malanga?

**Alice Nananga:** Nananga. Ni N si R.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** (inaudible)

**Alice Nananga:** Mimi pendekezo langu la kwanza ningependelea kila police station kuwe na women desk. Na kuwe na special attendant ambaye atakuwa akishughulikia mambo ya wanawake, watoto, kwa mfano kunajisiwa, domestice violence. Tunaona kwamba hawa wanawake wanasumbuka sana kwa issues kama hizo.

Pendekezo la pili ni kwamba kuwe na special judges na special lawyers for women kwa koti zetu ambao pia watashughulikia mambo ya divorce, divorce cases. Kwa jumla kuwe na ofisi ambayo itashughulikia mambo ya wanawake in case of divorce, and any women issues na pia kuwe na judges na lawyers wa wanawake pekee yake.

Pendekezo la tatu ni kwamba kwa mfano kama kukiwa na divorce, yule mwanamume awe atashughulikia wale watoto kwa upande wa elimu na mahitaji na mambo ya basic needs za maisha. Si mtu a divorce na bibi yake halafu mwanaumu apotee mwanamke aachwe na watoto akihangaika na watoto. Kwa hivyo yule mwanamume awe responsible na wale watoto kwa basic needs zao.

Pendekezo la nne ni kwamba ikiwa msichana amewekwa mimba na kijana, na yule kijana amekataa responsibility, yule msichana angojewe akizaa yule mtoto yule mtoto awe tested blood group. Ikiwa blood group ni ya yule kijana, basi yule kijana awe atalazimishwa kuwa responsible na yule mtoto. Ikiwa hana kazi yule kijana, wazazi wa yule kijana wawe responsible na yule mtoto. Tumeona wasichana wengi wanawekwe mimba halafu mvulana anakataa na ni yeye kweli lakini kwa vile hakuna evidence, msichana anabaki pekee yake akihangaika na yule mtoto na itakuwa yule msichana atakuwa ameharibikiwa maisha.

Pendekezo la tano ni kwamba kila district kuwe na kiti kimoja cha wanawake. One parliamentary seat in every district ambayo itakuwa ni representation ya mwanamke kule kwenye bunge. Tumeona kwamba kwenye bunge kuna maswala ambayo pengine kutakuwa na elections halafu kwa vile wanawake ni kidogo, hizi issues za wanawake hazipit kwa hivyo tunaonelea katika kila district Kenya kuwe na kiti kimoja cha wanawake.

Pendekezo langu lingine ni kwamba wakati wa kura tuna wanawake ambao wako na mimba, na wengine wanateseka wanapiga pia mlolongo na huku wakiwa wanapata shida sana. Hasa nimependelea wakati wa kura, pregnant women and women with

children ama watoto, wapewe first priority. Akionekana ni mwanamke yuko na mimba ama ana mtoto anapitishwa mbele anaende kupiga kura anaenda nyumbani. Si nayeye ako na mimba yake anasimama kwa laini mpaka afike ama pengine ako na mtoto, mtoto anamsumbua mpaka lazima asimame kwa laini, hiyo wanawake tunaona wanasumbuka sana.

Halafu Pendekezo langu lingine ni kwamba hii anti-corruption (*sentence incomplete)*

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Ngoja kigodo. Huko nyuma mjue tuna-record mambo hapa. Tafadhali mazungumzo ya huko yakome. Endelea

**Alice Nananga:** Anti-corruption unit. Mimi kwa maoni yangu naona kwamba haiko kwa police sector kwa sababu tunaona katika mabarabara yetu mapolisi wanasumbua matatu, wanatoa kitu kidogo na sisi wanaraia tukiona. Na tunasikia kwamba kuna anti-corruption unit huko kwa serikali ambayo naamini kwamba labda huko kwa police sector haifanyi kazi. Sasa nilikuwa nasema, sisi raia tupewe uwezo ikiwa tumeona vile na tunajua kwamba it is illegal, turuhusiwe kuchukua numba za wale polisi sisi wenyewe tuweze kushtaki, kuwashtaki wale polise ambao wanafanya hivyo. Lakini tunaweza kushtaki ikiwa hakuna njia ambayo tunaweza kutetewa sisi wananchi, basi, hali ile itaendelea lakini inatuchukiza sana sisi wananchi kuona polisi wanachukua hongo hovyo hovyo njiani. Matatu haina shida yeyote lakini lazima atatoa mia pale ama mia mbili ambayo si sawa. Kwa hivyo sisi raia tunapendekeza tupewe uwezo wa kuweza kushtaki polisi kama wale.

Halafu la mwisho ambalo namaliza ni kwamba hii Constitution tukiandika hivi, itakuwa haina maana yoyote. Lazima Constitution ikiisha iwe the public should be educated on the Constitution kwa sababu nasema hivi ni kwani, sisi wanawake tunajua kwamba it has been legal for women to inherit properties from their fathers. Ni haki kwamba mwanamke amepewa uhuru wa kuridhishwa mali na mzazi wake. Lakini wananwake wengi hatujui, bado hatujajua hivi. Tunaona labda wale wanaoridhi mali ni wanaume tu pekee yake. Kwa hivyo nilikuwa nasema kwamba ikiwa Constitution imeisha, hii Constitution iwe itaelimishwa kwa wananchi wote, wananchi wajue Constitution inasema nini. Ili kwa kipengele kama zile kusiwe na matatizo. Hata hivi leo bado watu wengi ama mababa wengi hawawezi kuridhisha mwanamke mali yake kwa sababu anaona kwamba ni illegal lakini ni kwamba hii Consitution tukiimaliza baada ya yote iwe itakuwa educated to the public. Asanteni.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** (inaudible) Nimetaka kuuliza kuna mama yeyote hapa ambaye ni mja mzito ambaye hatutaki afinywe hapa na watu? Kuna mama yeyote? Kama uko inua mkono nikuite uje utoe maoni uende. Basi hakuna mama. Alice Nananga hakuna mama yeyote hapa ambaye ni mja mzito kwa hivyo tutaendelea jinisi ilivyo. Salma Salim. Anapoendelea kuja nataka James Mukala awe tayari. James Mukala yuko? Basi uwe tayari huyu mama akimaliza, zamu ni yako.

**Salma Salim:** Mimi naitwa Salma Salim kutoka hapa Bamburi, Mlaleo. Maoni yangu niko nayo ni mengi lakini nitasema kidogo, yale machache kidogo. Niko na maoni kama haya.

Nataka Chief Kadhi achaguliwe na Muslims scholars. Ya pili alipwe kama vile anavyolipwa attorney general. Na tuwe na koti ya rufani ya kiislamu. Na tuwe na womens desk huko kotini. Tupewe womens desk ambako wanawake watapeleka maoni yao wasikilizwe. Tuwe na polisi wanawake wakufanya searching wanawake upande wa rapping pia, tunataka ichukuliwe hatua kali anayefanya raping mwanaume.

Bunge tupewe 30% wanawake, 10% vijana, youth hao, na 10% tupewe disabled. Prime Minister awe mwanamke na awe amesoma na awe amechaguliwa na raia. Mayor achaguliwe na mwananchi sio councilor. Twataka majimbo hapa coast. Usquatter wa hapa coast tunataka uishe kabisa. Kila mtu apewe titile deed hapa sababu sote hapa no masquatter na hiyo tunataka iondolewe kabisa. Vyama viwe vitatu kama maoni yangu vyama viwe vitatu na viwe vinatumika sawa kipesa na (inaudible) usawa. Isiwe ati chama kimoja ndio kitakuwa kimeshikilia tu vingine vyote viko chini vimekanyagiwa.

Vitambulisho viwe vimepewa mwananchi wa Kenya yeyote yule ambaye ni wa Kenya amekaa Kenya apewe kitambulisho. Pesa za coast zitumike hapa coast pekee yake. 10% ndio kama inataka kutolewa nje, watoe 10% tu itoke nje iende ikazaidie huko nje. Asanteni.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante. Mama uende hapa, hebu jiandikishe. Huyo alikuwa Salma Salim. Sasa James Mkala. Tafadhali tuwe kimya James Mkala atoe maoni, unamaandishi?

**James Mkala:** Naam niko nayo.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Basi umulike juu ya maandishi kwa kifupi.

**James Mkala:** Kwa jina mimi naitwa James Mkala kutoka (inaudible) Ninashukuru sana commissioners na wote mliofika ili tushirikiane kutoa maoni yetu. Kwanza ningeanza kuongea kuhusu mambo ya shamba, ama sheria za mashamba.

Sheria za mashamba hapa Kenya sisi hatukutunga, zilitungwa na wazungu ndio tukaletewa ili wao waweze kufaidika. Wachume hapa wakipeleka kwao mali wakifaidika. Na sheria, Katiba ya Kenya ilitungwa kule Lancaster na waafrika kidogo. Kama ingekuwa ni watu wote kama vile ambavyo inafanywa saa hii, watu wote wanahusishwa, wanatoa maoni yao, *(sentence incomplete)*

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Hayo tunajua, sasa wewe tupe maoni.

**James Mkala:** Sasa mimi kuhusu haki za uraia. Kila mwananchi ambaye amefikia umri wa miaka kumi na nane, apewe kitambulisho, apewe na Katiba yake. Serikali itoe Katiba ili yule mtu ajue kama ni makosa anafanya, iwe ile Katiba inamuhukumu mwenyewe. Na kuhusu mashamba, watu, yaani mali yote shamba yote iwe mali ya uma sio ati ni Rais ndio

anayetoa ardhi. Yaani tunataka mtu wa, kama ni mtu wa bara amiliki ardhi bara, mtu wa pwani kwao ili kila mtu awe ana haki sawa. Maana yake utapata mahali kwingine watu, mtu amezaliwa pale, babu yake amezaliwa pale lakini hana ardhi, inasemekana sijui mtu fulani kutoka mahali kwingine yeye ndie ana acre mia tatu, na yule mtu wa pale hana. Kwa hivyo tungeomba hii Katiba iweze kuangalia maswala kama haya. Naona ni hayo tu.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante. Unaweza kutoa haya maandishi yako kule na ujiandikishe. E.K. Ngutu. Ngutu anapokuja nataka John Mcharo awe tayari. Okay chukua nafasi, na Mcharo yuko? Okay akimaliza itakuwa wewe.

**Ephantus Ngutu:** Kwa majina naitwa Ephantus Kathanka Ngutu. Mimi maoni yangu ni kuhusu wizi. Wizi umeongozeka sana katika nchi hii. Na mimi nilikuweko wakati wa mkoloni mpaka uhuru tukapata, lakini kwa wakati huu ambaye ni wa uhuru, wizi umeongezeka sana. Mimi kwa maoni yangu, ninaonelea, watu siku hizi wanapora mali ya uma, pesa za uma, zinaibwa na watu wawili ama mtu mmoja. Mamilion ya pesa. Mtu yule anapopelekewa mashtaka, badala ya kupelekwa rumande, anaruhusiwa kuweka bond. Anatoka, sasa anaenda kutumia zile pesa kuweka mawakili mpaka kesi yake itakapoisha. Akipatwa na hatia, anafungwa kama miaka miwili, anakuja anaanza kutumia hizo pesa za uma. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba kama mtu anahusika na kuiba pesa za uma, asiruhusiwe kuweka bond. Siku hizi utaona mtu akiwa na pesa anaweza kumyanganya mtu ambaye hana pesa mali yake. Na atamnyanganya kwa njia gani? Yeye kwa vile ana pesa, atamwekea yule mtu hata mawakili kumi. Na yule maskini hana pesa, ama pengine ni shamba lake na shamba hilo, ni hilo hilo analo na atanyaganywa na yule mtu ambaye ana pesa. Kwa hivyo katika Katiba hii ambayo tunaiita ni ya Mwafrika maanake hii ilikuweko, hiyo ilioko sasa ni ya kizungu, kuwe na sheria kwamba iangaliwe. Ikiwa mtu hana uwezo wa kuweka wakili, na yule ambaye wanashtakiana naye asiruhusiwe kuweka wakili, wangangane kwa sababu sisi ni waafrika na tukiwa waafrika, tumeiga sana mpaka ikawa mambo yetu yote tumebakia ngozi tu. Sasa hawa watoto wetu hawa, wamebakia ngozi tu. Hayo mambo mengine yote ni ya kizungu. Kwa hivyo mtu kama huyo na yeye asiruhusiwe kuweka wakili, wangangane. Wangangane bila wakili. Mimi sina mengi ila tu nawachia hapo. Asanteni.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante sana mzee. Ende kule ujiandikishe. Next atakuwa John Mcharo na John Mcharo anapojitayarisha nataka Salim Mwambala awe tayari. Unamaandishi?

**John Mcharo:** Ee kidogo.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Kwa hiyo tumulikie.

**John Mcharo:** Nina maandishi kidogo. Kwa jina naitwa John Charles Mcharo na nataka kuzungumzia mambo manne tu basi. Memorandum yangu ni kizungu lakini pale nitakapoweza, nitajaribu kueleza kiswahili. Kwanza nataka kuzungumzia ofisi ya Rais halafu nitazungumzia kuhusu polisi, halafu nitazungumzia kuhusu serikali za wilaya yaani local authorities, halafu mwisho, nitamalizia na one or two general social issues. Kwanza nitaanza na ofisi ya Rais.

Tungependa hii Katiba mpaya ambayo inakuja iwe ita-treame down powers za President. Sisi tuliridhi Constitution kutoka kwa wazungu ikiwa ni nzuri. What happened is, ilipokuja hawa President wawili ambao tumewapata tangu tupate uhuru, kila President alioingia pale amejaribu sana kujifanya very powerful. Sisi tungependa, President wa Kenya asiwe ndio mambo yote. President apewe powers za kutosha za ku-run office of the President lakini asiwe yeye akisema leo hivi, iwe hivyo hivyo yaani sisi hapa vile tuko na culture ya kuwa President akisema shamba hile lipewe fulani anapewa, lile shamba si la President pengine mi mali ya uma na yeye hana ruhusa kumpeana rafiki yake kwa sababu yuko chama kimoja nayeye aseme ni lake. Twataka President apewe nguvu za kutosha just enough to run his office. Asiwe yeye ndio mambo yote.

Kuna Presidential appointments. Hii Kenya yetu inasifa mbaya kwa sababu utakuta heads of parastatals wale ambao wanachaguliwa na President, cabinet ministers, permanent secretaries ni watu ambao wanatoka sehemu mmoja. Ni President mwenyewe akifurahi na wewe kwa kuwa wewe uko chama hiki, anakupa ile kazi. Hata kama haukusoma, hata kama ile kazi hauiwezi, unakuta mtu analetwa ku-run KBA lakini hata hajui shipping ni nini. Unakuta mtu anachukuliwa ku-run a forestry department lakini hajui hata forest conservation ni nini. Sasa tunataka Presidential appointments zote ziwe vetted na Parliament. President akisema anamtaka huyu, awe mkubwa wa posta iende bunge kwanza. Tuangalie aweza ku-run posta ama hawezi. Ikiwa hawezi, ikipitishwa hawezi aambiwe huyu mtu wako hawezi, chagua mtu mwingine, hiyo namna hiyo. Lakini si ati akisema leo inatangazwa kwa saa saba KBC halafu ndio hivyo. Hata kama ni mtu mjinga amepewa posta ndio maana haya mashirika yetu yameanguka.

Sasa nataka kuingilia hukumu ya kifo. Hii hukumu ya kifo tungependa iondolew mbali. Na nikama imeondolewa maanake hakuja nyongwa mtu tangu mwaka wa themanini na sita sijui themanini na saba. Wale wote ambao wamehukumiwa kifo tangu mwaka themanini na themanini na saba, wanaoza kamiti, shimo na hizi jela zingine. Ni vibaya sana kwa sababu yule mtu yuko na thiki sana. Kama ulihukumiwa kifo mwaka wa themanini na sita, hujui kesho ndio ntanyongwa ama ni kesho kutwa ama ni wiki ijayo. Unakaa miaka kumi na tano wondering when I will be executed. This is very bad. Sasa huyu mzee hatujui kwa nini hajasema wale watu wanyongwe. Lakini kama ni kuwasamehe, awaambia nyinyi mmesamehewa, hukumu yanu sasa si kifo, hukumu yenu ni mfungwe maisha gerezani. Inakuwa relief kwa yule mtu. Na ipitishwe bunge kua hii hukumu ya kifo iondolewe. Tuliiridhi kutoka kwa wazungu, wazungu wenyewe waliifutiliwa mbali, sisi bado tuko nayo na it is very barbaric, we in the 21st century, we should not have the death penalty.

Provincial administration: Kulikuwa na ninio kuwa police administration iodolewe. Tusiwe na PC, tusiwe na DC, tusiwe na DO, tusiwe na Chief. Lakini wale walikua wakipiga vile vilio hawakutwambia ati akiondolewa DC, akiondolewa PC kuwekwe nani. Kwa vile hatujui mpaka sasa, nani anaweza kuwekwa, zile ofisi zibaki vile vile lakini, ziwe kazi za PC ziko clearly defined, kazi za DC na DO ziwe clearly defined. Kazi za Chief hasa huyu Chief ziwe clearly defined. Sisi hatujui kazi ya Chief mpaka ya leo. Ukifika kwa Chief uko na kesi yako anakwambia leta mbuzi, wewe uliyeshtakiwa ulete mbuzi, yule aliyeshtaki alete mbuzi, ndio kesi yenu isikizwe. This is very wrong. Mimi naona huyu Chief hatukatai awekwe pale lakini tuambiwa Chief kazi

yake ni A, B, C. Chief haruhusiwi kuchukua pesa za harambee, Chief haruhusiwi kusikiza kesi ambayo inayoweza kwenda mahakamani, Chief haruhusiwi kusema wewe fanya hivi, kutoa instructions. Mambo ambayo yangepelekwa kotini, Chief anatoa judgement yake pale pale kwa kua amekula mbuzi mbili zimekuja, we should not have this in the Constitution. If the Chief has to be there, we should know exactly what the Chief is supposed to do. Akija akiniitisha mbuzi, nimwambie sikupi mbuzi, nataka unifanyia kazi yangu, mtoto wangu anataka kitambulisho na hupati mbuzi na hupati pesa za harambee.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante. Umebakisha dakika moja tu. Moja tu kwa hio ona vile ambavyo (inaudible)

**John Mcharo:** Haya Police. Mimi ningesema polisi wapewe mshahara mzuri na pia wachukulie polisi waliyo soma. Saa hizi tuna polisi hawakusoma, mtu hakusoma amepewa bunduki, wanatuonea sana huku mitaani. Na ningetaka Mayor achaguliwe directly by the people. Na Mayor awe amesoma, amefika form four na ame-pass. Sio amefika form four na amepata E. Na mambo ya burials permit, wedding permits. Sisi tuko na matanga, tuko na mwili pale polisi wanaingia wanasema iko wapi permit. Permit ya nini unatuona tunalia na mwenzetu ndio yule pale amefariki? Harusi. Unaona bwana harusi na bibi harusi wako pale, polisi wanaingia wanasema lete permit. Permit ya kazi gani kwa shughuli kama hizi? Hatungependa mambo ya permit katika shughuli ambayo they are so obvious kama matanga na harusi.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Thank you.

**John Mcharo:** I am not even half way.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Kuna watu wengi ambao wangependa kuongea na kwa hivyo lazima tuwe fair. Unaweza kwenda kule ujiandikishe na utupe maandishi yako. Omar Yahi. Endelea, sema majina yako na uendelee.

**Omar Yahi:** Mimi ni Omar Z. Yahi. Maoni yangu kwa Tume hii ni kuhusu KWS ambayo inatunyanyasa sisi wananchi wa hapa na tunaona inatudhulumu sana. Nikisema hivi kama mimi nina port yangu kule na-chargiwa 400/= per person na KWS. Na mimi namcharge mgeni shilingi mia nane. Wakichukua mia nne nimebakishwa na mia nne. Mia nne ile nitatoa commissioner 150 kwa (inaudible) nikabakiwa na 250. 250 nimlipe captain wangu 30% na ninunue mafuta, na nilipe nakruu, nikishtuka mimi nimebakiwa na (inaudible) KWS na sijui pesa zinakwenda wapi. Nawanachukua mamillion ya pesa kule, na sisi wananchi wa pale tumezorota, kulikuwa kuna ma-boat karibu arubaini, sasa zimebakia kama boat nne. Nyingine zimeoza zote. Nataka (inaudible) zaidi ya mia moja, sasa zimebakia kama kumi. Naona hapa tutaomba mtufikirie sana sisi wananchi wa hapa tunaponyanyaswa na KWS na hajui kitu chochote pale kuja kwake anakwita kama jibwa. Wakati umechukua mgeni ukija, yeye yuko juu huku anafanya kukuita, we kuja hapa. Unampelekea pesa za bure, na hawana heshima wala hawana (inaudible) vibaya sana. Kwa hivyo naomba maoni haya mwakilishe kwa makini maanake tuko katika hali mbaya, tumeshindwa kujimudu sasa kimaisha. Pesa zote zinaliwa na KWS na hatujui zinakwenda wapi. Ninaushaidi huku wakutosha si pesa kidogo, mamillion ya pesa wanachukua. Sio kama mimi kwa port kwa mwaka napata tisaini na tano elfu.

KWS nailipa 1.5 million. Mimi mwenye board napata 96 thousand. Sasa hii naona haitakuwa fair. Kwa hivyo naona maoni kwanu nyinyi ni haya.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Ngoja kidogo mzee. Niwapi huko mzee ambapo (inaudible)

**Omar Yahi:** Marine Park wanatucharge. Upande wa Mombasa beach.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Mombasa beach. Na ile ya boat (inaudible)

**Omar Yahi:** Ile ya boat wacha boat mpaka madawa yale canow. Ukibeba mzungu tu unalipishwa 400/=.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Na ni official payment ama ni kawaida ama ni nini, hakuna receipt unayopewa ama?

**Omar Yahi:** Mimi naona hata zile receipt sio za haki.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante mzee unaweza kuja kule ujiandikishe. Sasa ni Bwana Mwambala. Na Bwana Mwambala anapokuja, nataka Aggrey Kilo awe tayari.

**Salim Mwambala:** Asante sana Bwana mwenyekiti kwa kunipa fursa hii. Kwa jina naitwa Salim Mwambala. Hasa ningependa kuzungumzia swala la Katiba. Ninawakika watu wengi sana mitaani hawajui mambo ya Katiba yatakayobadilishwa wapi, Katiba yawaathiri vipi, wao wanaabiwa waje watoe maoni hali ya kuwa hawajui ni wapi wanagusa. Kwa hivyo serikali ingefanya mpango wa kuwa, japo mara mbili swala la Katiba lingekuwa latangazwa. Watu wanfanya kuelezwa kwamba katiba yetu yasema hivi, kipenge hiki chasema vile, watu wapate kuelewa kwamba Katiba ya Kenya iko hivi na inamsaidia raia wake hivi na inamumiza hivi. Ndio pale watu wakija kaa wakiamua wajadili Katiba, watakuwa wanajua wanazungumza kitu gani.
Swala la pili ni hili la uwandikishaji wa kura. Swala ya uwandikishaji wa kura ingekuwa ni ubora pale mtu anapochukua kitambulisho, apewe kabisa kadi yake ya kura. Hino itazuia mambo ya kuchukua watu kutoka mji mwingine kuja kuwaleta waje kuchukua kura, ili yakua wakupitisha na hali ya kuwa wao si wakaazi wa pale. Na katika swala hili litakuwa pia linapunguza gharama na kwamba kila mwaka ikifika wa kura, inakuwa mpaka lazima (inaudible) wa commissioner kuandikisha kura, inakua ni pesa zingine zinatoka kwa serikali kuwalipa wale, na hali ya kuwa ni tax tunalipa sisi wananchi. Tunaumizwa kwa kila kitu.

Swala la tatu ni hawa raia wa makaratasi. Citizens by papers. Hawa citizens by papers tunaona kama nchi kama America vile, wao hawaruhusiwe kupiga kura wala kuchukua kura. Ningependekeza na hapa kwetu swala hilo pia liwepo maana yake hawa ndio wanakuwa na influence ya kutuumiza sisi kimawazo, kifikira na kihali ya uchumi kutokomana na nguvu zao za senti.

Na swala lingine ambalo ningependekeza ni kwamba hao wanao gombea ubunge. Lau mtu amepata term yake ya kwanza a serve term mbili pekee yake. Yaani kipindi cha miaka kumi. Baada ya miaka kumi ile, haruhusiwi tena kugombea ule ubunge kwa sababu atakuwa akili yake sasa imesha zorota kimaendeleo. Atakuwa sasa ni mtu wakujinufaisha matumbo yake na kugandamiza wananchi. Hakuna mmoja atakalofanyia. Mfano mzuri twaona Mvita huko.

Na swala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni ile wazungu wasema *"justice delayed, is justice denied"*. Serikali yetu kwa hakika ina senti za kutosha. Na hapa kutokana na kwamba ina senti za kutosha, ingeongeza idadi ya mahakimu, hawa magistrates, wangeongezwa wakawa wengi, na kukawa na transparency ya zile kesi. Sio mtu yule askari anashika, amemuona kabisa akitoka dukani amuuliza watoka wapi na waenda wapi. Si unaona mimi natoka dukani naenda nyumbani. Swala kama lile lirekebishwe kwamba yule mtu akishikwa akipelekwa kotini, atakuwa ni mtu (inaudible) wanakwenda pale, wanazungumza kesi yao, kama ni mashahidi anawaita, siku ile ile mashaidi wao wanazungumza kesi ile. Ikifika kwamba amehukumiwa kufungwa, anakwenda kutumika kisawa. Sio kwamba anakwenda kuhukumiwa kwa kwamba amegandamizwa. Tunaona sera hii inatumika Uganda, na sera hii pia inatumika Tanzania. Kwa nini Kenya tusiitumie?

Na swala lingine ni hili swala la mapolisi. Watu wengi wamelizungumzia swala la mapolisi na kama kila mtu anavyojua, sisi sote tukimwona polisi hata akiingia hapa kila mtu ataingiwa na baridi. Kwa sababu gani? Wamewekwa katika hali ya kuwa wao wana nguvu zaidi kutushinda sisi raia tunaowalipa. Maana yake wao hawajui mishahara yao inatoka kwa kodi zetu tunazolipa sisi, lakini imekuwa sasa wao ndio wanatugandamiza. Wanatugandamiza hali ya kuwa ukimwona askari yule askari anakuwa akikushika, ashakuhukumu maana anakupiga, anakuadhibu haraka upesi. Inakuwa wewe hakuna cha kujitetea wewe uko chini ya ulinzi, na anakwambia chochote utakachosema kitatumika kukuhumu koti, na hakuna koti utakayo fikishwa. Kwa hiyo lazima kuwekwe kipengele cha kwamba maaskari wafundiswe sheria. Wafundishwe transparency, kusaidia raia na kuwaokoa maisha yao, isiwe tu wanatuumiza.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Asante, asante.

**Salimi Mwambala:** Haya, shukurani.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Unaweza kutoa hayo maandishi?

**Salim Mwambala:** Ah Ah. Ilikuwa bado moja tu ningelizungumzia basi.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Ukizungumzia moja utatuachia?

**Salim Mwambala:** Ah si waachii, nafikiri mshaandika nyinyi wenyewe. Hize ni points zangu ndogo ndogo tu nimeaandika.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Okay. Mambo yako yote yameingia katika (inaudible)

**Salim Mwambala:** Yameingia hapo, asante.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Njoo ujiandikishe. Bwana Aggrey Kilo. Aggrey Kilo unamaandishi?

**Aggrey Kilo:** Ndio ninamaandishi.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Kwa hiyo mulika tu juu ya maandishi yako.

**Aggrey Kilo:** Nashukuru macommissioner na wananchi waliojitokesha hapa. Kwa majina mimi naitwa Aggrey Kilo vile Bwana Chairman alikuwa amesema na mimi nina vidokezo tatu tu ambavyo nitazungumzia. Kwanza kabisa ni kuhusu nyumba, nyumba za upangizaji. Unakuta ya kuwa Kenya sasa serikali ama munispaa, si kama mukoloni, mukoloni alikuwa anajenga nyumba za wapangizaji lakini serikali ya sasa ama munispaa ya Kenya saa hii, hawafanyi hivi. Na hatuelewi ni kwanini. Ile pesa mkoloni alikuwa anaokota ndio ile serikali ya sasa inarokota, na unakuta serikali ama munispa, hawatujengei nyumba za kupangisha. Sasa hio imeleta jambo ambapo sasa ni wafanyi biashara fulani wanajenga nyumba, (inaudible) kuna kuwa na wapagizaji. Sasa wale watu wanaweka sheria fulani. Anasema ukiingia kwa hii nyumba yangu, utalipa deposit ya miezi tatu ama mieze miwili. Sasa vile unataka kuingia kwa nyumba na una haraka unampa ile pesa. Ukisha mpa ile pesa pengine unapigwa transfer kwa haraka. Unamwambia ile pesa yangu nikupa ya deposit, si unipe. Inakuwa ni mkutano, ile pesa hupati. Kwa hivyo tungelipenda serikali iangalie hili jambo. Juu ukienda kwa watu wa lands tribunal wanakuambia ya kuwa hiyo sheria hakuna. Wanatambua wewe ulipe nyumba, hawatambui deposit. Hiyo pesa yako itakuwa nikuvutana ama pengine hata uwachane nayo. Umechukua transfer mbali kwa hivyo lazima Constitution yenye itakuja lazima iangalie hili jambo, tuweze kulindwa kwa hii mambo ya kulipa deposit.

Jambo la pili ni kuhusu elimu. Unakuta ya kuwa tumekuwa na (inaudible) office ama divisional office. Hawa watu wanatengeneza bairo zao. Unakuta wana either ma-head teachers wanawaambia, tumepitisha hili. Na juu sasa ma-head teachers wako chini yao, akikataa kufuata, atapigwa transfer mahali penye hataki, inabidi afuate. Wanakuja na sheria wanasema, ni lazima watoto wafanye common exam division mzima. Ambapo kila shule itarokota pesa ipeleke kwa division. Ile ni pesa nyingi sana ukichukua shule zote karibu (inaudible). Ile pesa haujui inaenda wapi na wale watu wamelazimishwa, akikataa, transfer. Na ukienda kwa ministry wanasema hatutambui hio. Hamtambui lakini iko (inaudible) Sasa tufanye vipi? Lazima Katiba mpya iangalie hao watu wasi (inaudible) na divisional officers mambo ile wanafanya na ikuwe legalized na serikali ijue ile pesa inarokotwa inatembea kivipi.

Jambo langu la mwisho ni kuhusu wanabiashara ambao wanajulikana kama jua kali. Jua kali wa sasa Kenya unakuta umepelekea mtu fulani vile mzee alikuwa ameongea. Umepelekea mtu vitu. Atatafuta kakosa kadogo, anakuruka kukulipa. Akisha ruka kukulipa, yeye anapesa ya kwenda kuchukua advocate vile yule mzee alivyokuwa ameongea tu. Ni wewe hauna

pesa. Sasa ile process ya kuenda kushtaki yule mtu ni ghali na wewe yule mtu mwenye jua kali hana hiyo pesa. Sasa unakuta yule mtu amedhulumiwa na yule tajiri. Kwa hivyo tena hiyo sheria lazima iangaliwe ikiwa hawa watu watawekewa sheria ambayo itawasaidia. Ikiwa hana pesa, atasaidiwa vipi ili kwenda kuitisha pesa zake.

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Nashukuru. Toa hiyo makaratasi yako. Kaboga Mbeji halafu anafuatwa na *(sentence incomplete)*

***End of Tape 1***

**Speaker**: Sasa ningependa kuzungumzia swala la Katiba. Nina uhakika watu wengi sana mitaani hawajui mambo ya Katiba yatakayo badilishwa wapi? Katiba yawaathiri vipi? wao wanaambiwa waje watoe maoni hali ya kuwa hawajui ni wapi ya wagusa. Kwa hivyo Serikali ingefanya mpango wa kuwa, japo mara mbili kwa wiki swala la Katiba lingekuwako la tangazwa. Watu wanafanya kuelezwa kwamba Katiba yetu ya sema hivi, kipenge hiki cha sema vile. Watu wapate kuelewa kwamba Katiba ya Kenya iko hivi na inamsaidia raia wake hivi na inamuumiza hivi. Ndio pale watu wakija kaa wakiamua wajadili Katiba, watakuwa wanajua manazungumza kitu gani.

Swala la pili ni hili la uandikishaji wa kura. Swala la uandikishaji wa kura ingekuwa ni ubora pale mtu anapochukua kitambulisho, apewe kabisa kadi yake ya kura. Hino itazuia mambo ya kuchukua watu kutoka mji mwingine kuja kuwaleta waje kuchukulie kura ili ya kuwa wakupitishe, na hali ya kuwa wao si wakaaji wa pale. Na kabisa swala hili litakuwa pia linapunguza gharama la kwamba kila mwaka ikifika wa kura inakuwa mpaka lazima kuwekwa watu wa Commissioner ya kuandikisha kura, inakuwa ni pesa zingine zinatoka kwa Serikali kuwalipa wale na hali ya kuwa ni tax tunalipa sisi wananchi, tunaulizwa kwa kila kitu.

Swala la tatu ni hawa waraia wa makaratasi, 'citizens by papers'. Hawa 'citizens by papers' tunaona kama nchi kama America vile, wao hawaruhusiwi kupiga kura wala kuchukua kura. Ningependekeza na hapa kwetu swala hilo pia liweko maanake hawa ndio wanakuwa na influence ya kutuumiza sisi kimawazo, kifikira na kihali ya uchumi. Kutokamana na nguvu zao za centi.

Swala lingine ambalo Ningependekeza ni kwamba, hao wanaogombea ubunge. Lau mtu amepata term yake ya kwanza, a-serve term mbili peke yake, yaani kipindi cha miaka kumi. Baada ya miaka kumi ile, haruhusiwi tena kugombea ule ubunge kwa sababu atakuwa akili yake sasa imeshazorota kimaendeleo. Atakuwa sasa yeye ni mtu wa kujinufaisha matumbo yake na kugandamiza wananchi. Hakuna moja atakalo kufanyia! Mfano mzuri twaona Mvita uko.

Swali lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni hili wazungu wasema 'justice delayed is justice denied.' Serikali yetu kwa uhakika ina centi za kutosha na hapa kutokana na kwamba ina centi za kutosha, ingeongeza idadi ya Mahakimu, hawa Magistrates. Wangeongezwa wakawa wengi na kukawa na transparency ya zile kesi. Sio mtu leo askari anamshika, amemwona kabisa akitoka dukani, anamuuliza watoka wapi, unaenda wapi? Si ananiona mimi ninatoka dukani ninaenda

nyumbani. Swala kama lile lirekebishwe kwamba, yule mtu akishikwa akipelekwa kortini, atakuwa ni mtu, hali ya kuwa wanakwenda pale, wanazungumza kesi yao, kama ni mashahidi anawaita, siku ile ile, mashahidi wao wanzungumza kesi ile. Ikifika kwamba amehukumiwa kufungwa, anakwenda kutumika kisawa. Sio kwamba anakwenda kuhukumiwa kwa kwamba amegandamizwa. Tunaona sera hii inatumika Uganda, na sera hii pia inatumika Tanzania, kwa nini Kenya tusiitumie?

Swala lingine ni hili swala la mapolisi. Watu wengi wamelizungumzia swala la mapolisi na kama kila mtu anavyojua, sisi sote tukimwona polisi, hata akiingia hapa, kila mtu ataingiwa na baridi. Kwa sababu gani? Wamewekwa katika hali ya kuwa wao wananguvu zaidi kutushinda sisi raia tunaowalipa. Maanake hao hawajui mishahara yao inatoka kwa kodi zetu tunazolipa sisi, lakini imekuwa sasa hao ndio wanatugandamiza. Wanatugandamiza hali ya kuwa ukimwona askari leo, askari anakuwa akikushika, ashakuhukumu, maana anakupiga anakuhathibu, haraka upesi. Inakuwa wwewe hakuna njia ya kujitetea, wewe uko chini cha ulinzi na anakwambia chochote utakacho sema, kitatumika kukuhukumu kortini. Na hakuna korti utakayo fikishwa. Kwa hivyo lazima kuwekwa kipenge cha kwamba ma-askari wafundishwe sheria, wafundishwe transparency, kusaidia raia na kuwaokoa maisha yao. Isiwe tu wanatuumiza.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Asante, asante.

**Speaker**: Shukrani.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Unaweza kutoa hayo maandishi?
**Speaker**: Hapana, ilikuwa bado moja tu, ningelizungumzia, basi.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Ukizungumzia moja utatuachia?

**Speaker**: Hapana, siwaachii. Nafikiri mshaandika nyinyi wenyewe. Hizi ni points zangu, ndogo ndogo tu nimeanadika.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Okay, mambo yako yote katika hiyo machine.

**Speaker**: Yameingia hapo eh? Asante.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Yameingia, njoo ujiandikishe tu. Bwana Aggrey Kilo. Aggrey Kilo una maandishi?

**Aggrey Kilo**: Ndio nina maandishi.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Kwa hiyo, mulika tu juu ya maandishi yako.

**Aggrey Kilo**: Ninashukuru ma-commissioner na wananchi waliojitokeza hapa. Kwa majina mimi ninaitwa Aggrey Kilo, vile Bwana Chairman alikuwa amesema, na mimi nina vidokezo vitatu ambavyo nitazungumzia.

Kwanza kabisa ni kuhusu nyumba, nyumba za upangaji. Unakuta ya kuwa Kenya sasa, Serikali ama municipaa, sijui kama ni mkoloni alikuwa anajenga nyumba za upangaji lakini Serikali ya sasa ama municipaa ya Kenya saa hii hawafanyi hivyo na hatuelewi ni kwa nini. Zile pesa mkoloni alikuwa anaokota ndio zile zile Serikali ya sasa inaokota na unakuta Serikali ama municipaa hawatujengei nyumba za kupangisha.

Sasa hii imeleta mambo ambapo sasa ni wafanyibiashara fulani wanajenga nyumba na kuna kuwa na wapangaji. Sasa wale watu wanaweka sheria fulani. Wanasema ukiingia kwa hii nyumba yangu, utalipa deposit ya miezi tatu ama miezi miwili. Sasa vile unataka kuingia kwa nyumba na una haraka, unampa zile pesa. Ukishampa ile pesa, pengine unachukua transfer kwa haraka, unamwambia ile pesa yangu nilikupa ya deposit nipe. Inakuwa ni mkutano, zile pesa hupata! Kwa hivyo tungependa Serikali iangalie hili jambo kwa sababu ukienda kwa watu wa Land Tribunal, wanakwambia ya kuwa hiyo sheria hakuna. Wanatambua wewe ulipe nyumba, hawatambui deposit. Hizo pesa zaki, itakuwa ni kuvutana na pengine hata uwachane nayo, kwa vile umepigiwa transfer mbali. Kwa hivyo lazima, Constitution ambayo itakuja, iangalie hili jambo, tuweze kulindwa kwa haya mambo ya kulipa deposit.

Jambo la pili ni kuhusu elimu. Unakuta ya kuwa tumekuwa na kitu kinaitwa (?) office ama Divisional fees. Hawa watu wanatengeneza by-laws zao. Unakuta wanawaita ma head teachers wanawaambia tumepitisha hivi. Na kwa vile ma head teachers wako chini yao, wakikataa kufuata, watapigwa transfer mahali ambapo hawataki, inabidi wafuate.

Wanakuja na sheria wanasema ni lazima watoto wafanye common exam, Division nzima, ambapo kila shule itakusanya pesa ipeleke kwa Division. Hizo ni pesa nyingi sana ukiichukua shule zote, karibu shule hamsini. Hizo pesa hatujui zinaenda wapi? Na wale watu wamelazimishwa, wakikataa transfer. Na ukienda kwa ministry inasema hatutambui hiyo, hamtambui lakini iko, ina exist. Sasa tufanye vipi? Lazima Katiba mpya ianagalie hawa watu (?) na divisional offices mambo yale wanafanya na ikuwe legalized, na Serikali ijue zile pesa zinakusanywa zinatumika vipi.

Jambo langu la mwisho ni kuhusu wanabiashara ambao wanjulikana kama Jua-Kali. Jua-Kali wa sasa Kenya unakuta umemplekea mtu fulani vile mzee alikuwa ameongea, umemepelekea mtu fulani vitu, atatafuta ka kosa kadogo halafu ataruka kukulipa. Akishakuruka kukulipa, yeye anapesa za kwenda kuchukua advocate, vile yule mzee alikuwa ameongea tu, wewe hauna pesa.

Sasa ile process ya kwenda kumshataki yule mtu ni ghali na wewe mtu wa Jua-Kali, hana hiyo pesa. Sasa unakauta yule mtu amedhulumiwa na yule tajiri. Kwa hivyo tena hiyo sheria lazima ianagaliwe ikiwa, au watu watawekewa sheria ambayo itawasaidia. Ikiwa hana pesa, atasaidiwa vipi? Ili kuweza kuitisha pesa zake.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Nakushukuru sana, toa hayo maandishi yako. Kabwoga Mrenje, halafu anafuatwa na Asha Charles, awe tayari. Mzee, unamaandishi?

**Kabwoga Mrenje**: Sina maandishi.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Endelea.

**Kabwoga Mrenje**: Basi hata mimi…

(Interjection) **Com Pastor Zablon Ayonga**: Sema majina kwanza.

**Kabwoga Mrenje**: Ninaitwa Kabwoga Mrenje, mzaliwa wa Mwakirunge Sub-Location, Ngutatu, Gandini. Shida ni kwamba Katiba ya Kenya ilivyo inatuendesha sasa tunapata taabu. Ikiwa nina miaka sitini na minne lakini ubovu ni kwambiwa ninaitwa skwota na hiyo ndio shida. Tunataka Katiba ya leo, ituamini kwamba sisi tunapoishi, pawe ni mahali petu kabisa. Kwa sababu tunateswa ikiwa Serikali yenyewe ndio inayosema hapo ni pa wenyewe na sisi tumezaliwa sisi wenyewe ni sisi. Kwa hivyo ninafikiri hayo ni maoni kwamba Katiba itake kutupa haki kama vile uhuru wa binadamu ni ardhi.

Hatutaki kule kunyanyaswa na hali tukikaa tunawasiwasi. Mtu ukiwa wewe umeishi mahali kwako lakini unaambiwa wewe ni skwota, ni kama mtu aliyekuwa amesimama ndani ya gari, hanu ukanuna hakuwezi kununua gari. Hivi sasa ninaona Katiba ijaribu sana, tuhakikishe hiyo ploti tunayoishi, tuhakikishe na wenzetu ambao hawaishi humu Mombasa wawe wanahaki kumiliki ardhi ile wanaoishi. Sina mengi, ni hayo kidogo nimeyatoa ili tupate haki na sisi.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Asante sana mzee, uje hapa ujiandikishe. Next ni Mama Asha Charles. Mama una maandishi?

**Mama Asha Charles**: Nilikuwa siyasomi mimi, nilikuwa na mwenzangu, atasoma.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Okay, basi unaweza kumulika juu ya hayo mambo.

**Mama Asha Charles**: Mimi ninaitwa Mama Asha Charles. Maoni yangu ninayotoa hapa kulingana na Serikali yetu hii, sisi kina mama katika Serikali hii hatuna sauti na hatuna haki. Kwa upande wa kuridhi, kwa upande wa wawaume zetu, tunadhulumiwa na Serikali huwa haitilii maanani.

Kama sisi Waislamu, waume zetu wameruhusiwa kuwaoa wake wanne lakini wana masharti yao ya kufanya waoe. Masharti yale huwa hawayashiki na akimwacha mke, kuna masharti, lazima yule mke aliyeachwa atimiziwe, hawatimiziwi. Kwa hivyo

tungeomba Serikali itie nguvu sheria ya Mwenyezi Mungu haifutiki lakini itie nguvu Serikali zile masharti zifuatwe za kuachwa na za kuoa.

Jambo jingine, sisi kina mama ndio tuanaopata shia katika community yaani katika jamii. Mama mimi nitazaa, niwalee watoto wangu, wakue, bahati nzuri wapate kazi. Ikiwa ni mume aoe yule bibi hata sitaangaliwa, nimefika umri wa kizee lakini mtoto wangu yeye na bibi yake tu, hajui kama mama amezeeka anahitaji msaada.

Ningeomba Serikali itoe jukumu ya kuwa kuwe na percentage fulani, mama wakifika awe kama watoto wake wanafanya kazi awe akipatiwa hizo pesa. Kwa maana, kina mama wengi wanapata shida na watoto wao wanafanya makazi makubwa, makubwa, wana magari lakini ukiangalia mamake na ile hali aliyo, imekuwa ya kusikitisha sana.

Lingine sisi kina mama wa Mombasa hapa tunatumiwa kama vyombo vya kupiga kura, baada ya kura imekwisha. Hatupewi nafasi ya sisi kina mama kujiendeleza. Tukiwa na shida zetu tukiingia kwenya maofisi ya Serikali, ikiwa huna kitu kidogo hutiliwi sign ujekupata kitambulisho, kwa chifu husikizwi kesi yako, kila kitu wewe mama ni lazima utoe kitu kidogo. Kwa hivyo sisi kina mama sasa tunataka haki utukike kutoka nyumbani kwa mzee aliyenioa mpaka kwa Serikali, itutambue.

Jambo jingine ambalo sisi kina mama tunadhulumika, kwa wazazi wetu. Wanaamini kuwa mtoto wa kiume ndiye anaridhi mji, lakini mtoto wa kiume yule hawaangalii wazazi. Mimi ndiye ninaweza kumbuka babangu amezeeka nikampelekea shati, mamangu amezeeka nikampelekea rinda lakini mtoto wa kiume akioa ni yeye na kwa bibi peke yake. Kwa hivyo uradhi utiliwe Serikali maanani kuwa mtoto wa kike aweze kumiliki kwa wazazi wake.

(***Clapping from the audience***)

Na recruitment katika Serikali, ianze kuanza (?). Kama ni polisi, ianze pale pale. Kuna Nyali, kuna Bamburi, lakini wakati wa kuandikishwa kazi unakuta watu wanatoka mahali kwingine, wanaletwa tu, hao ndio wamechaguliwa. Tunataka kila police station ku-recruit watu kutoka area ile, (***Clapping from the audience***) watoto wetu wapate kazi.

Sisi kina mama tusiwe tu ni bendera ya kuwa yafuata upepo. Saa hii tuanataka tuwe tumekita chini kabisa! Mume anaye piga bibi yake kupita kiasi si lazima ati kuwa maneno ya mume na mke hayaingiliwi, sheria itumike pale, yule mume aulizwe kwa nini amempiga bibi yake viel. Sio kusema ati umepigana na bwana yako wewe, hiyo ni shauri yako, hatutaki, tunataka tujue haki zetu.

Na hapa Coast, hizi polytechnics, iwe nafasi za kwanza zinapewa watoto wa Coast ambao zile polytechnic ziko. Lakini utakuta watoto wa Coast waki-apply wanaambiwa nafasi hakuna ama amefeli ama hakupasi vizuri. Tatizo hilo tuachieni kila watu na sehemu zao wamiliki, wajisikie na hao ni raia wa nchi ile. Asante sana.

(***Clapping from the audience***)

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Asante mama, lakini ngoja kidogo. umesema yule mume anayepiga bibi yake kupita kiasi. Kupita kiasi ni nini?

**Mama Asha Charles**: Karibu kuua.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Mpaka azirai?

**Mama Asha Charles**: Mpaka azirai ama pia kuua ama amtoe macho…

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Na yule mwanamke anayempiga bwana yake?

(***Laughing and clapping from the audience***)

**Mama Asha Charles**: Hilo ni kofi la mahaba, haliumizi.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Eeh, unajua kina mama wanapiga bwana mpaka hata wengine wamechemsha maji wakataka kumfanya kama kuku anayetolewa manyoya?

**Mama Asha Charles**: Ndio, lakini ninataka sheria itumike kote, kote.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Oh, sheria iweko kwa violence kwa wote wote? Isiwe ni ya wanawake, lakini iwe kwa kila mtu kwamba iwe ni mtoto, iwe ni mwanamke, ni mwanamume, asitendewe kinyama?

**Mama Asha Charles**: Ndio.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Asante. Ngoja kidogo.

**Com Paul Wambua**: Swali langu ni hilo hilo, ningelipenda kujua kiasi ni gani. Kupita kiasi ndio umesema lakini kiasi ndio gani?

**Mama Asha Charles**: Kama vile nilivyozungumza ya kuwa kuzirai ama karibu kufa. Yaani amempiga, hakum-punish, ame…

(Interjection) **Com Pastor Zablon Ayonga**: Lakini swali ambalo Commissioner anakuuliza, kwamba kiasi ni nini ambacho wewe ungesema ukimpiga hivi na hivi, hilo si neno? Haya endelea tu mama, utupe hayo makaratasi na ujiandikishe. Next kuna Eddy M.

Tafadhali watu ni wengi na ningalipenda ndugu zangu na dada zangu mchukue dakika tatu, tatu kwa kumulika maneno yenu. Ninataka kila mtu apate nafasi ya kusema kitu, kwa maana watu hawa… unaposema tano, huyu atabaki. Kwa maana nina majina hapa chungu nzima na yanazidi kuja. Na ninataka kila moja wenu apate nafasi. Njia tu ya kuwezesha kila mmoja wenu apate nafasi ni kukata dakika, mpaka itafikia wakati nitasema dakika moja, moja. Kwa hivyo ninaposema tatu, hebu tufuate hizo. Endelea. Hebu utupe mfano wa dakika tatu. Mnyamaze msikize tafadhali.

**Eddy Mzungu**: Asante sana Bwana Chairman, kwa majina ninaitwa Eddy Mzungu. Jambo la kwanza ninataka kuwafahamisha wananchi kuwa tunataka Katiba ambayo ni ya wananchi, Katiba ya wananchi. Saa hii ukitupatia dakika tatu, tatu kuna mpango gani hapo?

(***Clapping from the audience***)

Katiba tunataka ya wananchi, na ukiangalia katika registration yako, utaona kwamba… hata pengine utapata watu mia tatu. Kwa hivyo, ninafikiria mngerudi ma-commissioner, mkaanza tena kuhakikisha Katiba ni ya watu, million thelathini sio ya watu mia tatu hapa, mia mbili kule, hapana hiyo bado…

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Endelea, endelea.

**Eddy Mzungu**: Katika elimu, ninaguzia hapo katika elimu, ma-Commissioner tafadhali, muwafundishe watu Katiba. Katiba iandikwe katika kabila arubaini na mbili, kila mmoja apate haki ya kujua vile inaenda.

Tatu, ninataka kusema hivi, Katiba ambayo iko hapa sio kusema ni mbaya, Katiba ambayo tuko nayo sio mbaya vile, lakini ni utoshelezi, implementation wa hiyo Katiba ndio mbaya. Saa hii pia tunawaona pale nyinyi ni ma-professionals, ma-Commissioners ishirini na tisa. Mumepewa kazi, sijui ilikwenda aje mkauliza miaka mbili. Hata mkiwa mmekosea hesabu zenu, mnakuja tena kuuliza miaka kumi, hizi hesabu zenu na nyinyi ma-professionals, ma-professor. Mnakuja kupiga hesabu na mnazikosa, na mnakuja tena, muko na njama gani? Muko na njama gani nyinyi? Hebu mtueleze. Ikiwa hii Katiba ni Katiba ya mageuzi ya Serikali mtuambie, sio kuja hapa kutuambia ni Katiba ya wananchi, hapana, iko njama nyinyi mnataka. Mkiwa mshaandika Katiba pia, mtueleze, ikiwa mshaandika.

(***Clapping from the audience***)

Sisi hapa tulipo na Wakenya wote, hakuna mtu asiye na kabila. Mambo machifu katika nchi yetu yameletwa na uchoyo, na mambo mabaya. Usiseme huna kabila, kabila bado liko na kila kabila ina nia zake, ina madesturi yake. Kwa hivyo kuondoa haya yote, tunauliza Serikali ile ya mwanzo, Serikali ya majimbo.

(Clapping from the audience)

Tunataka kuondoa P.C. Huu ni mpango wa Serikali. Nani anataka P.C? Nani anataka D.C? Nani anataka chief? Nani anataka mambo yote hayo? Hatujawachagua hawa watu, kwa hivyo hatuna haja nao.

Katika Serikali ya majimbo, tunataka vyama vinane, kila jimbo na chama chake. Ma-commissioner, mkifanya kazi yenu, tunataka idadi ya wale wameshiriki katika badiliko la Katiba. Hapo tutajua ukweli, ikiwa Katiba ilikuwa ya wananchi au ilikuwa ya Serikali ya KANU.

Pia, katika elimu, tunataka nini, tunataka Katiba ienezwe kila pahali. Hospitali, kuna mama wengine hapa hata Pwani na kila pahali. Utakuta mama, yeye ni mwenye kichaa lakini mama yule ukimwangalia pia utamkuta yuko na mimba. Akifika hospitali, anarushwa rushwa huku, anaraushwa rushwa huko, haeleweki. Kwa hivyo, wale ambao wako na kichaa, wakina mama ambao wako na kichaa na wako na mimba, tafadhali Katiba ije na mtindo mwema wa hudumiwe.

Disabled, hawa ni watu wetu. Zamani tulikuwa hatujui lakini sasa naomba katika Katiba wajengewe ma-estate yao ambayo watakuwa kule, wawe na infrastructure zao, tunajua pia wanataka viti, tunataka ma-crutches. haya ni mambo ya kupewa bure, kwa maana tunafahamu Serikali iko na pesa na iko na pesa kweli kwa maana hata commissioner pale, zile anachukua pia sio za kawaida.

Mbunge: Mbunge wa kulala hatuna haja naye. Kwa hivyo mimi nina-propose, mbunge yeyote ambaye hafanyi kazi yake sawa, wananchi wale wale wamepiga kura, wawe na uwezo through the Ombudsman wa kumwita na kumfuta kazi.

(***Clapping from the audience***)

Tatu, mayor achaguliwe na wananchi. Local Government yetu iwe ni ya wananchi wenyewe. Hapa tumesema tunataka majimbo kwa hivyo hatuna haja na Rais, tuko na haja na Prime Minister. Prime Minister kazi zake ninampatia ni tatu tu. Defence, taxation and foreign affairs.

Majaji, tutawaandika sisi wenyewe katika region kwa maana tumesema majimbo. Kwa hivyo katika majimbo tunataka governor na ma-senator ambao kila mtu atamchagua kutoka jimbo lake. Prime Minister ni mmoja tumesema na ikiwa tunataka kuwakilishwa, tutachagua wenyewe huyo Prime Minister.

Regional governors watakaa na Prime Minister to determine foreign affairs, taxation na defence. Tunataka pia na sera zifuatazo:-Ombudsman, independent Judiciary, Public Service Commission na kadhalika. Mamabo yote yatoke kutoka majimbo. Asante Bwana Chairman kwa kunisikiliza.

(***Clapping from the audience***)

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Asante Bwana Eddy, je una maandishi utatuachia?

**Eddy Mzungu**: Niko na maandishi na ninafikiria nimeweka kila kitu pahali pake.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Thank you so much. Next atakuwa, Mal, Jan. Hakuna jina lingine ni hilo tu Mal Jan. hakuna mwenye jina hilo? Pengine nimelitaja vibaya. Okay. Kahindi? Mwasoke Joseph?

**Mwasoke Joseph**: Hamjambo?

**Response from the audience**: Hatujambo.

**Mwasoke Joseph**: Mimi kwa majina ninaitwa Mwasoke Joseph kutoka kwa Kamati ya Eleimu ya haki za Uraia, Ziwa la Ng,ombe. Nitatoa maoni kulingana na vile walivyoyatoa watu wa Ziwa La Ng,ombe, na nitazungumzia katika nyanja tatu. Nyanja ya siasa, nyanja ya mahakama na raslimali. Nitaanza.

Katika nyanja ya siasa, kamati hii inataka Serikali ya majimbo. Pili, mtu yeyote anayetaka kupigiwa kura awe ni mkaaji wa eneo analotaka kuwakilisha. Pia, mayor wowote wa mji achaguliwe na wananchi na sio madiwani. Awe ni mkaaji wa sehemu hiyo.

Pia, kila Mbunge na Diwani awe na kamati katika eneo lake itakayo mfuatilia kazi yake na pia yale aliyoahidi kutekeleza wakati wa campaign na awe na ofisi katika eneo lake. Wananchi wawe na uhuru wa kuchagua viongozi wanaowataka, na wasilazimishwe kwa hongo.

Miswada yote katika Bunge, iwasilishwe kwa Speaker, kwa lugha ya Kiswahili na pia ijadiliwe kwa lugha ya Kiswahili. Madiwani wote wawe na maofisi katika wadi zao. Mawaziri wachaguliwe na Bunge na sio kupendekezwa na Rais.

Katika nyanga za mahakama. Mkuu wa Sheria achaguliwe na kamati ya Bunge na sio kupendekezwa na Rais. Rais anapofanya makosa, ashatakiwe akiwe mamalakani. Mtu yeyeote mwenye deni la Serikali, asisimamae kwa uchaguzi. Katiba

ifundishwe mashuleni. Katiba iandikwe kwa lugha ya kueleweka na nyepesi. Machifu wachaguliwe na wananchi.

Kitabu cha Katiba kiwekwe kwenye maktaba na viuzwe kwa maduka ya vitabu kwa bei nafuu. Kenya iwe na vazi la kitaifa la heshima. Wafungwa wa Kenya wawe na uhuru wa kupiga kura na magerega ya Kenya yawe na uangalifu wa kiafya. Vazi la kuonyesha sehemu za siri liwe ni hatia Kenya. Wazee wa mtitaa walipwe mishahara.

Katika haki za raslimali, kamati hii imependekeza yafuatayo:- Raslimali zinazopatiakana katika maeneo zifahidi wakaaji wa sehemu hiyo. Raslimali zinazoptikana katika maeneo yote zitambuliwe na Serikali na zipewe haki sawa katika kutafutiwa masoko ya hapa nchini na hata nchi za nje, ili ziwafaidi Wakenya wote.

Viwanda vilivyofilisishwa, vifufuliwe na Serikali na seria ziwekwe kulinda raslimali hizi. Ardhi ambazo zinamilikiwa na matajiri ambao hawazitumii kimaendeleo zigawiwe maskwots. Wafanyi biashara wa Kenya na wa kigeni, walazimishwe kuweka pesa zao na benki za humu nchini. Hii inafuatia wale Wahindi wanao weka pesa zao katika nyumba zao ambazo hazi nufaishi ama hata hazikatwi ushuru wowote kwa Serikali.

Kila Mkenya mwenye umri wa miaka ishirini apewe ardhi amiliki kutoka kwa Serikali, anapotoa maombi. Serikali isimamie na kulinda bei za bidhaa zote. Mwisho, tamaduni za Wakenya zidumishwe na kudhaminiwa. Asanteni.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Na shukuru. Unaweza kutoa maandishi hapa. Roy Hombo, halafu Bahati Musa awe tayari. Roy unaweza kuendelea na kama una aandishi, tafadhali umulike tu makubwa makubwa ya maandishi yako.

**Roy Ibongo**: Kwanza ninasimama hapa nikiwa mmoja wa wale viongozi ama kamati ya Ziwa La Ng'ombe settlement scheme. Wale wamekaa ningependa kuwatambua ni akina nani ama ni wawakilishi gani ambao watakuja hapa na kutoa maoni. Kwa majina ninaitwa Roy Ibongo kutoka Ziwa La Ng'ombe.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Endelea.

**Roy Ibongo**: Hasa tulipokuwa tukichambua tumekuja kupata ya kwamba kunastahili kuwa na Serikali ya majimbo. Na labda ni kufafanua, Serikali ya majimbo imesemwa na wengi lakini ni ya kwamba hasa wengine hawaielewi na wengine wengi wanaielewa lakini ni kutaka kuiharibu ili isieleweke kwa usawa.

Hivyo ni ya kwamba, katika Serikali ya majimbo, itafunga mlango mmoja. Wa kwanza mheshimiwa wa kwanza aliyekuwa hapa Kenya, Kenyatta, alichukua jukumu la kuhakikisha kwamba watu wake wote wataridhi viwanja vyao na halafu viwanja vya wengine.

Halafu katika vile ilivyokuwa imeemdelea, yeye amefanya yale aliyokuwa akitaka. Mwingine amekuja kuingia hapa, tusiwe na uoga wa kuzungumza ya kwamba Rais Moi, Amechukua hatamu ya kuhakikisha ya kwamba kila province ameweka watuw ale mizinga, mizinga, kama P.C, kama D.C. Kama hakuna P.C. Mnandi, basi D.C. ni Mnandi.

Ikifikia wakati wa kwamba tunakuja kumchagua Rais mwingine atakaye kuwa ni kabila nyingine, yeye naye akakuja na sheria zake na atafahisisha watu wake. Je tukiwa na sheria za majimbo ama Katiba ha majimbo ama Serikali ya majimbo si tutatkuwa haya yote tumeyamaliza? Hiyo ndio ninaeleza.

(***Clapping from the audience***)

nikiruka mbele, ninakuja kwa nafasi ya machifu. Machifu Tunapendekeza ikiwa itawezekana, machifu wachaguliwe na wananchi wenyewe. Kwa sababu gani? Saa hii tukimwona chifu ni kama tumemwona askari na tunapomwona askati saa hii, tunakuta kwamaba, nafikiri mwenzangualilyekuja hapa amesema kwamba saa hii askari akitoka pale mlangoni akipita hapa, karibu kila mtu atashtuka ndani ya moyo wake, ni kama tumeona dude lingine, yani imebadilishwa ya kwamba badala ya tuwe tumemona mwizi ndio tushtuke, sisi tukimwoana askari ndio tunashtuka sasa. Afadhali yule mwizi. Hiyo ni ya kwamba machifu wachaguliwe na wananchi wenyewe.

Halafu tukisonga mbele tena tumesema ya kwamba tuwe na vazi la kiserikali, yaani ni vazi la kitaifa ambalo tutakuwa sisi wenyewe tunajivunia. Tukisema ya kwamba labda kuna sherehe zilizo labda pengine, kwa sababu kuna sherehe nzuri zilizo zina mark mambo yaliyofanyika hapa Kenya. Hivyo ni ya kwamba vazi kama lile likitumika tutakuwa tunaweza tukaangalia Kenya ikiwa yang'ara. Kama vile kwa mfano tukienda Nigeria, nguo za Wanigeria pahali popote ukiona hivi hata ukiona kwa T.V, utajua tayari hi ni Nigeria. Ndio tunaomba sisi tuwe na vazi kama lile. Nafikiri tumependekeza mapaka tukataja lile vazi na nafikiri tutawapa maandishi.

Lingine ni ya kwamba tuwe na hali ya mlolongo wa mavazi, huku nyuma yaliyo labda pengine vazi la kitaifa liko pale lakini kuna sheria za mavazi haswa. Kwa sababu hata likiwa la taifa, labda wengine wanaweza kulivaa vibaya. Hivyo ni ya kwamba tuelekee pahali pa mavazi yasiyoleta utatanishi.

Vazi la kujionesha mwili wako, ukiwa uko nje limeenea sana haswa hapa Pwani. Tulikuwa hatuna hilo. Nikiangaza macho hivi nilikuwa hakuna na tulikuwa tunajua kabisa ya kwamba labda wazungu ndio wakija hapa wanatuletea haya. Baadaye ikaja ikaagua wazungu kwa sababu wazungu walikuwa wamezoea kutembea na costume hata kwa ma-towns, wakapunguziwa wale wazungu lakini tumekuja ku-adopt ya kwamba wale wasichana wetu ndio wanavaa hata zaidi ya wale wazungu.

Kwa hivyo tuwe na sheria ya kwamba, mtu kama yule ama tuweke kitu kama… tuseme kama kwa club, wewe unajistarehesha kule kwa club. Tuwe tunaweza tukatambua hawa watu wako kivipi sio akavae vazi lile na wengine hata ni mabibi za watu!

Wanakuja kuvaa mavazi yale wakiwa wanatembea. Je, mimi niliye mwanamume, niliye damu yangu inatembea, ninakuja kukupata msichana unatoka kutoka pale na unaingia hivi ukiwa matiti wazi, vikiwa vimesimama namna hii na huku mapaja nayaona yale. Je, nitafanya nini?

Sasa basi, hiyo ni ya kwamba inakuwa ile inarekebishwa kwanza, tuwe na sheria hiyo, pili ndio tunaweza tukarudi hapa, kuna mama amaesema raping cases ziwe strict. Kusema kweli hata mimi ninapenda hiyo. Ya kwamba hizi raping cases tuhakikishe… kwa sababu siku hizi hata mzee wa kiume ana-rape mtoto wake wa kiume! Kwa sababu imekuwa kuna freedom ana pesa na amini usiamini tumewaona wengi sisi wengine ya kwamba anafanya hivyo na anakwenda na anawekwa tu siku au pengine miezi miwili au mwezi mmoja, ametoa pesa, ameweka advocate amekuja kutolewa na hakuna kesi yoyote kwa sababu ana uwezo.

Samahani, katika vile ilivyo, tulikuwa tunataka tupendekeze vivyo hivyo ya kwamba wazee wa mitaa nao wapate haki za kulipwa mishahara kwa sababu ndio walio na shida kubwa zaidi kushinda hata chief. Asanteni kwa hayo machache.

(***Clapping from the audience***)

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Thank you. (Inaudible).
**Roy Ibongo**: Nafikiri (inaudible) are two things.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Hebu uje hapa ujiandikishe. Next atakuwa Bahati Musa. Mama unamaandishi?

**Bahati Musa**: Hapana, sina maandishi.

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Kwa hivyo tumulikie mawazo yako.

## Bahati Musa: Habari zenu?

**Response from the audience**: Mzuri.

**Bahati Musa**: Mimi ninaitwa Bahati Musa kutoka Ziko. Maoni yangu upande wa haki ya nyanja za kisiasa huko Ziwa la Ng'ombe, tumesema tunataka majimbo. La pili, tumesema mtu yeyote anayetaka kupigiwa kura, awe ni mkaaji wa eneo analotaka kuwakilisha, sio atoke pahali pengine. La tatu, wananchi wawe na huru wa kuchagua viongozi wanaowataka na wasilazimishwe au kununuliwa.

Lingine ambalo nitazungumzia ni kwenye haki za mahakama. Kitabu cha Katiba kiwekwe kwenye maktaba na viuzwe kwenye maduka ya vitabu na pia ifunzwe shuleni ili kila Mwanakenya aielewe.

Lingine, Kenya iwe na mavazi rasmi ya kiheshima. Kwa upande wa eleimu pia, tunaomba elimu iwe ya bure ili kila mwananchi wa Kenya awe na elimu. Lingine ni kuwa…

(Interjection) **Com Pastor Ayonga**: hebu maongezi ya kule nyuma, tafadhali tumsikilize huyu mama.

**Bahati Musa**: Lingine kwa maoni yangu ninaomba kuwa matibabu ya hospitali yawe ya bure ili kila mwananchi apate huduma. Asanteni.

**Com Pastor Ayonga**: Asante mama, kama unaweza kutoa hiyo karatasi yako na ujiandikishe. Huyo alikuwa Bahati Musa. Sasa ni Tumu Hamisi. Halafi anayeitwa Harry, ajitayarishe. Tafadhali tuwe kimwa ili tuyasikia maoni ya mama Tumu Hamisi.

**Tumu Hamisi**: Hamjambo?

**Response from the audience**: Hatujambo.

**Tumu Hamisi**: Kwa majina kamili ninaitwa Mwanatumu Mwinyi Hamisi, ninatoka kwenye kamati ya Ziwa la Ng'ombe settlement scheme. Nimekuja hapa kutoa maoni.

Maoni yangu ya kwanza yanasema kuwa, mkuu wa sheria achaguliwe na kamati ya bunge na sio Rais. tunataka Serikali ya majimbo. Miswada yote katika bunge iwasilishwe kwaq Speakeer kwa lugha ya kiswahili na pia igadiliwe Kiswahili. Madiwani wote wawe na ofisi katika wardi zao.

Mawaziri wachaguliwe na bunge na sio Rais. kila mbunge na Diwani awe na kamati katika eneo lake, itakayofuatilia kazi yake na yale aliyoahidi kutengeneza wakati wa campaign na awe na ofisi katika eneo lake. Ni hayo tu.

**Com Pastor Ayonga Bahati Musa**: Asante mama. Wapi Harry na Bakari Sire awe tayari.

**Harry Philip Mbai Njoro Ali**: *Assalam aleykum*!

**Response from the audience**: *Warahmatulahi wabarakat*.

**Harry Philip Mbai Njoro Ali**: Mimi ningependa kwanza kusimama, tafadhali. Sipendi kuketi. Jina langu ni Harry Philip Mbai Njoro Ali. Mkaaji wa Free town, kabila langu ni Mdigo Mkauma.

Kwanza ninashukuru wote waliotoa maoni, watu wote, wote kwa sababu yale walioyasema ndio niliyoyaandika hapa

hatasiyataki tena nitatoa yangu. Swali kubwa ambalo ninalo mimi leo, ni juu ninahakikisha wote walio hapa wengine hawana kazi. Kina baba, kina mama, wamesomesha watoto hawana kazi.

(***Clapping from the audience***)

Katiba ya Kenya inatuambia pakijengwa hotel, ni parastatal iko Katiba hiyo, iko, kwamba 60% ya waandikwa watoke sehemu inayowakilishwa na bunge (?). Leo kitu kile hakuna. Uhuni na wizi uko, utakuwako, hautakuwako. Utakuwako, hautakuwako uhuni na uwivu? Ikiwa mimi ni Mjaluo nimezaliwa hapa Coast Province, mimi ni Mcoast. Kwa nini muchukue Mjaluo kutoka siay auje umwandike kazi hapa na Mjaluo ule yuko hapa hapa?

(***Ululation and Clapping from the audience***)

Katiba iko? Kama walivyosema wenzangu. Matelekelezo ya Katiba hakuna na Katiba iko. Ni urongo ninavyosema?

**Response from the audience**: Kweli.

**Harry Philip Mbai Njoro Ali**: Kwa nini? Wasomi wako, wajumbe wako, kwa nini hivi? Kuna lengo. Kuna kusudi eh, kuna tabia ya kumdharau mzaliwa kutoka jimbo la Pwani, iko, iko na huo ndio ushahidi, ushahidi ninatoa. Wakati pipeline ikijenga mapipa yake ya mafuta, kazi ilianzia Nairobi kuja Mombasa, na mafuta yako Mombasa! Kwa nini haikuanzia hapa ikaenda kule? Ili tukose kazi.

Pili, ninasizitiza Serikali ichukue jukumu la kuelimisha watu bur, hospitali bure na especially hili jimbo la Pwani lichunguzwe juu ya kilimo. Ni kwa nini ninasema hospitali bure? Leo kuna kina mama wamezaa hospitalini na wamefungwa hospitalini. Hospitali za Kenya zimekuwa jela! Mama amefungwa hatoki mpaka alete shilingi elfu kumi na mama ashagifungua. Mume yuko kazini. Aadae chakula cha bibi, atampelekea saa ngapi, mama anakula nini pale hospitalini? Serikali hailioni hilo. Iko Serikali hakuna? Linaliona kwa nini yanafanyika yale?

Jambo jingine juu ya ardhi nchi Coast. Maswota thamanini kwa mia ninaamini wako jimbo la Pwani. Lakini kura zote za viongozi kule huja wakataka kuchukua Pwani, lakini bado maswota wengi wako hapa Pwani. Katiba iko? Iko. Inasema mtu akiketi katika ardhi fulani miaka kumi na mbili asilipe tena. Iko? Nikanusheni. Iko? Na kwa nini tunalipa? Ikiwa ni miaka kumi na miwili nimelipa miaka hamsini, miaka thelathini na nane nimelipa pesa za haramu, nitalipwa na nani? Sasa hiyo (inaudible).

Hali kadhalika,kuna vitisho vinatoka katika ma-agent. Wanakwambia nitakuuzia nyumba na wanauza nyumba za watu bila kuchukua karatasi za kortini kuonyesha nyumba imeuzwa, anakuja kukuuzia. Mama anaanguka ana faint anakufa. Na hili liko,

Serikali iko inaliona.

Lingine, ninazungumzia habari ya polisi. Leo unapokuwa unasafiri usiku, watoka free town mpaka Nyali na wahuni wamejaa. Utafika Nyali? Ukipiga simu Nyali unaambiwa gari hakuna. Ukienda wewe Nyali unaambiwa weka mafuta, Serikali haina mafuta siku hizi. Nani mwenye kuumia? Mwananchi, lakini kura zitoke hapa, hapa kwetu, kura zitoke hapa, twakataa. Ndipo ndugu angezungumzia habari ya majimbo ni kweli.

Tuliambiwa Wamaasai walikwenda katika kiwanja cha (?) huko kwao, Narok, wakazingira kile kiwanja wakasema mtatuwandika kazi hamtwandiki? *Ero*! Tunataka kazi… Wakaandikwa kazi, Wamaasai.

(***End of tape***)

Haya yote ninayatoa kwa sababu Serikali haituthamini. Inathamini pesa za korti, refinery na ma hoteli na kuleta watu wao kuja kuwaandika. Sisi tubaki hapa kama watumwa, kazi kuwapigia kura tu. Ndivyo twasema, katika umri wangu wa miaka hamsini na nane, nasema nalikataa na wananchi mkatae!

Kisha ninazungumza juu ya uhuru wa kuabudu. Uhuru wa kuabudu umechafuliwa nchini Kenya. Kwa nini Waislamu tunyamaze kimya, Wakristo tunyamaze kimya ikiwa mwanawe anakwenda tupu uchi? Baba wataka kuchungulia mwanao? (?) na hata husemi! Wakristo twanyamaza, Waislamu twanyamaza! Imekuwa mpaka leo watu wakienda makanisani ajipamba ka ambaye Yesu ataka girlfriend!

(***Laughing and clapping from the audience***)

Wajipamba wale kabisa! Wale kama ni bibi arusi waingia kanisani! Uhuru wa kuabudu huo. Katiba yetu tafadhali ichunguze vitu kama hivyo. Vichunguzwe sana. Na hatutaki kuona gari ya polisi mtaani ikiinga, ukiona imejaa ni walevi watupu na kortini hafiki! Jamani poleni kama kuna mlevi hapa, nitakusema bure tu.

(***Laughing from the audience***)

Akichukuliwa akifika Nyali apigwe fine arudi nyumbani, kweli urongo?

**Response from the audience**: Kweli.

**Harry Philip Mbai Njoro Ali**: Polisi wamekuwa korti. Serikali haiko haioni. Nimetembea bara mimi bwana, nimeona kunavilabu! Leo unashikwa wewe unaambiwa unakula pombe ya haramu, bia tu, pombe ya haramu. Kwa Mwenyezi Mungu,

pombe yote ni mbaya. Serikali wafunge viwanja vyote (inaudible) vifungwe. Ikiwa hawtaki mnazi uendelee.

(***Clapping from the audience***)

Nasimulia kisa wakati (inaudible). Alisema ya kwamba, kuwe na Coconut Board of Kenya, mnazi ulindwe na sheria za nchi! Mnazi ule umefanywa vile? Kahawa ina Board, pyrethrum in a board, chai ina board, mnazi patupu. Kwa sababu watoka wapi? Watoka Pwani!

(***Laughing and clapping from the audience***)

Wayakataa hayo? Mheshimiwa haya maneno (Inaudible) kuna chuki. Hatuna chuki na mtu wa bara. Serikali iliyopita ilituambia hakuna cha bure! Ronald Ngala akasema, kusema vile (in vernacular). Ma hoteli yote kule yamechukuliwa na nani? Wamemlipa nani? Na sisi tungali maskwota. Lamu kumepelekwa watu (inaudible). Wamemlipa nani? Wamemlipa nani? Hawakulipa! Tumeambiwa hakuna cha bure huku vitu vyatolewa. Lakini Ngala alisema (in vernacular). Hatwafukuzi lakini wajipe katika jimbo la Pwani, watulipe katika jimbo la Pwani. Ama sivyo mtapokea chuki viongozi na haya yasemwe, hakuna kuogopa. Ikiwa mmetuita hapa na tunauhakika tuko free, haya yasemwe.

Lingine ni juu ya Local government. Imekuwa ni desturi ya manispaa kuingia mjini (?) kwa mtu aliye na title deed yake, mama amabaye hata hajiwezi, amefiwa. Ama ni mtu ambaye (inaudible) anaambiwa atoe pesa (?) sheria hiyo ilitoka wapi, mtu mwenye title deed ku…(***Laughing and clapping from the audience***).yatoka wapi? Wazee (?) wa town wako hapa na watu wanaona. Title deed unayo, manispaa inakuja inakwambia wewe ni lazima ulipe ama nyumba inauzwa.

Mabwana Commission, tabia hii tunatishwa na municipal kupitia kwa Bwana Jagani. Kama mnauwezo wa kumkanya mumkanye. Kwa sababu leo nikichukua hatua wewe utakuja niambia sikukuambia hivyo! Lakini umetosheka?

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Asante mzee.

**Harry Philip Mbai Njoro Ali**: Ninakushukuru mzee mwenzangu lakini, dakika tatu ni kidogo.

(***Laughing, clapping and ululation from the audience***)

**Com Pastor Zablon Ayonga**: Bakari Baya, mzee. Tafadhali tuwe kimya tumsikie Mzee Bakari Baya.

**Bakari Baya**: Ni mimi ndio mzee Bakari Baya. Hamjambo?

**Response from the audience**: Hatujambo.

**Bakari Baya**: Mimi nimebahatika kufika hapa leo kwa kutoa maoni na nina maoni ambayo sasa hivi pia ninaona haya kuzungumza kwa maana yote yashazungumzwa! Kulikuwa na Mkamba huko kwao akaja Mombasa (inaudible).

(Interjection) **Com Pastor Zablon Ayonga**: Mzee mulikia tu.

**Bakari Baya**: Hapo, Mkamba akasema *asi*, nilikuja kuonyesha meno yangu lakini sasa imekuaje?

(Interjection) **Com Pastor Zablon Ayonga**: Tafadahali…njoga kidogo mzee. Katika democrasia iliyoko, huyu anapoongea, wengine wote tumenyamaa tumsikilize. Sasa nyiyi wale mnatutupia maneno mmuambia asimame, hana haki ya kusimama. Akitaka kusimama kama yule mzee mwingine ni uchaguzi wake. Lakini sisi tuna kiti ambacho angeketi. Uchaguzi ni wake. Nyinyi kimya mmusikize.

**Bakari Baya**: Poleni kwamba singesimama kwa sababu nimekuta mtu wa kwanza amwekaa na mimi kama nilivyofundishwa nimeambiwa nikifika mahali, wenyewe wakiwa wamekaa, na mimi pia nikae. Kwa hivyo tafadhalini nimekaa, ninataka nitoe maoni yangu. Tafadhalini ndugu zangu mnisamehe kama nimewakosea.

Nimetaja Mkamba kwa sababu Mkamba yule alileta uzuri Mombasa (inaudible), hiyo sijatukana mtu ni mfano. Pili, nikitoa huo mfano, ni mifano mingi sana ambayo iko. Tuliona maana mimi sasa hivi nina miaka sitini na mitatu. Nimezaliwa 1938, August. Huu ni ugonjwa tu, ni wa maradhi ya pumu, asthma, lakini bado kijana. Nikivuka barabara, twaenda tu.

Kwa hivyo, agenda zangu nilizokuwa nimezipanga nizizungumze, zimezungumzwa lakini nitazizungumza tena kwa sababu hapa kutoka zamani sana tunalia ya kwamba, tunasikia ati kwaja Katiba mpya lakini maoni yetu tukikaa majumbani mwetu au tukienda maofisini mwetu ama tukitembea, tunasema Serikali moja imetuchokesha, tunataka majimbo. Tukiwa tunataka majimbo, majimbo yale yale yakiwa yatakuja, yawe na waziri mkuu, na governor wake na mabaraza yake, yale, yale mawili kama ilivyopangwa kutoka huko Lancaster House hapo mwanzo.

111 – end of my work(Lillian)

Pili, tuna mashamba yetu ambayo tumekaa sisi hapa. Mimi nimekaa mahali hapa kutoka mwaka wa arubaini na tano mpaka

leo, ninaumia sana, mara ninafuatwa, ninambiwa wewe umekataa kulipa? Utashtakiwa, (?) mashtaka. Wale wazee hawakuniambia vile ni kwamba hawa mimi nina mahali pangu, sina nyumba, mpaka upige magoti ndio uingie ndani, na ni kwangu simfichi mtu.

Kuna wengi sana walikuja wakaniambia, mzee unauza nyumba? Nikawaambia kamuulize mamako, umwambie hivyo mtu mwingine kwa sababu hii ni matusi. Mgonjwa akiwa mgonjwa huombewa apoe, humwombei afe. Tunaelewana?

Hapa ikiwa tunaelewana hapo, nishapata watu wengi kwangu. Mzee, ma-Commisioner hamjui kwangu lakini kwangu kama ni wale watu wa tamaa, siku hiyo pia mimi ningeshika mapanga nikaanza kunyaganya watu, kwa maana sina kitu. Ni nalala nje. Pia mimi ninatosheka kwa sababu mimi nimechukua mfano wa Mwenyezi Mungu. (In Arabic). Mwenyewe alipopata utume kutanganza Usilamu kuutanganza kwa Wasilimu alipewa utajiri akaukataa. Leo utajiri ndiyo wa tumaliza. Hayo yote yako na ni

mengi yako lakini sitwanza kuendelea kuzungumza mengi.

Tunataka Serikali Katiba ijayo iwe ya Majimbo na iwe na Waziri Mkuu wake,na Governor wake, na ma-senetor wake. Na wa wajumbe walioko sasa au watakao kuja baadaye pesa wapatazo ni nyingi sana. Watu wanakula sima la papa, wao wanapata million, million, million! Wana kazi gani kule wamefanya?

(***Laughing from the audience***)

Wabunge wa sasa wapukunzwe chini kabisa pesa zao wanazopata zipewe… wapewe hata laki tatu, tatu, tosha kabisa. Kwa sababu waende kutudanganya huko kwetu ah, basi mimi nikienda, mwajua nitaleta reli, lakini (inaudible) is bila reli, kule kuna bahari bwana! Ukitwambia utaleta train Mtwapa, Kijipwa huko, (?) utatudanganya wewe, utaipitsha wapi reli hiyo?

Daranja hilo limekaa siku nyingi kwa bahati Mjapani akaja akatuokoa. Tulikuwa tunazile ambazo zinaitwa ferry, sijui ni zile za kusukumwa na kamba zile. (in vernacular)

Sasa hapo ni kwamba wale Wabunge sisi twatoseka nao kwa sababu twapenda tunawapa kura lakini tukishawapatia kura halafu hutunyanyasa. Wakifika huko Bunge, wajiongezea mishahara. Wasijiongezee mishahara wenyewe hao Wabunge. Utandikwa na tajiri uongeze utajiri ati, si wewe mwenyewe (?) Utazichukua zote wewe! Kwa hivyo sina mambo mengi, ningetaka kuyasema lakini yashasemwa yote kwa hivyo asanteni Commissioner na ndugu mlioko hapa. Asante sana.

**Com. Pastor Zablon Ayongo**: Asante. Unaweza kuja ukaweka kidole.

**Bakari Baya**: Nitaweka kidole.

**Com. Pastor Zablon Ayongo**: Mwana Idi Juma, basi kama yuko na wakati anakuja nataka Masumbuke awe tayari. Ajetayaresha baada ya huyu mama. Mama una mandishi? Okay, unaweza kutoa maoni yako.

**Mwana Idi Juma**: Jina langu ninaitwa Mwani Idi Mohammed Juma.

(Interjection) **Com Pastor Zablon Ayonga**: Tafadhali mumwachie nafasi yake na sauti yake.

**Mwana Idi Juma**: Nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia maoni. Maoni yangu ni machache kwa sababu mengi naona yashazungumzwa na wenzengu ambao nilikuwa na mimi pia nataka kuzungumzia. Lakini madogo ambao nitakayo yachangia hapa ni kutokana na mambo ya Chief kwa sababu tuna matatizo kwa mambo ya ma-Chief.

Tunavyo pendelea maoni yangu nilikwa napendalea Chief awe ni mzaliwa wa pale katika kijiji kile amejua watu abapo ikuwa mtoto yeyete atakwenda kwa Chief au mtu yeyote katika kijiji kile atakwenda kwa Chief awe Chief yule yuamjua kiurefu. Kwa hivyo akijitaja yule mtoto ikiwa hakumwelewa akimtaja baba yake aweza kumwelewa, akiwa hakumwelewa baba akimtaja babu/nyanya yake atamwelewa. Lakini ikwa ni Chief ambaye anayekuja hajulikani kwao ni wapi lakini amekuwa Chief pale kuna matatizo mengi. Kwa hivyo kuna watoto wengi wapata taabu na ni watoto wa pale pale na wazazi wao ni wa pale pale, na pia nyanya zao na babu zao lakini ma-Chief hawawajui

Kwa hivyo maoni yangu nilikwa napendelea ma-chief wakuzaliwa pale pale au mwenye kuja akawa ameishi kwa maisha marefu katika kijiji kile. Kwa maana ma-Chief wamekuwa watumia wazee wa mitaa ambao wazee wa mitaa ndio wafanya kazi zetu kuliko ma-Chief wenyewe. Kwa hivyo, maoni yangu ni kuhusu ma-chief na kuwasaidia watoto, au mtu yeyete anayetoka katika lile kijiji lakini hamuelewe sasa inakuwa wanamusubua sana.

Na wazee wa mtaa wanafanya kazi nzito kuliko ma chief ambao wao ndio wanaojua watu wanaoishi pale, wazazi, watoto, vijana. Kwa hivyo ma-chief ni lazima wachaguliwe kutoka kile kijiji. Na ma-chief, uchaguzi uje kwa mlolongo kama zamani mimi nikiwa mtoto niliona ma-chief wanachaguliwa na wananchi wa kijiji kile, tena kwa mlolongo, chief wanayemtaka kwa sababu ndiye atakayekuwa anawajua. Maoni yangu nafikiri ni hayo kwa maana mengi yashazungumzwa.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Asante mama Mwana Idi, unaweza kuja hapa ujiandikishe. Masumbuke, Kuna mtu aliye na jina linalofanana hilo? Basi hayuko, atakapo patikana atasema. Amina Mwinyi.

**Amina Mwinyi**: *Assalam aleykum*!

**Response from the audience**: *Aleykum salam!*

(Interjection) **Com. Pastor Zablon Ayonga**: Wakati huyu mama anapo jitayarisha nataka Pastor Makwaya awe tayari.

**Amina Mwinyi**: Jina langu naitwa Amina Mwinyi natoka hapa hapa Kisauni. Katika maoni yangu nashukuru Mkuu wa hii Commission kwa kutufikia na kutusikilinza maoni yetu katika Kisaunu hii, shukurani kubwa.

Kwa hiyo mimi langu la kwanza katika Kisauni nikiwa ni mama wa Kisauni, maoni yangu ni kwamba sisi wananchi wa hapa Kisauni kama Kisauni division tungeonelea tuukataye (?) japokuwa umezungumzwa na watu wengi na watu wengi wametoa maoni yao kwa pendekezo hilo maanake linaumiza wananchi wengi wa hapa kwetu Kisauni.

U-squatter tuukatae kabisa na ikiwa wewe mwananchi umezaliwa hapa na unataka haki yako ya kuwa wewe ne raia wa Kenya, na unataka huu uraia wa Kenya kweli umezaliwa hapa, na uko katika u-squatter, yaani unchangia umaskini mkubwa katika hii division yetu wa Kisauni.

Tunakuwa ni watu ambayo hatujewezi kwa sababu ya u-squatter. Umeenea sana sana hatuna haki, hatuna nguvu na imani ya kushi kama wenzetu. Kwa hivyo tungeomba mtusaidie na tuwe na haki kama wenzetu, tukiwa ni kina mama wa Kenya, tukiwa ni waume wa Kenya, tuwe ni raia wa Kenya, huu u-squatter uondeke na kila mtu apate haki yake kama mwananchi wa Kenya.

La pili ningeomba kwamba kila mkoa upate Chuo Kikuu. Tupate chuo kikuu katika Pwani hii na kila mkoa.

La tatu tungependelea sisi wazazi ambao ni kina mama katika Pwani tunapata shida kubwa ikiwa ulevi ni wetu sisi kina mama, tunazaa watoto, na watoto ndio wanapata shida, wanapata taabu kwa sababu ya kitabulisho, kwa sababu ya pasipoti , tungeonelea sisi kina mama taabu hii maanake mzee anakwenda kutafuta riziki, mzee anakwenda katika shughuli za kazi, ktututafutia mkate wa kula. Lakini wewe mama unayebakia na yule mtoto unahangaika naye mpaka unashindwa hapati kitabulisho. Tungeomba iwe kwamba mzazi akimzaa yule mtoto apewe haki ya kuwa ni mwana raia wa Kenya.

Apati kuidhinishwa yeye ni Mwana Kenya, kuliko kukaa miaka kumi na nane aanze kuhangaika kitabulisha wengine wanamjua wengine hawamjui inaleta shida kubwa kwa mwananchi kupata haki yake, ku-vote ama kupiga kura. Miaka kumi na nane amefikisha, kura zimechukuliwa, hakupata kitambulisho. Lakini ikiwa atapata haki yake, siku ya kuzaliwa anapata uraia wa Kenya atasaidika mambo mengi.

La nne, tungetaka huduma za afya na za skuli ziwe bure, kwa kuchangia umasikini ambao umeingia Kenya kwa sababu ya

maradhi ni mengi mtu hana njia ya kujisaidia, hana kazi hana chochote na anaenda hospitali hatibiwi. Ana mtoto anapeleka hosipitali apati kutimbiwa maafa yanakuwa mengi. Tungeomba huduma, hospitali za Serikali ziwekwe kiwago cha kuwa mwana wa chini aweza kujisaidia, ama iwe bure kabisa. Na elimu kwanzia class cha kwanza mpaka nane mtufikirie watoto pia wawe wanasoma bure angaa waweza kuondoka katika hali ya umasikini, na kutojua kusoma kidogo.

La tano, Tungetaka sisi kina mama hali zetu ni hadhifu kumenyina na ma-bwana kama nyinyi mulipewa kipawa cha kutumiliki, na Mwenyenzi Mungu akawapa hali ya nguvu. Sisi tungeomba kina mama katika hii Ubunge maalimu, na Udiwani maalimu, wangeachiwa kina mama wakapewa jukumu hilo la kutumikia katika Ubunge ama katika U-councilor. Tungeomba sisi kwa maana kumenyina na akina baba huwa tunashindwa lakini tutaminyana na pia mtuaangalie katika haki hiyo ya ubunge maalum tupatiwe. Asante.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Asante mama, kwa mawazo yako, tafadhali uende kule ujiandikishe. Mwingine ambaye atamfuata ni M.V. Mbunga. Ongoja kidogo, nani ni nani?

**Mkwaya Raymond Chengo**: Asanteni, mimi kwa majina ninaitwa, Mwakwaya, Raymond Chengo sio Pastor kama ulivyo nitaja Bwana Commissioner.

**Com Pastor Ayonga**: Jina nililonalo hapa…

**Mkwaya Raymond Chengo**: Jina ndio hilo hilo, lakini hilo pastor nafikiri ni lako wewe. Limekuwa refered kwako hilo.

**Com Pastor Ayonga**: Endelea, nimeelewa sasa.

**Mkwaya Raymond Chengo**: Asante sana. kwa majina ninaitwa Mwakwaya Raymond Chengo. Nitaongea mambo matano kwa haraka sana maanake naona wakati umekimbia sana. Mwanzo nitongea juu ya Katiba, pili nitongea juu ya elimu, tatu nitongea juu ya Utali nne nitongea juu ya ardhi, tano ni taongea juu ya vijana, sita ni mambo ya pamoja, ambao sitayataja watajisomea wenyewe.

Mwanzo Katiba yetu ya Kenya imeandikwa katika lugha ya Kiingereza ambao ni lugha ngumu kuweleweka kwa urahisi. Yaani imeandikwa katika lugha ya kitaalamu ngumu sana. Basi vijana wanapendekeza Katiba hiyo iaandikwa katika lugha ya Kiswahili na hata kama ni ya Kiswahili hivo hivo ni irahisiswe zaidi. Maanake Kiswahili nacho uwa kigumu wakati mwingine, pia ifundishwe katika shule za Sekondari na Primary na iunzwe reja reja. Ipatikane hosipitali, mahatolini, mosque, churches, na kila mahala.

Jambo la pili ni kuhusu elimu: elimu ya mfumo wa 8-4-4, si nzuri kwa Serikali yetu ama kwa nchi yetu ya Kenya, ivyo basi

imekuwa ngarama sana mzazi kuelimesha ama kuwaelimisha watoto wake. Pia vile vile elimu hiyo imewafanya walimu wakuu kuwa wajeuri sana, hata Wizara inapoamua kuwa school fees zipukuzwe Walimu Wakuu wanakataa.

Tungependekeza hivi elimu ya shule ya Primary iwe bure lakini ile ya shule za upili malipo yake iwe ya nusu maanake ngarama za uchumi zimekuwa juu hatuwezi kusema elimu ya shule za upili iwe bure. Hivyo basi wazazi wapeleke watoto wao shule kwa lazima, na mfumo wa nane nne nne utupiliwe bali turundishi ule mfumo wetu wa zamani, na walimu wasiwe waandishi/Secretaries wa BOG, PTA, ama Kamati za Shule , wazazi wenyewe wasimamie mirandi hiyo yote, na wachaguwe Secretary na walimu wabake walimu tu.

Examinations, vieti vitolewe tu kwa wali ambao wamehitimu, wamesoma kutoka darasa la kwanza mpaka lile nane, apatiwe cheti, si mtu akae nyumbani ikifika siku ya mutihani ananunue mtihani anafanye na anaapatiwe cheti, si sawa hiyo, inafanya watoto wasiende shule kila mtu ategee wakati wa mtihani ndiyo apate cheti. Serikali ipige marafuko vile shows ambazo zina onyeshwa katika vibindi vya radio, hazivaye kwa watoto na vina tabia mbaya. Kila Wilaya iwe na National School, na kila mkoa uwe na University lakini hapa Pwani ziwe mbili kwa sababu tunaona kumekuwa na muchanganyiko wa ma-kabila tofauti, tofauti ata tukisema University moja watajaa wale wa bara, sisi tutakosa sisi tutakosa.

(***Clapping from audience***)

Swala la tatu, ningependa kuzungumzia juu ya utalii: Utali utakuta sana sana uko hapa kwetu lakini zile sehemu ambazo zinafanyia Utalii, ziko tu un-different, na utali unatia pesa nyingi katika Serikali hii yetu, hivyo basi nengisema hivi pesa zote zinapatikana na shuguli za Utali, asirimia arubaini iregishwe huko huko apapo kumetoka hizo pesa, ziwe sinasidia ma-shule, serikali, barabara mandeleo yote ya mitaa ya kutoka pale pale apapo sehemu ile ya Utali imetoka. Vile vile Chuo cha Utalii kijengwe kule, apapo kule Utali umetoka kama vile Utali College, “tafadhali na endelea kumaliza Bwana Commissioner.”

Nikimalinzea ni ta zungummzia swara la aradhi, aradhi ndiyo chanzo cha shinda kubwa, kuna land clashes, na hii yote ni sababu ya kuwa ne irregular issuing of land. Na pia hivo hivo tungependekeza hivi. Kila kabila ikaye mahali pake apapo Mwenyenzi Mungu aliwapangia kuishi. Ikiwa mtu atataka kufanya kazi inje ya pahali pake awe kama mgeni halafu kitu ingine mtu isiruhusiwe kuanza shamaba rahisi hivi hivi , kiwango cha kunza shamba kwa mtu ama mtu kununia shamba iwe acre kumi. Na mtu kununua ama kunza shamaba kwa Commercial use ziwe acre hamusini pakee yake. na pia vile vile unajue aradhi haiongezeke na wanadamu wanaongezeka kila kukicha. Hivo basi tungependekenza hivi. Kila familia iwe inawenza kuruhusiwa kuwa na watoto wawil pake yake.

**Interjection**: Kicheko.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Hayo ni maoni yake.

**Mkwaya Raymond Cheko**: Hivi tunaona kwa sababu hata tunapo zaa watoto wengi, watoto ndiyo wanapata shinda si nyinyi wazee. Tena tu-discourage polygamy. Polygamy pia inaleta musongamano wa watoto na inafanya watoto kuwa wana rada rada ovyo ovyo. Tafadhli Bwana Mwenyekiti ni malezia.

Youth wamekuwa wakitesika sana hivyo pasi wamjetupukinza katika drug abuse, child labour, early marriage, abortion, prostitution. Tungependekeza vijana kuwe na Tume ya kushugulikia mambo ya vijana. Tume hii ietwe Nationa Youth Commission. Tume hiyo itangalia mambo ya elimu ya vijana, employment, sport, health na politics.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Asante, asante munda wako umekwisha naukapita. Tumpe maandishi ili umesema uko nayo. Mohamed Omari Mugumba.

**Mohamed Omari Mugumba**: Kwanza Ni na ombi kupitia Tume hii ya Marekibisho ya Katiba ikwa mtaniruhusu ndiyo ne endelee kutoa maoni yangu Pointi mbili pakee yake.

Ombi langu ne kwamba ile tume ya Njonjo muiyambie irundi hapa kama vile mulivyo kuja nyinyi leo. Ilikuja lakini haikukuja Kisauni, na haya maoni yote ambayo ni nayo toa hapa yanaumiza wakanzi wa Kisauni Kwa hivyo ningeomba Tume hiyo ya Njonjo inje hapa Mlaleo Primary School kama vile mulivyo kuja nyinyi. Kwa sababu matatizo yote yalifanywa na huyu Njonjo na tuna maswali ya kumulinza.

Kwa hivo Pointi zangu ni pili tu: kwanza na sikitika kuwona kwamba Katiba iliyoko sasa na Serikali iliyoko ilitilia manani sana wanyama, kuwapa makao kuliko binadamu, kwa sababu wanyama wametengwa buga zao kule na huwenzi kusikanyaka, ukikanyaka unasitakiwa lakini binadamu ndiyo ambayo wamewachwa nyuma mpaka tunaabia tu-masquanter.

Hasa nikezungumzia zaidi ni Pwani nzima lakini zaidi hapa upande wa Kisauni, kwa sababu aradhi hizi za Kisauni zilitolewa zamani sana na hayo waliopewa aradhi hizo hawako tena ulimwenguni, wali walio shikilia ne watu ambao wanatunyanyasa hivi sasa ambao wanataka kutulipisha kondi ya kila mwenzi.

Kuna sheria apabo sijue hii sheria ilitoka wapi ya kwamba ati a House without Land. Nashangaa mimi maanake ata mumia mwenyewe umemie chini ya aradhi hii nyumba ambayo inaampiwa a House withou land ne sheria ya ina gani.

Pili nikimalenzea katika zile pointi zangu pili nilizo sema ne khusu mambo ya ma-dalali, au Auctioneers. Katika hayo ambayo wametunyanyasa kwa mambo ya kulipa rent wao upitia kwa Madalali na wanatutia ngarama sana kwa sababu wanapitia katika hawo Madalali na kutaka kunza hizo nyumba zetu ambazo tumejenga katika aradhi inzi ni nazo zizungumuzia , hawapitii katika njia ya sawa.

Hili ndilo lime ni fanya ni kasema kwamba wa tume ile,-- tume ya Njonjo inje kwa sababu hawa Ma-Actioneers kama hakuta-chukuliwa hatua haraka, bila huu mwaka kumalizika basi kuna wengine baadhi ya Ma-Actioneer tuta wapiga mpanga sisi. Ni hayo tu.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Pita hapa kwanza ujiandikishe. Ninani? Abudalla Hamisi,

**Abudalla Hamisi**: Yangu yote nilio kuwa kuwa nao yamezungumzwa, lakini na ya tilia nguvu kwa tu tunataka Majimbo, Majimbo manane yaliyo na nguvu sawa sawa. Kila Jimbo, kile kinacho toka pale kiwe kinagawiwa wao kwanza yaani sabini na tano ziwe ni zao na ishrini na tano Serikali ipewe.

Vile vile katika Ndini: Ndini ipewe nafasi nzuri sana, Ndini zote wa wenze kujipangea mambo yao ya Kindini maanake wana vitabu vyao na wafuate vitabu sawa sawa, bora tu Serikali itoe nafasi sawa na ya ki haki. Sina Mengi.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Asante sana Bwana Hamisi tafadhali ujiandikishe kule. Tunajua maneno yako imeingia. Anaye fuata ni Kibwana Abudu, (wengi hawako).

**Kibwana Salimu**: Salaamu Malaiko Mara (Arabic--------------). Naishe Kisauni, Madhumuni yangu ya kusema hapa ni kuwatetea Waisilimu. Waisilamu wanadhurumiwa, hawapati haki zao sawa sawa. Waisilimu katika mkorti wahukumia bila Sheria ya Kisilamu. Na Waisilamu hawana haki yoyote. Kwa hivyo twaomba Tume hino itufanyie sisi Waisilimu Korti letu na Ma-Judge wetu na Ma-Officer wetu. Hatutaki kuhukumia katika Korti lingine ambalo si la Ki-silamu.

Jambo la pili, katika hapa Kisauni, Kusema kweli twaonewa, kwa sababu sisi tunaishi kama ma-squantta zaidi ya miaka tharathin na tano, na twalipa kondi, na yule unaye mlipa kondi hakuhudmie kwa kitu cho chote, mwisho akufungia nyumba ata upepo pahli abapo unakaa hupati. Nderisha ukifungua wagoka nyumba la mwingine. Mvua ikinyesha maji ya ingia kwa nyumba. Ukimwabia mwenye kondi akwambia "wataka kaa hutaki funga nyumba yangu." Ulipo anza kujenga ulimpa pesa karibu elefu hamusini za kujenga. Pesa zenye unampa hazina kazi zinafanya unampa tu mbure, na kila mwezi ataka shilingi mia tano.

**Com. Pastor Zablon Ayonga**: Asante sana Mzee, Hezron Juru. uko na maandishi?

**Hezron Juru**: Ndiyo niko na ma-pendekenzo na maoni. Ya kwanza ne kuhusu Electoral Commission, ya pili ni Type of Government, ya tatu ni political parties , ya inne Senior position in Judiciary and Parastatal Organizations, ya tano ni Justice na ya sita ni corrupation, ya saba ne labour law, ya nane ni education, na ya tisa ne khusu Parliament.

Ya kwanza ni khusu Electoral Commission ningependelea Commissioners wa Electoral Commission wawe appointed na Parliament, na Parliament pia e-vett wali Commissioners. Pia Commission ipewe nguvu ya ku-prosecute Election Offenders.

Provincial Administration should be de-linked from the activities of the Commission.

Type of the Government. I would recommend a Government of National Unity, na President asiwe above the law.

Viama via Kisaisa vipatiwe pesa kutoka Conslidated Fund.

Senior Position, Ma-judge wote na wali wanachaguliwa ku –learn Parastatal Organizations all appointees should be ventted by the Parliament for competence.

Justice: Kuna wakati mwingine utakuta kasi iko kortini na Attorney General ana-tuma Prosecutor na kitu kinaitua nol pro seque, katika sheria iliyoko sasa, Attorney General hatakikani kusema kwa nini ana enter nol pro segue yaani kumalinza ile kasi kabula haijaisha. Mimi ningependelea Attorney General akimalinza kasi aseme ni kwa nini, kwa sababu hii inampa frusa ya kutumia hiyo previlage vibaya. Maanake pengine anwenz kuwa ni rafiki yake ama ni mtu well connected in politics.

Nguvu za Magistrate and Judges, wakati nilikuwa na andika hizi report zangu, saa hii kuna kasi imekuwa ruled kule Nairobi. Mtu ame-rape mtoto wa miaka minne na ni kama amewachiliwa huru na hali sheria katika Katibu inasema anatakikana afanywe nini? he should be jailed for fourteen years lakini kwa saa hii amewachiliwa kwa sababu Judge/Magistrate ametumia Discrational powers hizo ningetaka ziangaliwe vinzuri sana. Haki itumike.

Corrupation: Utakuta sasa kama kortini, wengi wanjua ukiwa na pesa ata kama umefanya kasi gani unwenza kuachiliwa bora tu mfuko wako ni mzitu. Pia ningependa, kuna mtu anaitwa Auditor General, ambaye anahesabu pesa zenye zimetumika na Mawinzara ya Serikali. Kila mwaka anatoa reporti lakini ile reporti haishugulikiwe, hatujapata kusikia mtu yeyote ameshikwa na anakuwa prosecuted kulingana na reporti ya Auditor General. Tungetaka mtu ye-yote ata kama ni nani, ikiwa ni Cabinet Minister, achukuliwe hatua.

Pia ne nge-recommend tuwe na Offisi ya Ombudsman. Hii ndiyo sisi Wananchi wenyewe, wananchi wa kawinda, pengine umeona Polici anahongwa, kama ni Traffic Police Officer unawenza kwenda reporti, kama saa hii ukienda kutoka hapa, Commissioners mukepata nafasi muende (in-cognate) utakuta all the way, ni kitu kinasitikitisha vile wanachukua pesa., vile conductor anaakusha pesa , na matatu inaondoka na hali tunaona zile number za wali Polici. Kama tukepewa ouwenzo kwe na Offici neutral tuna wenza kwenda ku-reporti na yule Offiser achukuliwe hatua.

Wakati mwingine pia utakuta kama ni Polici Station yule mkubwa may-be saa ingine amefirisika anatuma ma-polici wake huko mitaani kushika watu na wanapelekwa kama ni Nyali, na anajua ikepeleka idadi ya watu kama mia moja kuna rate ile ameweka pali. Unajua kama ni mfanye kazi ukipelekwa kortini nayo kazi kule utapoteza. Sasa umewekwa idadi pali may be it ranges from K.shs.500/= to K.shs.2000/= hiyo watu wanatoa. Unakuta kuna kitu inaitwa Drank and Disoderly unakuta saa hiyo pengine wewe ata hunywe pombe na umeshikwa umepelekwa Nyali, kama you don't buy your freedom utapelekwa Kortini.

Ukipelekwa Kortini yule Magistrate haulinzi yule Polici reporti ya Dakatari kuonyesha ulishikwa ukiwa mulevi. Na sheria mimi na fikiri ina sema ni lazima you prove ulikwa mulevi.(marudiyo).

Katika Labour Laws zetu ningeteka pia sifafanuliwe, Labour Laws zetu ziko kwa kitabu lakini hazitekelenzwe, unakuta unfutwa kazi, kasi inapo chukiliwa na Union inaenda Industiral Court inachukua ata miaka mitatu hupate Justice nu huko familia yako inateseka na hujui hiyo kasi itakwa ruled na muna gani. Ningependelia hiyo kasi iwe ruled as fast as possible.

Pia kuna kitu

End of tape 2.

**Tape 3**

**Com. Prof. Ogendo:** …………………(inaudible) Ali Taabu Azaa, ajitayarishe. Uko na maandishi?

**Ericson Njiru:** Niko na maandishi.

**Com. Prof. Ogendo:** Kwa hivyo tafadhali umulike juu ya maandishi.

**Ericson Njiru:** It is okay, jina langu ni Bwana Ericson Njiru. Niko na mapendekezo na maoni.

- Ya kwanza, ni kuhusu Electoral Commission;
- Ya pili, type of government;
- Ya tatu, swooping of political parties;
- Ya nne, senior positions in Judiciary, Parastatals and ……… (inaudible);
- Ya tano, ni justice;
- Ya sita, ni corruption;
- Ya saba, ni labour laws;
- Ya nane, education;

- Ya tisa, ni kuhusu Parliament.

Ya kwanza, kuhusu Electoral Commission: ningependelea commissioners wa Electoral Commission wawe appointed na Parliament, na Parliament pia …….. (inaudible) wale commissioners.

Pia, Commission ipewe nguvu ya ku-prosecute election offenders. Provincial Administration should be delinked from the activities of the Commission.

Type of Government: I would recommend a government of national unity, na President asiwe above the law.
Vyama vya kisiasa: vipatiwe pesa kutoka consolidated funds – vyama vyote.

Senior positions: ma-Judge wote na wale wanachaguliwa ku-run parastatal organizations, all appointees should be vetted by the Parliament for their competence.

Justice: kuna wakati mwingine utakuta kesi iko kortini, na Attorney General anakuja na kitu, anatuma prosecutor na kitu kinaitwa "nolle prosequi", na katika sheria ilivyo sasa, Attorney General hatakikani kusema kwa nini ana-enter "nolle prosequi", yaani, kumaliza ile kesi kabla haijaisha.

Mimi ningependelea Attorney General, akimaliza kesi, aseme ni kwa nini. Kwa sababu, hii, inampa fursa ya kutumia hiyo privilege vibaya, maanake, pengine anaweza kuwa ni rafiki yake, ama ni mtu ambaye anapendelewa ki-politically. He is well politically connected.

Hiyo ingine, ni kuhusu mitigation of powers za Magistrates and Judges. Wakati nilikuwa naandika hizi report zangu, saa hii kuna case inakuwa ruled kule Nairobi, mtu ame-rape mtoto wa miaka mine, na ni kama ameajiliwa uhuru. Na hali sheria katika kitabu inasema anatakikana afanywe nini. He should be jailed for 14 years, kama sikosei. Lakini, saa hii ameachwa kwa sababu Judge or Magistrate, ametumia discretional powers. Hizo, ningetaka ziangaliwe vizuri sana. Haki itumike.

Pia, hii ni kuhusu corruption: utakuta sasa kama kortini, saa hii, wengi wanajua, ukiwa na pesa, hata kama umefanya kesi gani, unaweza kuachwa, bora tu, mfuko wako ni mzito.

Pia ningependa, utakuta kuna mtu anaitwa Auditor General ambaye ana-audit pesa zimetumika na ma-wizara za Serikali. Kila mwaka, anatoa report, lakini ile report, haishugulikiwi. Hatujapata kusikia mtu yeyote ameshikwa, amekuwa prosecuted kulingana na report ya Auditor-General. Tungetaka mtu yeyote, hata kama ni nani, ikiwa ni Cabinet Minister, ikiwa ni nani, ajukuliwe hatua.

Pia ninge-recommend, tuwekewe office ya Ombudsman. Hii ndio kama sisi wananchi wenyewe – wananchi wa kawaida. Pengine umeona polisi anahongwa, kama ni traffic police officer, unaweza kwenda ku-report. Kama saa hii ukienda kutoka hapa, kama Commissioners mungepata nafasi, na mwende "in cognito", utakuta, all the way, hata pale Bamburi ni …………………… (inaudible). Ni kitu kinasikitisha, vile tunaona wanaona wakichukua pesa, conductor utaona ametoa mkono anaangusha pesa, matatu imeondoka, na hali tunaona vile namba za wale polisi.

Kama tungepewa uwezo, kuwe na office neutral, tunaweza kwenda ku-report, na yule officer achukuliwe hatua.

Wakati mwingine pia, utakuta kama ni Politician, yule mkubwa pengine amefirisika, anatuma ma-police wake huku mtaani, kushika watu na munapelekwa kama ni Nyari. Na anajua, ikipelekwa idadi ya watu kama mia moja, kuna rate ile ameweka pale. Maana unajua, pengine wewe ni mfanyi kazi, na ukipelekwa kortini, nayo kazi kule utapoteza. Sasa imewekwa idadi pale. Maybe it ranges from Kshs.500/-to Kshs.2,000/-. Hiyo watu wanatoa, na unakuta wale watu wote, almost three-quarters, ya wale watu wametoka. Hapo ningependa kusisitisha, utakuta kuna kitu kinaitwa "drunk and disorderly". Unakuta saa hiyo, pengine wewe hata unywi pombe, na umeshikwa, umepelekwa Nyari, kama you don't buy your freedom, utapelekwa kortini. Ukipelekwa kortini, yule Magistrate, hata haulizii yule police report ya daktari kuonyesha ulishikwa ukiwa mlevi, na sheria, mimi nafikiri inasema, ni lazima a-prove ulikuwa mlevi. Mara kuna watu wengine hawanywi pombe, na umeshikwa, lakini sasa, ukienda kule kortini, unajua ukikataa tu, maanake unaulizwa tu, "is it true or false?". Ukisema ni false, unakuwa remanded immediately. Na sasa kule lazima waajiri wetu pia ni …………… (inaudible) huku, hata ukienda kumweleza ni nini, hasikii. Kazi yako ushapoteza.

Katika labour laws (Bwana Chairman kidogo tu, niko karibu kumaliza) zetu, ningetaka pia ifafanuliwe. Labour laws zetu ziko kwa kitabu lakini hazitekelezi. Unakuta umefutwa kazi, kesi inapochukuliwa na union, imeenda industrial court, inachukua hata miaka mitatu upate justice. Huku nako, familia yako inatezeka, na ujui hiyo kesi itakuwa ruled namna gani. Ningependelea kesi iwe ruled as fast as possible.

Pia, kuna kitu tunataka kujua. Tunataka kujua kama Kenya hii sheria zetu ziko, na kitu kinaitwa legal strike, ama kama hakuna, iweko. Kwa sababu wafanyi kazi wananyanyazwa na hata munachukua ile tender inatakikana, lakini Minister in-charge anasema, it is an illegal strike, na munavutwa nyote.

**Com. Pr. Ayonga:** Thank you, thank you, thank you. Saa imekwenda na ni lazima nifunge saa sita-na-nusu, na nina majina mengi ya ajabu hapa. Kwa hivyo kila mmoja wenu akisema angalau mimi moja, ni lazima nikate huyo. Hivyo tu ndivyo itakavyokuwa. Mzee!

**Ali Asaa:** Naam.

**Com. Pr. Ayonga:** Unafikiri utaongea dakika ngapi?

**Ali Asaa:** Zile utakazo ni ruhusu wewe, lakini ningependa…..

**Com. Pr. Ayonga:** Lakini unapoona wengi, wewe unaona aje? Wewe ni mzee mwenzangu.

**Ali Asaa:** Ni mzee mwenzangu kweli, lakini, nipe kidogo leo, maanake siku ile tuli…..

**Com. Pr. Ayonga:** Leo?

**Ali Asaa:** Siku ile tuliwachana kati kati. Kama wataka kuniweka mwisho, pia ni sawa.

**Com. Pr. Ayonga:** Tafadhali, ni mimi ninaongea naye. Mzee!

**Ali Asaa:** Ndio.

**Com. Pr. Ayonga:** Tafadhali ……………………. (inaudible) tafadhali.

**Ali Asaa:** Asante sana. Asante. Kwanza, napiga shkurani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa wafsi kama huu, kuja kuhudhuria kikao kama hichi. "…………….. (inaudible)", sisi Waislamu kabla ya kuanza jambo lolote, Mwenyezi Mungu ametuamulisha tumutangulishe yeye. Mawazo yangu na maoni yangu ni haya:-

Jina langu kwa kikamilivu ni Ali Taabu Asaa.

Ninalopendelea mimi kwanza, linalouma watu wa Kisauni pamoja na mimi mwenyewe, na Waislamu wote, na wakaaji, hata Wakristo – ndugu zote, ni squatters wa Coast, hasa hii Mombasa, Kisauni, umeishi muda mrefu sana. Kwa hivyo, tungependelea, na kuiomba Serikali yetu tukufu, iondoe kabisa, marufuku kabisa, hapa mwaka ujao, tukute sisi si ma-squatters tena.

Jambo la pili, tungependelea, Rais akiwa ni Mkristo, makamu wake awe ni Muislamu ……………….. (inaudible). Na mvumu wa Serikali hiyo yote tunayozungumzia, iwe ni ya Majimbo.

Na tungependa Waislamu wenyewe, wawajiwe mambo yao wajiamulie kulingana na …………………………. (inaudible).

Na Kadhi wetu apewe mamlaka sawa na ma-Judge wale walioko kortini, maanake wote wako katika nyuma ya Serikali. Chief Kadhi apewe gari, apewe na driver, na wale ma-Kadhi wadogo pia kadhalika, wafanyiwe usawa na wale ma-Judge

wengine. Hapo tutajitambua kwamba sisi, hatubaguani.

Na pili, kuna ubaguzi mmoja wa siku kuu moja ambayo kwamba Waislamu hatukupatiwa hiyo pamoja na ndugu zetu Wakristo. Tungependa tukipatiwa, tupatiwe zote, isipaguliwe hiyo ni Waislamu pekee yao, ndugu zetu Wakristo wawe wanatumezea mate. Hatuwezi kula pale, na ndugu zetu Wakristo wanatuangalia hivi. Korani haikuamulisha hivo, kula wewe, na jirani yako mpe kidogo naye ale.

Siku kuu tukufu ambayo ni "Idd-Ul-Hajj", wale Waislamu wanapokwenda kuleMecca. Tungependa pia iwe ni public holiday, kama ile "Idd-Ul-Fitr".

Na kadhalika, sisi hapa ni wazima, lakini kuna wenzetu wako ma-hospitalini, ni wagonjwa. Watembelewe pia, wasikia na Commissioners. Wakawaulize maoni yao ni nini? Wangechangia, kwa sababu hao ni wagonjwa, si kupenda kwao.

Pili, ni ndugu zetu ambao kwamba walifanya ualivu, Serikali yetu ikawatia mbaroni na kuwaweka kwenye discipline ya kuwafunga magerezani, wapatiwe pia muda na wao wakutoa maoni.

Kwa hayo machache ndugu yangu, ningependa kuzungumza barua hii ndefu, lakini Mzee tutaonana.

**Com. Pr. Ayonga:** Asante. Hebu utupatie hayo maandishi yako. Na ningependa kumpa nafasi Jacob Ochola Okwiri. Mbona usikae hapo mzee. ……………… (inaudible), kuongea ukiwa hapo. Sema majina yako.

**Jacob Ochola Okwiri:** Jina langu ni Jacob Ochola Okwiri – miaka sitini-na-tano.

Maoni yangu, ambayo imeleta mimi hapa, nasikia watu wanapendelea ati Waziri Mkuu. Mimi sikupendelea Waziri Mkuu awe nchi yetu hii. Kwa sababu, nchi ingine kama saba, zilikuwa na ma-Waziri Mkuu, zilimwaga damu. Kwa hivyo, Katiba yetu hii, ituwezeshe kuwa na Rais moja, ambaye ana uwezo, na serikali moja, na jeshi moja. Kwa hivyo, nilipendelea tusiwe na Waziri Mkuu.

Na tuwe na Makamu ambaye ni mume.

**Com. Pr. Yonga:** Tafadhali tuwe kimya ili tumuzikize.

**Jacob Ochola:** Napendelea hapa Kenya, ikiwa mtu anapendelea atume jina lake, asikwe karibu na Serikali, awe ni Mkenya harisi. Ikiwa hata ni Mpwani, lakini awe Mpwani Mkenya.

Ikiwa kazi yeyote inatokea kupeleka hata mtu wa Kenya nje, awe ni Mpwani-Mkenya harisi. Ndio tunaona, Mabalozi wetu ambao wanatoka hapa, wanatoka wageni tena, ndio wanaenda nchi za kigeni.

Tukipata kwa wenye kuenda Tanzania – kwa Bunge, wanapeleka mgeni, na watu wa Kenya wanakaa hapa. Hiyo nilionelea, ikiwa mtu kama huyo anapenda kazi kama hiyo, hata akienda kwa councillor, hata akienda kwa Mbunge, awe mtu wa Kenya harisi. Na familia yake yote iwe ya Kenya.

**Com. Pr. Ayonga:** Asante sana Mzee Okwiri. Huyo ni Okwiri. Sasa nataka mama Asha Athumani Juma. Asha Athumani Juma? Tafadhali tupunguze sauti, ili mama Asha Athumai Juma aanze. Mama unaweza kuanza, nimekupa dakika tatu tu. Wakati mama anapojitayarisha, nataka ……. Mama endelea.

**Asha Athumani Juma:** Jina langu ni Asha Athumani Juma. Mimi Asha Athumani Juma, kilio changu ambacho nikachokitoa hivi leo, ni sisi Waislamu. Waislamu sisi, tunasema, wananchi wa hapa, tunataka tupate Jimbo letu. Na hili Jimbo letu nalo, tukishalipata, maanake, Jimbo ndio msingi tutakayofanya mambo yetu, au tuseme maneno yetu, ambayo yatajulikana.

Jimbo hili tulilonalo hapa, maneno yote yashazungumzwa, yale nilikuwa mimi nataka kuzungumza. Lakini sasa, maoni yangu ni hivi. Hili Jimbo wakati tukishalipata hapa, tutakusanya zile pesa zetu zote zilizoweka hapa. Ikiwa ni airport, ikiwa ni kilindini, tukishazipata, robo tatu tutamia wenyewe kwa miradi yetu. Tutapata robo moja tukapeleka makao makuu, kwa sababu ile miradi, kisha tushapata ile Jimbo letu, na zile pesa robo moja tumepeleka kule, hizi robo tatu tutajenga ma-shule yetu, na halafu tukipanga mambo yetu, tutayapeleka makao makuu tupate kuidhinishwa kule. Halafu miradi ile, ndiyo tutakuja kuifanya hapa.

Kuhusu serikali zetu, sisi wanawake wa Kiislamu tuna haki zetu. Na zile haki zetu hatujapatiwa, kina mama Wakiislamu, wakati unapokwenda kujifungua hospitali generali, unazalishwa na wanaume, na haki ya Kiislamu yakataza kabisa. Maanake mwanamke ukizaa, uko hali mbaya, uwezekani kwa kitabu chetu cha dini cha Mwenyezi Mungu, mwanamke kuonekana na waume wengine isipokuwa mumeo. Isipokuwa wataka uonekane na mumeo pekee.

Kuna mwanaume wa Kiislamu, yuko pale, yuadungwa shindano na mwanamke ambaye pia hausikani, kidonda kiko pahali pabaya, yuaoshwa na mwanamke, ambaye hauzikani. Kwa hivyo, twataka sisi Waislamu, wanawake wazalishwe na Waislamu ……………. (inaudible) wao, na Wanaume watipiwe na wanaume………. (inaudible) yao.

Nikiendelea mbele, kuna ma-shule yetu. Ma-shule yale tulionayo, wanawake wa Kiislamu wasichana wavaa nguo fupi, skirt ya kufika hapa. Na Wanaume nao, ni siruari zao fupi. Twataka Waislamu wawe na mavazi siruari zao ndefu, ma-shirt ya mikono mirefu, mwanamke awe na "hijabu". "Hijabu" mwanamke awe nayo, na mwanaume suruari ndefu na kofia ya msikitini. Hapo tutakuwa tushatimia kwa Waislamu.

Halafu sisi, tukipata vitu vile, tutakuwa twenda na sheria ya dini ya Mwenyezi Mungu, tupate vitu vile.

Tukiendelea tena, wasichana wetu wakae bega kwa bega na wanaume …………….. (inaudible) na wanawake ……………… (inaudible), na waume nao …………………. (inaudible) kuoa wanawake wasimokuolewa. Kuna kugurumbana gurumbana ndio wacha mwanamke sasa yuafanya mambo mabaya akitoka pale, maanake, kitabu chetu cha kataa mme na mke wawe wakajongeleana.

Nikiendelea tena, …………………… (inaudible) za wanaume mbali, na sturi zetu ziwe na wanawake nao wamegombana.

Tukifuata tena mambo ya Kiislamu, ma-bar ni mengi sana, dirisha lako hili bar hilo, lo si ile, wasichana wetu hawana mwanamke, yuafika kwenya lodge na mwanamme, mtoto wa Kiislamu yuangalia, akiondoka nitafanya ualibifu. Sasa kwa hivyo sisi Waislamu, twataka tutengeze ma-shule zetu za Kiislamu, twataka tujengewe kila kitu chetu cha Kiislamu, maanake, kitabu chetu cha turuhusu mambo ya Kiislamu.

Nikiangalia tena, ni kama kuhusu, hizi kazi zetu tulizonazo hapa sisi Waislamu – wana wetu …………… (inaudible), Waislamu wana wetu wavuta bhang, Waislamu wana wetu …………….. (inaudible), kwa sababu zile kazi wavulana hawana. Tujitahidi kusoma, kumusomesha lakini kazi hakuna. Na zile kazi, ikiwa ni manisipaa mia moja, tuwe ni sisi wenyewe hapa. Watu kumi, wawe ni wale wageni wetu. Na ikiwa ni pahali popote kwenye kampuni, …………………………………… (inaudible) ikiwa itakuwa ni …….. ………………….. (inaudible) finali hiyo, iwe itafuata mwendo ule, …………………….. (inaudible) wetu, tuseme watoto wote, na wa ndugu zetu wa kiume, wawe wataingia mtambo ule waendelee na kazi, halafu, wakipata kazi zile, roho zitakuwa na imani, kuna …………. (inaudible) utaondoka, kwa sababu mwana yule hana cha kukila, mamake na babake wamekuwa mtu mzima, hana cha kufanya. Tulikuwa tunabahari sisi wa hapa, watu wa Mkoa wa Pwani wote, wale wazee wasiokuwa na kazi wakienda baharini, baharini ku…………. (inaudible), hakuna mwananchi yeyote hawezaye kuenda baharini. Je! Waislamu, tutajisaidia na kitu gani?

**Com. Pr. Ayonga:** Asante, asante mama.

**Asha Athumani Juma:** Hatuna cha kufanya sisi watu wa hapa.

**Com. Pr. Ayonga:** Asante, mama dakika zimepita, na asante kwa maneno yako ya ujasiri wote ambao umesema na tena mazuri kabisa. Sasa nitachukua watu wawili tu ndipo tufunge kwenda kwa "Sala". Kuna Ngaumu Seif. Si jina limeandikwa vigumu, siwezi kulisoma vizuri, lakini kama unajisikia ilo jina linataka fanana na lako…… Seif, kuna Seif ambaye ni Ngwaumu.

**Response:** Alikuwa hapa tu …………….. (inaudible)

**Com. Pr. Ayonga:** Ngoja tafadhali. Ngoja tafadhali. Tunataka kufunga ili watu waende kwa "Sala". Kwa hivyo, ninaposema watu wawili, ni time. Na tafadhali ni mimi ninaye manage time.

**Interjection (audience):** ……….. (inaudible)

**Com. Pr. Ayonga:** Nina uhuru huo.

**Response:** Ameenda.

**Com. Pr. Ayonga:** Ameenda. Na kuna ambaye anaitwa Patrick Makato au Makabo?

**Response:** Makalo.

**Com. Pr. Ayonga:** Ni wewe?

**Patrick Makalo:** Kwa jina naitwa Patrick Makalo. Natoka kwa chama cha walemavu. Nataka kuzungumza kuhusu masirai ya walemavu kuhusu Katiba.

**Com. Pr. Ayonga:** Ndio.

**Patrick Makalo:** Kitu cha kwanza, ningetaka kusema ni kwamba, ningeliomba ma-Commissioners, ile alama ya kubagua watu walemavu, iondolewe kabisa katika jamii. Sisi walemavu ni watu ambao tumewekewa mipaka. Kwa hivyo tungeliwaomba, mipaka kama hiyo muiondoe.

Kitu jengine ni kwamba, tungeliomba Tume hii, tunajua kwamba nchi ya Kenya ni mwana chama mmoja wa ma-taifa, na Katiba mikutano hii, tulipitisha asimio kadhaa ya umoja wa ma-taifa, kuhusiana na watu ambao wamelemaa. Na ikapitishwa asimio za kutosha kuhusiana na maisha ya walemavu. Ningelipendekeza kwamba, mambo kama haya yachukuliwe, na yasingatiwe na ya fuatiliziwe, maanake, yanausiana na mambo ya elimu kwa mtu mlemavu, mawaziliano, yaani, jinsi anaweza kupata usaidizi wa clutches, wheelchairs, na kumusaidia ili aweze kuwa anatembea vizuri.

Katika masimio haya, alizungumzia mambo mengi kuhusu elimu, jinsi Serikali inaweza kuwasilikiza walemavu ili waweze kutengenezewa barabara, waweze kutembea vizuri, na wakati nyumba zinajengwa, zijengwe nyumba ambazo wanaweza …….. badala ya kutumia ngazi, zitumiwe …………. (inaudible) za kuweza kutembea na wheelchairs, na kadhalika. Na katika asimio hizo, yaona kwamba Serikali imetia mkazo kabisa kupata maagizo hayo.

Kitu ingine, tungeliomba uakilishi katika Bunge na kwa Municipal Councils. Walemavu ni watu wametengwa kabisa. Katika Bunge hawako, kama wako, basi, ni wachache, hata wakiongea, hawawezi wakasikizwa. Na kwa upande wa councillors, tena hapa Mombasa hakuna hata mmoja. Kwa hivyo, wanapokuwa wanajadili kuhusu maisha ya watu walemavu, sisi huwa tumetengwa kabisa, na huwa hata hatusikizwi.

Kitu ingine tunataka kuongea ni kuhusu national funds for the disabled. Hii fund imekuwa ni shida sana kwa mlemavu ambaye yuko hapa chini kabisa kuipata. Tungelitaka hii fund, iwe constituted, iwe inaweza kujadiliwa kuanzia chini, sio kuanzia Nairobi peke yake kule juu. Watu wa hapa, hawajui wanaweza kuipata vipi. Na kama itaamuliwa, inaamuliwa tu huko Nairobi.

Tuko na shida nyingi ambazo tumeweza kusisema, lakini hatuwezi, kwa sababu hakuna msaidizi wowote tunaweza kupata kutoka kwa serikali. Tukienda kwa social service, wanasema hawawezi kutusaidia, na tukienda kwa National Fund for the Disabled, iko mbali uko Nairobi. Watu wengine hawawezi kufika huko, kwenda kusikizwa shida zao. Tungeliomba hiyo kitu iregeshwe chini mashi……. (inaudible) kabisa, kwa district level, ili tuweze kuwa tunaweza kufikisha shida zetu.

Mambo mengine ni kuhusu – nina maoni kuhusu nominations. Sisi walemavu, ni watu ambao asirimia yetu ni kidogo, lakini tumo katika jamii. Kwa hivyo, tungeliomba Bunge, ichague watu maalum ambao wanaweza kuwakilisha shida za walemavu. Sio tu Bungeni, hata kwa councils pia. Hizo ndizo shida tuko nazo sana.

**Com. Pr. Ayonga:** Kumalizia.

**Patrick Makalo:** Kumalizia, ni kuhusu security. Upande wa security, hasa tuseme kwa mfano mtu mlemavu akishikwa, akiwekwa ndani kwa hizi seli ziko hapa. Huwa hazina zile vifaa vya kuweza kuhudhumia mlemavu. Kwa mfano, mtu akiwa kwenye uizi ameshikwa, kule ndani ya seli aruhusiwi kuingia na ile wheelchair yake. Ina maanisha kwamba, sasa atakaa pale, atambae, kwa hivyo itakuwa ni hali moja mbaya sana.

Kwa ujumla, hapo ndani ya seli, hakuna ………………. (inaudible) zote ambazo zinaweza ku…………. (inaudible) kabisa. Ni hayo tu, asante.

**Com. Pr. Ayonga:** Asante sana. Ndugu unaweza kuja hapa ujiandikishe, na utupe hayo maandishi yako. Sasa, wewe ni mtu wa Ijumaa, sio? Si wewe, naongea na wewe?

**Hassan Mboga:** Jina langu naitwa Hassan Mboga, mkaaji wa Kisauni – Magoboni.

Swala la leo ni Majimbo: sisi tukiwa hapa kama watu wa Pwani, na wazaliwa wa Pwani, uhuru ulipatikana mwaka wa sitini na tatu, na watu wote wa Kenya walipata uhuru, lakini wa Pwani hawakupata. Maneno ambayo kwamba wa Pwani hawajapata

mpaka sasa, na wanatendewa ni kama kudhulumiwa. Kwa sababu, ikiwa sisi watu wa Pwani, ndio maana tunataka Majimbo, ni kwamba, utajiri wote wa Kenya, watoka Pwani hapa – kodi. Lakini utakuta kodi hii, Wapwani wenyewe hawapati hata kitu kimoja. Kwa hivyo, ndio maana tunasema Wapwani tupate Majimbo. Na tukipata Majimbo, hii Pwani yetu, sisi wenyewe hii kodi tunaweza kutekeleza maneno yetu.

Hii kodi yetu sisi tunaweza kujengea university, tunaweza kutengezea miradi yetu ya hapa Pwani. Ndio maana tunasema kwamba watu wa Pwani tupewe majimbo, na sisi nasi tupate kuinuka kama wengi wetu.

Tukitaka Majimbo, utalii wote, hoteli zote za utalii ziko Pwani, bahari iko Pwani. Tukitaka Majimbo, tuna maana yake. Utalii College, iko Nairobi. Anayesimamia Utalii College ni 'Njoroge', na utalii uko Pwani kwetu hapa. Sisi tunapata nini? Kila hoteli kila mwezi, kila hoteli, inalipa elfu ishirini na tano kulipia utalii, pesa zile zapelekwa huko Rift Valley zikienda zikijenga uwanja wa ndege. Sisi hapa hatupati chochote.

Tukizungumza, tunazungumza neno hilo kulingana na kwamba, sisi Wapwani hapa hatupati lolote katika ule utalii wetu hapa. Kwa hivyo, ndio maana unasikia kwamba, watu wa Pwani, wanataka Majimbo. Tukitaka Majimbo, tunataka maana yake.

Ule Rais wetu alipata uhuru kama Wakenya, na wanafaidika. Lakini sisi hapa hatupati. Hakuwezi kuondoka Katana hapa au Salim akaenda akapigania hapo councillor kule. Ikiwa munataka Katiba igeuke, kwanzia sasa, kila Mkenya akiwa amesema kwamba Katiba igeuke iwe ya Kenya, na kila mtu awe Mkenya, kila mtu apiganie kiti katika eneo alilotoka babu yake. Katiba igeuke Bwana Chairman. Kila Mkenya apiganie u-councillor, u-Bunge, katika eneo lake alilotoka babu yake. Katiba imegeuka ya Kenya. Tupate faida na sisi, nasi ya uhuru ni nini?

Lakini ikiwa haiwezi kugeuka hivyo, tutasimama hapa na akina Odongo, sisi bwana hatutakubaliana. Tupeni Majimbo, katika ya sasa. Na sisi nasi tupate kufaidika.

Nataka Katiba igeuke, Utalii College igeuzwe. Tuletewe hapa na sisi. Katiba imegeuka. Twataka Katiba igeuke, Bwana Commissioner, tafadhali, nisamehe lakini, usiseme naingilia sana mambo ya ndani.

Ile head office ya Port, itoke Nairobi, irudi Mombasa. Bwana Chairman nisamehe lakini.

**Com. Pr. Ayonga:** Endelea.

**Hassan Mboga:** Tuna mambo mengi ambayo kama sisi hapa, tunayo -- tuna uchungu. Tukiangalia hivi, pilot anaondoa meli hapa Port, ni 'Kamau'. ……………. (inaudible) anaelewa aje mambo ya bahari? Anaelewaje mambo ya bahari? Na sisi wenyewe tuko hapa. Kwa nini hatuna uwezo ule? Twaambiwa sisi hatuna elimu. Kunao ma-professor. Inaweza enda yale

mambo ya kwamba, ukabila hauwezi kuisha. Kama munataka ukabila uishe, mutuambie Katiba hii igeuke, kila mtu apiganie mahali kwake.

Elimu – tukiingia upande wa elimu: sisi tuna taabu sana Bwana. Watu wa Pwani hatujapata uhuru. Bado tunaumia. Elimu tunapata lakini hatupati kama kawaida. Wakati wa university, watu wanapelekwa wanaenda kusoma university bure, tulikuwa sisi hatupewi nafasi hii. Lakini sasa watu wanalipa mpaka university, ndio unaweza kukuta watu wa Pwani ambao wana nafasi sita, tano. Kwa hivyo, hatujapata uhuru. Kama university tunapata hapa ………….. (inaudible) hau Shimo la Tewa, hau tukajengewa hapa ………. (inaudible), ingekuwa tu sasa watu wetu washasoma university. Ilo ukiuliza, waambia sisi watu wa Pwani tumezoea kukaa chini za miembe. Ndio msemo ulioko………….. huo ndio wananyanyazwa, na ndio sisi tunazungumza.

Si maoni ya Hassan Mboga peke yake, ni maoni ya wengi. Hivi usiwaone hawa waliokaa hapa, wamekaa hapa, lakini wakitoka kule nje, wanamsemo huo huo. Hapa wataogopa kusema kwa sababu, mtu akozoea. Hasa wanawake wetu wa Kiislamu, munawadhudumu kuwaweka mbele ya watu wengi namna hii kuzungumza.

Katika hii Tume, ungekuwa umeweka mahali pa wanawake kuenda kutoa maoni yao, kabla ya mbele ya waume hawa.

Kwa hivyo Bwana Commissioner, ningezumza sana, lakini umesema time yangu imeisha. Na mimi naweza kukupa ruhusa kwamba uendelee na wakati wako. Lakini, maoni yangu, mutupe Majimbo. Naye ikiwa utatupa Majimbo, kila mtu apiganie kwao. Musituwekee hapa kina 'Njoroge', akina nani, kutusumbua.

**Com. Pr. Ayonga:** Asante sana. Nataka ujue kwamba yote uliosema, kanda imeyashika yote kabisa. Na hebu nikwambie kitu kimoja, cha kukusahisha kidogo. Shule ya Utalii College, kiongozi wa kule sio Njoroge, kiongozi wa huko anaitwa Mwakio. Hiyo, la! hiyo tu ni habari ya kusemezana.

**Hassan Mboga:** Haya nakubali. Nakubali.

**Com. Pr. Ayonga:** Na Mwakio huyo unajua ni shemeji yangu, kutoka hapa Pwani. Asante. Sasa ndugu zangu na dada zangu, ni saa sita unusu, ambavyo ni saa sita unusu, na kokote ambako tumekuwemo, saa sita unusu ikifika, tunafunga mikutano, tunawauliza watu waende msikiti, waende wakaomba Mungu, na halafu tunarudi saa nane. Kwa hivyo, muende na tukutane saa nane. Asante sana.

**AFTERNOON**

**Com. Wambua:** Tutaendelea kuyapokea maoni. Kwa hivyo tuendelee na majina kama yalivyo katika horodha. Tulikuwa

tumefikia wa mwisho katika horodha, alikuwa ni Ali Taabu Asaa, ambaye alizungumza. Kwa hivyo, tungependa kumuita Yusuf Hassan kama yuko. Yuko? Sasa mzee, watu ni wengi, kwa hivyo, dakika zako zitakuwa ni tatu tu, uzungumze kwa haraka haraka.

**Yusuf Hassan:** Jina langu ni Yusuf Hassan. Nimetoka katika mtaa wa Mishogoroni, ambaye ninawakilisha kama chairman wa pale. Na ufungu wangu mkubwa ni juu ya ardi. Naona swala la ardhi, Katiba haiwezi kuingia bila ardhi. Ardhi ndio swala kubwa katika Kenya yetu hii. Tunataka wafikirie sana mambo ya ardhi, maanake tumepata taabu kuangaishwa na wageni, ambao hatujui walitoka wapi. Ikiwa mimi ni mwananchi wa hapa, na muzaliwa wa hapa, sina ardhi, mtu ametoka sijui dunia ya wapi, yeye ana ardhi, na sisi watu wa hapa hatuna ardhi. Ndio maana swala la Majimbo ni lazima liweko. Maana sisi wenyeji wa hapa, tunadharauliwa sana. Tunaambiwa tungojee maembe. Hii mambo, swala la kuwa sisi watu wa hapa tumezaliwa, na bado tunaangaishwa na wageni. Hii Katiba iangalie sana kwa line la u-squatter. Sisi sio wale wanyama wanaoitwa "chura", maanake, they have no places – hawana makao. Sisi ni watu ambao tumezaliwa hapa, mufikirie sana swala la ardhi. Hatutaki ardhi irudishwe kwa watu wetu wote hapa nchini. Tunataka sisi wenyeji wa hapa, ardhi zetu zitolewe katika mikono ya wageni. Zirudishwe kwetu wenyewe.

La pili ni elimu kwa watoto wadogo: naona wakati nilipokuwa mdogo, nilisoma kuanzia shule ya pakitani, mpaka tukaenda shule la hewa. Tulikuwa tunasoma vizuri sana, na pesa zilikuwa, sio kama hizi siku hizi ukimpeleka mtoto, taabu sana. Watoto wanaranda randa, hawana elimu. Hawasomeshwi. Hakuna nursery, hakuna namna ya kuwasomesha watoto. Kwa hivyo, tunataka watoto wasome bure, na warudishiwe maziwa yao kama tulivyokuwa tukinywa, sisi wazee.

Swala la chakula: chakula kiangaliwe, maanake, chakula siku hizi zimepandishwa bei. Hata masikini hawawezi kujimudu. Tunataka swala la chakula liangaliwe. Food control, maanake, tunaona katika board ya upande wa chakula, ina taabu sana. Mara huyu anapandisha kile, na huyu anapandisha vingine. Hili swala la chakula liangaliwe. Lakini sio kupandisha "kiolela". Iangaliwe katika sherika ya Katiba. Vyakula vyangaliwe vizuri Bwana Commissioner.

Swala la upande wa prisons – jela: tumeona haki …………………………. (inaudible), wanateswa sana. Hawana ………. na vyakula vimewekwa kama ……………………… (inaudible) tumepewa uhuru, na ni lazima tuhutumie uhuru wetu. Watu ambao wamewekwa kule, sio wanyama, ni wanadamau. Na hili swala la wa-prison, ni lazima liangaikiwe na lishugulikiwe, maanake, tuko katika Kenya uhuru. NI lazima wale walio fungwa – wafungwa waangaliwe vizuri afya yao. Sio kuchukua wafungwa, na mara tunasikia wafungwa wengine wananyongwa. Kwa njia gani? Hau kuna kinyume gani? Kuna njama gani ya watu wanapelekwa, na huku tunasikia watu wameuwawa katika ma-jela. Twataka kujua kwa nini wanauliwa namna hii. Hili ndilo swala ambalo linasikitiza sana. Vyakula pia hawapewi, vyakula ki-sawa sawa. Hata wengine wanakuwa ni swala lingine, ambalo lina aibu pia. Mtu apati chakula mpaka anajitoa yeye mwenyewe kuwa kama………. hivyo ndivyo ni aibu. Tunataka tuangalie upande wa chakula katika prisons – yaani jela. Jela iangaliwe kwa ……….. (inaudible) kwa wafungwa. Waangalie sana mambo ya jela.

Swala la mwisho, ambalo ninaenda mbio mbio kwa sababu munasema tuende haraka. Police watumie midhamu. Sio kushika shika watu ovyo. Sisi ni Wakenya bwana. Sisi sio wageni. Huwa ooh, unatembea, unaambiwa simama. Toa kitambulisho. Mimi ni Mkenya, kitambulisho, mimi sio mgeni. Nikiwa nimemwambia nimesahau kitambulisho changu, mwingine yuko mbele yangu, ni mweupe anamwaambia yule, wewe kwenda. Wewe kuja hapa. Sasa hili swala hili ni swala geni sana. Sisi Wananchi, tunaweza kusimamishwa kama mnyama wa mwitu. Kwa njia gani? Na tena anasema, toa kitu kidogo. Hii mambo ya "toa kitu kidoto", bwana, tunataka isaahuliwe kabisa.

**Com. Wambua:** Mzee Hassan!

**Yusuf Hassan:** Naam.

**Com. Wambua:** Tumeyasikia yote, yameingia kwa tape.

**Yusuf Hassan:** Lakini Majimbo ni lazima.

Hayo tumesikia pia, na yameingia kwa tape. Kwa hivyo, asante sana. Tumuite Kalume Mumba. Haraka haraka Kalume. Dakika ni mbili tu. Watu ni wengi hapa. Endelea Mzee.

**Kalume Mumba:** Asante sana Waheshimiwa, kwa kunipatia uwezo, hata sasa niko hapa, kwa mambo yangu, na sisi tunaendelea.

**Com. Wambua:** Endelea tu, endelea.

**Kalume Mumba:** Jela ziwe na madirisha makubwa. Jina langu naitwa Kalume Mumba Thome kutoka Mutopanga Primary School.

Number one, nataka jela za hapa Pwani ziwe na madirisha makubwa.

Kitambulisho cha Pwani kiwe tofauti na cha bara.

Tume ya Kurekebisha Katiba iwe na uwezo wa kupanga jeshi lote, misaada ya pesa, na mahindi mengi, tupewe hapa Pwani.

Rais asiwe na uwezo wa kutangaza vita.

DO, DC, ma-chief, waondolewe. Ofisi zote za hapa Pwani zirudi.

Hapa Pwani pawe na chuo na kikuu.

Hapa Pwani pawe na Bunge.

Mtu akishikwa, kukija siku ya pili, apelekwe kortini.

Tume ya Katiba, isimamie uchaguzi ujao.

Kuwekue Sheria ya kuhakikisha kujali viwete.
Hukumu ya kunyonga iondolewe hapa Pwani.

Watu wa Pwani waandikue kazi – themanini na tano percent.

Mivereji iwe free. Isiwe na meter.

(xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx (From here transcribed by TINA ODHIAMBO)

Watoto wasome mpaka darasa la nane bure.

Serikali isiwe na uwezo wa kutoa pahali. Lazima anayepata kuwa na uwezo wa kumiliki pahali, ni jamaa wa hapo.

Rais atakaechaguliwe aapishwe na Tume.

Mabadiliko ya wapigaji kura, yawe kuanzia miaka kumi na miwili.

Anayepasa kua na mamlaka ya nchi, ni Tume ya Katiba.

**Com. Wambua:** Tumupatie muda tafadhali atoe maoni yake. Endelea Mzee.

**Kalume Mumba**: Pombe ya kienyeji jiwe free popote zipikwe.

Sheria ya utoaji permit za matanga iondolewe.

Tajiri na masikini wakikosana wakaenda kesi, kusiwe na upendeleo.

Kue na wakubua wa ma judge hapa pwani.

Watoto wa hapa wapewe maharagwe ya bure mashuleni, wapikiwe pale na wale hapo, hapo.

Sheria ya undanganyifu kwa raia wa pwani iondolewe.

**Com. Wambua**: Mzee malizia tafadhali.

**Mzee. Kalume Mumba**: Asanteni sana ndugu. Hayo ndio ya mwisho. Kwa sasa time za enda.

**Com. Wambua**; Asante. Swali mmoja tu. Nani atakae wapatia watu hiyo pombe bure? unapendekeza nini wewe?

**Mzee Kalume Mumba**: Serikali iruhusu watu wawe wana kunyua tembo ya bure sababu tembo kikwetu sisi hapa, ni ya kizee. Pahali panapo olewa mtu, lazima tupawe na ile tembo ile na hata pahali matangani, tupawe ili tembo ile, sasa ile ni kinywa cha ambacho ni cha kizee, kinatakikana kiwekue free.

**Com. Wambua**: Asante sana. Hii ni kusema kusiwe na kushikua na kutokulipa.

**Mzee Kalume Mumba**: Kushikwa na askari ama ku -------

**Com. Wambua**: Asante sana. Jiandikishe pande hio. Kuna Hussein? Hussein ama Hassan? Hassan? Tafadhalini, tafadhali tutulie ndio tusikize wenzetu. Kuna Hassan? Hassan? Kuna Maua Jini ama Maua. Haya mama kuja hapa. Maua.

**Maua Jini**: Jini yangu ni Maua Jini na ninakaa Kongowea. Mimi maoni yangu ni hivo ma plot hizo tunapangisha ni ya shida sana maana yake kukichelewa na hizo pesa wanaanza kuja kuuzia hiyo nyumba. Ndio maoni yangu. Na kisha maoni yangu ingine tena, kuna Mwarabu alijenga nyuma ya nyumba yangu na ananifungia maji. Sasa vile ananifungia yale maji, yani mvua kubua ikiija inaweza kuangusha na nyumba yake ni ya gorafa. Kila nikimuambia nilikwenda Municipal kwenda kuseme yale maneno, nafikiri alipeana kitu kidogo. Na mimi sina chochote. Sasa nyumba ile ikianguka nitailisha naye nini na watoto wangu jamani? Ndio yayo tu nilie nayo. Sina mengi.

**Com. Wambua**: Asante sana mama. Jiandikishe huko. Tumeasikia yote hayo. Nitamuita David Chaka. David Chaka. Yuko? Haya Kuna Johnson Katana? Johnson Katana? Patrick Makalo? Patrick Makalo. Walter Mbotela? Frederick Kuledi. Okey endelea.

**Frederick Kuledi**: Kwa majina ni Frederick Kuledi mkaaji wa Freetown settlement na tangu asubuhi nimekua hapa nimesikia karibu robo nzima ya watu walikuja hapa. Wame taja taja juu ya majimbo na ninge omba kuyaongezea kutulia nguvu jamo la majimbo. Tukiwa hapa Freetown kama wakaaji wa hapa, nafikiri hata ndani ya Biblia ime taja habari ya majimbo. Mwenyezi Mungu mwenyewe alitaka watu wawe na majimbo yao. Walipo kua wajaribu kuketi pamoja walipo kua njenga mlima Babe wakatawanya na kila mtu akawa na mahali pake kwa hivyo majimbo ni wazi kua itaweko. Na sisi watu wa Freetown, nikusema hapo kwa majimbo yako ni watu ambao tulipate jimbo letu mapema hapo Freetown kulingana na Katiba ya pale ilivyo ya CMS na British Government. Kuna sehemu yetu ambao tumepangiwa pale kuketi pale. Kwa hivyo tungependa kuipigania sana Freetown.

Juu ya hapo, tukiangalie sasa wakatu uhuru ulipo patikana wa Kenya, 1963 mahali hapo ikachukuliwa na Municipal Council ya Mombasa kama Trustees, wadhamini tu, lakini kwa sasa Municipal Council ike tuingilia imechukua mali zetu, imechukua kila kitu chetu, hatuna nafasi pale hata ya kusema. Hatujui tume wekua namna gani. Vile protection tulikua nazo za British Government na CMS si ilioko sasa. Sasa tuko chini ya Municipal ambao haituangalii kwa vyo vyote. Hali imekua ni ngumu tunatozua kodi za juu ambazo pia ni za matatizo kuzilipa. Ningeomba katika Katiba hii mpya kama settlement zote ambazo ziko katika Kenya, Freetown ambao ni settlement ya kwanza katika East Africa ifikiriwe pia kua ni settlement kama kawaida na tuangaliwe kama kawaida ya watu wengine.

Katika kifungu chenu katika hizi kitabu hili nilicho nacho, Constitutional Review, ukurasa ya kumi na nane na kumi na tisia, hapo juu imetajia habari ya communities ambao sisi ni kama community hapa Freetown. Katika Clause number kifungo cha tisa imetajia habari ya (-------) ambae sisi tuna (-------) yetu ambae iko kwa maandishi hio pia tunapigania iangaliwe.

Tukija page 19 kuangalia haki za watu, mali yao, properties zao, pia iko hapa ambao sisi tunataka haki zetu zirudishiwe kutoka kwa Municipal turudishiwe wenyewe ambao tuko na (-----) yaku angalia mambo hayo sawa sawa.

Ningependa kutangulia kwanza, kwanza watu wa Freetown ambae watu wote wanajua historia ya Freetown kua pale ni wale watu ambao watoka nchi za mbali, kama Malawi, Zambia, Zimbabwe na Tanzania ndio waliwekua hapa Freetown. Na wakati mwingine wa kuchukua vitambulisho tunasumbuliwa sana, tukienda kuuliza habari ya vitambulisho, unaambiwa wewe nenda kwenu Zanzibar, nenda Tanzania, nenda hivi na hivi. Hali ya kua sisi ambao tuajulikana na historia yetu inajulikana kirefu.

**Com. Wambua**: Mzee malizia tafadhali.

**Frederick Kuledi**: Kwa hivyo tunataka Serikali ituchukulie kama raia wa Kenya na tena ituangalie kama settlement schemes zingine za Kenya. Hayo tu yangu, asante.

**Com. Wambua**: Asante sane mzee, kwa hivyo tunamuita hapo mama Zainabu Said. Yuko? Najua ameketi hapo tangu

asubuhi. Kuja hapa usungumuze.

**Zainab Said**: Asalamualekum.

**Audience**: Aleikumsalam.

**Zainab Said**: Mimi ninajulikana kama Zainab Said nimkaaji wa Kongowea lakini Kisauni Division.

Neno la kwanza linalo niuma hapa kwetu ni mambo ya ardhi. Sisi tunalipia ardhi na tunaowalipa sio wa Kenya na isitoshe wengine hawaishi hata hapa Kenya, wako Canada, wengine wako America lakini anaokota pesa kutoka kwa wa Kenya. Sioni sababu tuendelee kuwalipa pesa watu hawa.

Jambo la pili ni kuhusu kina mama. Kina mama tunaambiwa kuna fungu la pesa utengua na Serikali kwa maendeleo ya akina mama na shuhuli zote za akina mama. Lakini tuafanya kusikia kwa majina tu. Hatuzijui pesa hizi wala hatujui azipokeae ni nani wala zitamfaidi nani lakini tuajua budget yetu ikitengua kuna pesa ya akina mama. Shuhuli za maendeleo za akina mama Serikali aijisumbui nayo. Mukitengeze vikundi mtakuja muambiwe fanyeni vikundi, fanyeni nini, fanyeni nini, mtasaidiwa, lakini yale ua ni maoni pengine ni Mbunge ataka kura, pengine ni mkubua ataka sifa, lakini hakuna chochote tunacho fanyiwa. Hasa wale wamama walio chini kiwango cha chini. Na wakubua wanao shikilia vieo kule kwa maendeleo huwa ni wale, wale hawabadilishwi. Ninataka mkubua akishika cheo akae muda flani aondoke ashike mwingine. Sasa tutamjua kama alikua na makosa ama alikua ni mtu mzuri.

Tatu, upande wa Kazi: Kina mama tunasumbuliwa kwa njia nyingi sana. Wewe ukiwa ni mrembe basi olewako. Ukienda kuandikiwa kazi, General Manager, iwakutaka Director, iwakutaka wewe Karani, iwakutaka wewe mpaka ofis messenger pia, wakujitetea huna. Ukiwa wewe ni secretary, basi wewe u secretary wako wakalamu na u secretary mwingine juu. Vile boss anavyo taka ndivo utakovyo fanya. Hata ukiwa ni mku wa mtu. Na katika hali yetu tulionao kwa sasa hatuna pesa, hatuna nini pengine hata yule mume hana kazi wewe ndio waangalia kila mtu. Wengine wanalizimika kukubali, ili alishe familia yake. Laki ni njia mmoja ya kunyanyasa kina mama.

Hawa rapists nao, wanawachua free. Mtu yule ati anapewa community services. Hataona msichana mdogo mwingine amrape? Ama hataona mama mwingine amrape? Rapist na mnyongaji wote hali mmoja. Waoze huko huko jela.

La mwisho ni askari wetu. Askari wanatunyanyasa. Si askari pekee, ni wao na watu wajivitambulisho pamoja na watu wa jikaratasi za Passport. Kila mmoja ukimkuta tu tumbo li huko. Hapokei mshahara. Mshahara ni wewe. Ukienda wewe huna pesa, huna Passport na nafikiri Passport ni haki yangu. Birth Certificate, watoto wengine sio kina mama wote wana pesa kwenda kuzalia hospitali. Na saa zingine kuzaa ni kama kifo. Hakuagi. Unaweza kutoka hapa waenda pengine Utange,

unaumua njiani, unamzaa yule mtoto. Kuna Midwife pale ambae ataandika kila kitu. Utakapo kwenda hospitali hakuna anaekusikiza. Ukienda kwa Birth Certicate, hoo, nilizalia nyumbani, ndio balaa kabisa. Sasa watoto kama hawa tuafanyie nini?

Na watoto walemavu, ukienda nae hospitali akiwa bahati mbaya ametiliwa mimba ni wakike, ukisema niacheni nimzungumuzie, hakuna anaekusikiza 'mama kaa nje hii ni labour'. Mimi ni mama, sistahili kufukuzua kutoka kwenya labour. Nataka kumsaidia huyu, lugha yake nailewa mimi. Nyinyi hamuielewi na hamna watu special ambao mume waweka kwa kuhudumia. Sasa mlemavu yule atakua kuambiwa 'sukuma wee, yuaruka'. Kisha wanampiga.

**Com. Wambua**: Mama tumeyasikia hayo yote kwa hivyo asante sana na ujiandikishe pande huu.

**Maua Said**: Na mimi nashukuru.

**Com. Wambua**: Mama jiandikishe hapa tafadhali. Tuna Amina. Amina. Yuko? Rev. Joseph Kashuru? Rev. uko na maandishi umeitengeneza? Basi tutakupa dakika tatu tu tafadhali. Watu ni wengi. Mulika tu yale yalio muhimu na utupe haya maandishi. Tutaenda kuyasoma yote.

**Rev. Joseph Mangaro Kashuru**: Kuma ungenipa tano --- haya. Mimi ni Rev. Joseph Mangaro Kashuru na ninawakilisha Kanisa la Ki Anglicana, Mombasa. Tuliandika mambo haya kwa ki lugha ya kimombo lakini tuko Mombasa, nitaongea tu Kiswahili halafu mwingine atasema Kizungu huko mbele.

Katiba tulionayo haituambii sisi wa Kenya tumetoka wapi. Kwa hivyo hakuna ajuae ni Mkenya kivipi? So, tungependa Katiba iwe na ile inaitua kwa Kizungu Preamble ili ittujulishe sisi wa Kenya tulitokezea wapi, na tulitoka Shungwaya au tulitokea Matondo? Hilo ni la kwanza.

Jambo la pili, tungelipenda Serikali iwe ya Majimbo. Hilo hatuwezi kuli -----(clapping)
Na huyu ambae atakua kiongozi wa kule juu, angalau aweze ku serve kwa terms mbili za miaka mitano, mitano. Akimaliza miaka yake kumi, hata kama ni mzuri sana aachue. Twende kwa jimbo lingine nalo lionje hio cake kubua.

Tungelipenda tuwe na Regional Assemblies ambao ziko chini ya ma Governor ambao watakua wakifanya kazi na dhani mna elewa nyinyi Serikali ya Majimbo inakaa je kuliko sisi. Kwa hivyo ninadhani mnaelewa ninasema nini? Huyu kiongozi kwanza awe mwananchi, huyo President.

Pili, kama ni kusoma, angalawo awe amefika Unversity na kiuwezi au kifedha awe ni, anaitua kwa Kizungu Economically stable asije apewe u President halafu akaanza kuinufakia pekee yake halafu, mengine akaharibika.

Na umri, awe na miaka arubaini na mitano mpaka sitini na mitano. Aki zidi hapo mara ingine akili zitarudi chini. Ijabo wale wazee walioko wasinielewe vibaya.

Kwa hivyo nina mengine mengi. Tukiija kwa swala ya ardhi, tungeipendekeza kwamba tunasikia, hatuja jua vizuri kwamba mwananchi anapo pewa ardhi, zake ni futi tano kwenda chini. Huko chini ya futi tano si kwake. Swala ni kwa nani? Tungelipenda nikipewa kipande cha ardhi hata kama ni futi elefu saba chini, kuwe ni kwangu. Kama kuna madini, yawe ni yangu, si ya Serikali. Swaha hilo tukikosa kuna fujo kule Kwale kwa sababu madini yako kule chini hayako futi nne. Report za Satenium inaleta shida kule chini.

Kwa mambo ya uhuru, uandishi, tungelipenda uandishi wapewe uhuru, lakini yale wanaandika wengine yaleta shida. Sipende kuona picha ya msichana akiwa nusu uchi, na ni gazeti ile. Jameni majimbo tuyapenda lakini haya nao tuiangalie. Angalao tuwe na mulekeo mzuri. Ningeungana na wale wengine wanataka mavazi yawe mazuri kwa sababu ukivaa nusu uchi unavyo sivyo mno, kwa hivyo jameni nina mengine mengi, lakini karatasi iko ilio andikua Kizungu. Asante.

**Com. Wambua**: Asante sana Rev. kwa hivyo jiandikishe huko na utupatie hio memorandum, tutaisoma. Kwa hivyo tutamuita Juma Kumala. Yuko? Ako wapi? Athumani. Haya kuja hapa Mzee Athumani. Tunakupa dakika mbili umalizie, unalizie mzee yale ya muhimu.

**Athumani Mbwana Kumala**: Jina langu ni Athumani Mbwana Kumala. Mimi sina zaidi ya maneno. Yatakuja mzemaji lakini mimi nitasema kama maili tu.

Jambo la kwanza naiomba, Tume hii itukatie mpaka baina ya Fiji mpaka huko Kisauni. Upande ule uwe Mombasa. Na kwa sababu? Maanake huku kwetu waliletua kule Mombasa hawaoni kuwa sisi ni viongozi wala sisi tuataka kuongoza. Hawajui. Wajua huku ni mashamba, hakuna watu. Lakini ilikua ni mashamba zamani lakini sasa mashamba ina watu. Kwa hivyo ukatua mpaka uwe huku pekee yake. Ikiwa ni Mbunge, awe wa huku, Councillor awe wa huku, hata kama atawakilisha Mombasa, lakini awe amechanguliwe sehemu ya Kisauni.

Na huku Kisauni kuna matatizo mengi ya ardhi kwa sababu wenye ardhi wote wako Mombasa. Sasa huona sisi huku ni kama Manyani tu. Wakiija, waja kututembelea, washika njia waende zao. Lakini sasa tuataka funga mpaka wawe hawaji tena huku. Sisi wenyewe tuchukue ardhi zetu, tujitawale wenyewe.

Jambo la pili kwa kusemea hivo kuwa mpaka ukatue wale wa kule hawajui kama huko Kisauni kuna Waislamu, wafrica hawajui. Waona kule hakuna Muislamu hata mmoja. Na kosa hili inatokana na Serikali pia tukisema. Maanake Serikali aitambui mtu. Muisalim, Mafrica, yeye kila akiangalia aona Mwarabu ndio Muislamu. Hata kame ni myaudi, lakini mweupe ni

Muislamu tu.  Lakini kuna Wafrica Waislamu waki sawa sawa kushinda hawa Waarabu huko juu.  Wana elimu ya dini.  Wajua kusome, lakini hawathaminiwi kwa sababu mpaka ufanyua mmoja.  Lakini tuaomba ukatwe.  Na sisi tuwe nasi tuna sauti ya kutosha sehemu ya Kisauni.  Ya tosha hayo.

**Com. Wambua**:  Mzee, asante sana.  Jiandikishe huko.  Tumuite Mambogo W.T.  Yuko?
Mambogo W.T.  Haya.  Tumuite Hamed, kuna Ahamed.  Muhammed?  Stephen Musyoka? Musyoka, nataka kukupa dakila mbili tafadhali, uko na memorandum?

**Stephen Musyoka**:  Naomba tatu tafadhali.

**Com. Wambua**: Ni mbili tu.  Watu hapa ni wengi. Ninataka kumpa kila mtu nafasi.

**Stephen Musyoka**: Asante.  My names are Stephen Mulei Musyoka.  I am sorry kwa kuwa yangu nimeandika kwa Kiingereza na nitasema kwa Kiingereze maanake itaenda kwa wale nadhani wata

**Com. Wambua**: Endelea, endelea tafadhali.

**Stephen Musyoka**: The Supremacy of the Constitution:  The Constitution should be superior to all other lawa.  The basis of the democracy is the rule of law.  So the law should be applied consistently and that all the citizens are equal before the law.

The Constitution should be the reference point for all the other laws and for the action of the State officials.

Enforcing the Constitution:  The Constitution should be accessible to the people. In true democracy people are sovereign so they should be able to understand what their Constitution says and feel that it belong to them.

Our new Constitution should be written in a clear straight forward style that any person can understand not just a lawyer or academicians.  Kenya is a multi-cultural society so we should consider writing our Constitution in every mother tongue that is spoken by the Citizens.

Our new Constitution should be taught in schools deseminated through the media and discussed in citizen meetings throughout the country so that everyone becomes familiar with it.

Citizens should have the right to sue to enforce their Constitution.  Usually a Constitution is made by people who not only live together ---

**Com. Wambua**: Bw. Musyoka, don't read that memorandum, just highlight the main points and give us the memorandum, we are going to read it. You cannot finish reading that memorandum tafadhali.

**Stephen Mushyoka**: Asante. Fundemental Rights and Freedom: Our current Constitution protects only the classic and civil and political rights. The right to life, property, to freedom of assembly, association, movement and (word not clear). We should have first generation rights, freedom of information.

The point is about the Seperation of Powers: There should be separation of powers in the branches of Government.

The last point I refer is: We should have Parliamentary system of Government where we should consider adapting a Parliamentary system of Government. Parliament should have a central law. We should have a Prime Minister, cabinet governed with the support of the majority in Parliament and they shoul be answerable to Parliament for the way they run the country.

**Com. Wambua**: That is your last point. Asante sans Bw. Musyoka. Please record your memorandum there. Let us have Sudi Hussein Pati. Utatumia dakika mbili tu ndio utasema yale unataka kuyasema.

**Sudi Hussein Pati**: Mimi Nitasimama badala ya kukaa.

**Com. Wambua**: Bora tu uchukue dakika mbili. Uko na dakili moja na nusu sasa.

**Azimio Hussein Pati**: Ma bibi na ma bwana, hamjambo?

**Audience**: Hatujambo.

**Azimio Hussein Pati**: Kwa jina naitua Azimio Hussein Pati ama Sudi Maarufu Mapinduzi.

Jambo la kwanza ni kwamba Katiba yetu imtambue Mwenyezi Mungu kitu ambacho hakuna katika Katiba zetu. Katiba imtambue Mwenyezi Mungu. Ijue Mwenyezi Mungu ni nani ndipo pale tutakua na mambo hayo ya uchoyo, unafiki, kuuana, kudhulumiana, kote hakuna.

Jambo ya pili, tuasema tuataka Jimbo, ndio suluhisho ya maatatizo yote katika Mkoa yetu ya Pwani na Kenya yote kwa jumla. Maswala kufichana hakuna. Jimbo litakalo sisi ni kwamba, ma wakili wale mashuhuri wale watolewe hapa wapelekwe Africa Kusini, wapelekwe Canada, wapelekwe Australia, wengi wakasomee ni ma Jimbo sababu gani twaitaka hapa? Jimbo tukilipata, habari ya ardhi kila kitu kitaondoka. Kutakua hakuna matatizo ati vijana wetu wakose kazi, sijui hata upande gani?

Sijui kuna kitu gani? Tumefaamikiana? Zote sisi tuko kwa kodi mmoja, Bwana Wambua Musili, twataka Jimbo, ndio suluhisho ya sisi hapa. Hakuan maswala ya kundanganyana hapa, ati kama ardhi, yote yatakuja baada ya Jimbo kulipata. Kwa hayo machache, asanteni.

**Com. Wambua**: Tumeyasikia hayo. Tumuite Patrick Barawa.

**Patrick Barawa**: Ma Bwana Commissioner, kwa jina mimi naitua Patrick Barawa, nimkaaji wa Kisauni Mlaleo na nina machache tu ya kuweza kuwaeleza kuhusu hio Constitution Review.

Kwangu mimi, maoni yangu ni kwamba, Constitution tulio kua nayo ya kwanza ambao iko currently ni National Constitution na hii National Constitution, kama inavyo onekana ilikua ifaidishe kila mwananchi katika nchi ya Kenya. Lakini kwa sababu flani isizo weza kueleweke kwa wote tulioko chini, tumeshinda kupata fadia hii yote. Si Pwani pekee, bali katika Kenya nzima. Oni langu kuu katika hivi, ninge omba wana Constitution Review Committee members, kupendekeza kwamba hii National Constitution ambao ndio National Government tuliokua tunanaye, hii Katiba haikufadishal kila mwananchi na hasa Pwani. Nikisema hivi nikumaanisha hivi, ardhi ilioko Pwani au baada ya uhuru, ardhi kuko bara ilikombolewa halafu wakapewa wananchi wa kule bara. Pwani wetu hawakuweza kukumbolewa ikapewa mpwani. Hili ni jambo la kushangaza ambalo mpaka sasa utakuta wale waliokuja Pwani hii tulio wakiribisha katika Pwani hii, wakina Mazrui, ndio waliopewa mamlaka na vyeti hivi ndio leo hata sisi kuvipata wana pwani halisi ni shida. Ni jambo la kusikitisha. Ili niweze kufafanua, nitawacha hii kitu pale, ela nitaenda kwa step ya pili.

Step yangu ya pili, tunalomba hasa kwa sisi Pwani, ili tuweze kufaidika kama wengineo wote katika Kenya, nikupata utawala wa Majimbo. Majimbo yenyewe tunaamini kwamba yataweza kuondoa ile Centralization power ambao hio imewekua mahali pamoja. Tukisema hivi naweza kupanulia mmoja, mbili. Ni juzi tu, sasa imewezua kurekebishwa, lakini haija rekebishwa sawa, sawa. Sema kwa mfano hivi mtu ametelewa na mkewo, sema kwa mfano wakatu huu sasa, mtu amemaliza kustafu, anataka kupata ile gratuity yake, kitu ichi ya gratuity huyu mtu aitamzidi aende Nairobi ili akaweze kupata gratuity, hii pesa yake. Ni jambo la kusamenesha kwa sababu lina chukua mdu mrefu tukienda Nairobi. Lakini ninge omba Wana Constitution Review Committee ituangalilie jambo hili kwa Serikali ili tuweze kupata kuona mamlaka ya kuweza kuomba rati wetu tunaweza kupata kwa urahisi.

Pendekezo: Ningependa utawala wa majimbo ambao utafanya kuvunja mamlaka au devolution of powers kuipa mamlaka maeneo kamili.

Pili, Serikali ya majimbo itaweza kuondoa the separation of powers kuweka hii mamalaka juu ya wale wananchi katika kila jimbo au kila mkoa. Hasa ninajua mengi yangeweza kuondolea katika mkuu ambao President ingewezwa kuwekua kwa Governor wa Mkoa. Ningependa, wana Constitution Review kwamba, kuwaomba hivi, ili basi maendeleo yaweze kupatikana,

kama ilivyo kuwa imeanza DDC baadaye ikisha imekuja imevunjuz nguvu, hatuelewi ni kwa nini? Hiyo DDC au hayo mamlaka, tukisha pewa sisi wana Pwani, tutaweza kuangalia elimu yetu vile inavyo weza kuendelea, hospitali yetu, mafunzo kama colleges na kadhalika. Leo hivi utaona shida ambazo ziko za waalimu mashule, kwa mfano, mwalimu yuko hapa na hakuna Serikali yoyote duniani, hakuna mkuu yoyote katika dunia ambae apitii mkona wa mwalimu. Lakini utashangaa mtu anaempa elimu President, mkuu yoyote katika nchi, kule ananyanyaswa anapewa shilling elfu tatu. Mbunge anapewa shillingi elfu mia tano na yeye alipata elimu, yaweza kusimamia jambo kama hili kutokona na mwalimu huyu, huyu. Sisemi ati na kashifu Mbuge wangu. Kwanza nampende na ndio nampigia kura wakati customer hii. Na hata akisimama wakati huo, nikiambiwa ni kura, mimi nitampigia customer hii. Lakini ni jambo la kusikitisha kwamba mwalimu anasononeshua.

**Com. Wambua**: Patrick, malizia, malizia na upeane memorandum pande hio.

**Patrick Barawa**: Thank you, Sir, nashukuru sana Hata ume ni confuse. Let me conclude it. Nikusema hivi. Elimu yetu kwanza ya sasa ambae ni ya mfumo ya 8-4-4(nane, nne, nne) imeleta mzogo kwa watoto ambao wakatu huu wanabeba mikoba mikubua, mikubua na vitabu vingi na hatuoni faida yake. Tuki compare hii hali na ile yetu tuliokuwa nayo wakatu ule wa zamani, kwanza hata ulikua unafanya mtihani unapewa cheti cha performance sio cheti ya kuonyessha kwamba ati umemaliza masomo. Ukipata ku pass wewe, una ambiwa umepata grade A kama tuseme School Certificate, una ambiwa wewe ni Division One, Division Two, Division Three, sasa haijulikani Division One ni nani, Division Two nani, Division Three ni nani? EACE ni nani? Unapata tu mtu ni Certificate of completion of education but not performance. Ndio naomba wana Committee wa Review Commission wamuambie Bwana mkuu wa Serikali ambae anahusikana na mambo haya atusaidia kutuletea ile Serikali tunaoitaka ya Majimbo. Asanteni sana.

**Com. Wambua**: Jiandikishe hapo, Bwana Patrick. Tutamuita Bwana Kadir Muga, Kadir? Tafadhali tunakupa dakika mbili tu na kama uko na memorandum kuzie tu yale ya muhimu halafu injiandikishe hapo tafadhali.

**Kadir Muga**: Asanteni. Kwa majina naitua Kadir Hamisi Munga. Mimi ni mzaliwa wa ziwa wa ngo'mbe.

Mimi nilikua nina machache ya kueleza kulingana na ------- hayo mengine nitayatoa pale.Mimi. Mimi ninaongeza tu yale kwamba Katiba zifundishwe katika zile ----zote na vile vikundi vya maendeleo na mashuleni maksudi sisi wananchi tujue Katiba ya nini. Hivi sasa nikama mnatasumbua tu kutuambia Katiba, Kariba, na kuna wazee wetu wengine hapa hawaijui hiyo kitabu hata hawajaiona kutoka tupate uhuru.

Kitu kingine ni biashara. Katika hizi biashara, kuwe na ratiba ile kama ya zamani ya kikoloni. Kuna karatasi ya kuonesha bei ya bidhaa iko pale, mwananchi anajua vipi ataweza kununua bidhaa hio si kama sasa vile maduka yamepewa uhuru wengine wanauza shilingi mbili, shilingi tatu, shilingi nne, hatujui tunamlekeo wapi wakibiashara. Na wale wanyaji biashara ya kigeni, zile pesa ambazo wanaweka kule nje, zizuhuliwe. Pesa zote waweke Bank ya National Bank, bank yetu ya Kenya kwa muda ya

miaka mitano ili zile faida zote ambazo ziko hapo kwetu wanazozichukua zitufaidishe ndio wao wachukue hizo pesa wazi bank. Maanake kuna ma shirika mengi sans kima hoteli sasa, hawateju pesa hapa. Pesa, tikiti, watu wanakatia huko, huko. Huku ni swimming pool pekee yake ndio zina katua.

Kitu kingine, hii habari ya labour. Labour na vyama vya wafanyagi kazi. Kuna hizi hoteli. Hizi hoteli zina wananyanyasa sana watu kama sisi wengine ambao tumestafu mpaka sasa hatujapata pesa zetu mpaka sasa miaka mitano. Mtu anakaa anangojea pesa, notice yenyewe haja pewa, pesa za miaka alipewa akaambiwa utapata, hajapata. Na ukifika kule, kuna maskari wamewekua kule mlangoni wakuzuia mtu. Ukisema unataja kuingia hapa, unaambiwa huna ruhusa kuingia wewe sasa hata hujulikani tena. Lakini wakati ulipo kuwa unafanya kazi na nguvu zako zote miaka yote, ulikuwa unaweza kuingia hotelini ukafanya kazi na tajiri akafurahika kupata pesa kwa damu yako. Kwa hio mimi ningeomba vyama vya wafanyaji kazi vitiliwe sheria za mkazo na labour iwe na sheria kali ya kulinda haki ya mfanyaji kazi, mwananchi wa Kenya.

Kitu cha mwisho nilikua, naona unachukua microphone unataka kuniondoa, lakini ninataka kusema kitu cha mwisho. Kitu changu cha mwisho ---

**Com. Wambua**: Maliza tafadhali.

**Kadir Muga**: Kitu changu cha mwisho, ni viwanda, hapa kwetu Pwani. Tuna viwanda ambavyo vinaweza kusaidia wananchi kama kule pale za Ramisi. Wale vijana ambao walikua wakifanya mitambo vya sukari Ramisi, walikuako wakifaidika kule, wakulima hivi kile kiwanja kikefungua, wafanyaji kazi hakuna, yani watu wanapata taabu. Na upande wa Kenya Cashew Nuts, hicho kiwanda kimefungua. Upande wa uvuvi kuna National Park katika bahari na hio zamani ukoloni kulikua hakuna National Park. Mvuvi alikua anaenda kuvua samaki mpaka kule pande za Kilifi na anapata biashara zake. Ningeombe Tume hii ikienda, iende ikawasilishe itufanyia hayo, Majimbo ndio tunataka hapa kulingana na mfumo wa Senate kutoka zamani Local Government vile ilivyo, Legislative Council ilivyo kuwa imepangiwa iwe ni hivyo hivyo. Hiyo ndio mimi naomba.

**Com. Wambua**: Asante sana. Ujiandikishe. Nitamuita Sevele. Sevele?

**Simon Sevele**: Naomba nionge niki simama.

**Com. Wambua**: Okey, sawa sawa endelea tu lakini dakika ni mbili tu.

**Simon Sevele**: Asante sana.

1. Ya kwanza ----- mimi nawasalamia kwanza.

2. Ya pili, jina langu naitua Simon Sevele.

3. Ya tatu, mimi naeleza Commission, asante kwa nyinyi kuja hapa. Kusema kweli, hapa Mombasa, baado tuko kwa ukoloni kabisa, kabisa, hatuja pata uhuru, kabisa. Hatuja pata uhuru kwa njia gani? Rift Valley. Watu walipewa wale wazungu walikua wamechukua Rift Valley yote na walikua foreigners, wali nyanganyua mashamba yote na wakarudi kwao ikapewa wananchi. Hapa Mombasa baado utumua uko mpaka saa hii na ndio kwa nini tunasema hatuna uhuru. Baado utumua unachanganyikana ugonjua mwingine unaitua ukoloni kwa kitu kimoja. Hawa kweli si walikuja hapa. Walichukua mashamba hii yote mpaka Malindi, mpaka Papi, mpaka Kaloleni. Wakachukua ma Title Deeds, waheshimiwa walichukua mpaka hata nafikiri walikua wanauza watu mpaka watu wakakimbia. Wakachukua mashamba bure. Sasa wakatu huu, sisi tunatoka bara hawa wengine wale wenyeji wa hapa tunanunua mashamba, ma ploti. Tukinunua ma ploti, ukinunua ploti unatoa laki moja au laki mbili. Ukinunua na unajenga, mwenyewe anakufuata, mwenye ile shambe anakuambia, hio mimi ploti ninakuuzia ni plot without land. Hata hapa tuko saa hii, nyumba hii ati ni plot without land. Kutoka hapa, mpaka Malindi, mpaka wapi, plot without land, kwani hii ni Abunuasi?

4. Point ya pili, akikuuzia pale, anakuuzia land pekee yake. Anarudi anakuuzia miti. Anarudi tena pale, anakufuata anakuambia ya kwamba, mimi ninataka kodi kutoka sasa mpaka wakati ule. Ile kodi unalipa mpaka watoto wako tumbo wanalipa. Itawezekana hio? Tena kutoka hapo, nyumba ikianguka, Waiheshimiwa, ikianguka kama umeijenga, anasema sasa hauna land pale, kwenda nyumbani, ni haki hio?

5. Sasa, ya mwisho, kufika pale, wakati sasa labda aseme atakuuzia, haya unanunua mara ya tatu. Inakua mara ya tatu. Hiyo ni haki kweli? Hiyo kweli ni haki? Pamoja na nini munasema hakuna ukoloni hapa na utumua? Baado iko hapa Coast.

6. Mimi point yangu nyingine, nafanya haraka, point ya pili, kuna simba mmoja tunae anaitua Serikali, anaitua GK. Simba huyu ukipewa Title Deed ya shamba, upewe Title Deed sasa ni umiliki hapo ni kwako kabisa. Kama usha umilikii pale, sasa uko na Title Deed yako umepewa ukipeleka Bank unapewa loan, sasa Serikali inataka saa ile unachimba na ile kajembe yako, usichimbe na tractor, saa ingine unagundua shamba yako iko na Gold, au iko na almasi, Serikali inasema feet yako ni nne tu. Sasa ni kama unapata Gold pale, lazima uhame, uende pande pengine. Tunataka Bwana Commission, hio ibadilishwe. Hiyo ni haki ya mtu. Pale umepewa Title Deed na ni shamba lako, iwe kabisa ile pale ni Mungu ame kumiliki na sikia ile ni Mungu amekumiliki ukapata bahati pale, ukapata Gold pale upewe barua ufe ile Gold, lakini si uje unyanganyue na Serikali tena uambiwe ile ni mali ya Serikali.

7. Point nyingine, mimi namalizia: Mambo ya maji. Mambo ya maji katika Coast. Tunalipa maji pale kwa wale watu wa maji, tunalipa water, mpaka iko kodi ya kulipa maji ati ya kulipa ile dawa ya kuwekwa maji. Saa hii Bwana Commissioner, tunakunyua mchanga Mombasa hata ni bahati umepata hii watu hapa. Haungepata mtu mmoja hapa.

Tuna kunyua mchanga, hakuna dawa kabisa, kabisa, without exageration. Hakuna dawa. Tunakunyua mchanga, ukifungulia. Je, hii jin tulibandikua na Serikali aki saidiana na yule mwenye shamba at squarter, ni nini hio? Squarter ni nani?

**Com. Wambua**: Asante sana Bwana Sevele. Jiandikishe hapa tafadhali. Sass tutamuita Mwachatamu. Mwachatamu yuko?

**Mwachatamu**: Jina langu naitua Mwachatamu Juma Hassan kutoka Vok, Kisauni. Maoni yangu, natka kila mwananchi ya Kenya awe na makao kamili ya kuishi. Kila mwananchi wa Kenya awe na makao.

**Com. Wambua**: Fanya haraka kidogo.

**Meachatamu Juma Hassan**: Mashamba yote ambao kwamba amemilikiwa na watu binafsi yachukuliwe na Serikali.

Serikali ya nchi ya Kenya na pendelea iwe ya majimbo.

Dini ya ……… (tape complete)

**Speaker:** Ukiwa unagundua shamba yako iko na Gold au mercies, Serikali inasema vitu yako ni nne tu, sasa si kama unapata Gold pale, lazima uhame uende pahali pengine, tunataka Bwana Commissioner hiyo ibandilishwe, hiyo ni haki ya mtu, pale umepewa title deed na ni shamba lako, iwe kabisa pale ni Mungu amekumiliki ukapata bahati pale, ukapata Gold pale, upewe barua uuze ile Gold, lakini si uje unyanganywe na Serikali tena uambie ni mali ya Serikali .

La tatu na mimi namalizia sasa, mambo ya maji, katika Coast tunalipa maji kwa Minister of water, mpaka iko kodi ya kulipa ile dawa ya kuwekwa maji. Saa hii Bwana Com. tunakunywa mchanga Mombasa, hata ni bahati umepata hawa watu hapa. Ungepata mtu mmoja hapa. Hakuna dawa kabisa, kabisa without exgerations. Je hii jina tulibandikwa na Serikali, akisaidiana na ule mwenye shamba eti Squater, nina huyo?

**Com Paul:** Asante sana Bwana (inaudible) jiandikishe hapo tafadhali. Sasa tutamuita Mwacha Tamu, Mwacha Tamu yuko,

**Interjection inaudible**

**Com. Salome**: Uanze na jina lako**.**

**Mwacha Tamu Juma Hassan:** Jina langu naitwa Mwacha Tamu Juma Hassan, kutoka Vok Kisauni, maoni yangu, nataka kila Mwananchi wa Kenya awe na makao kamili ya kuishi, mashamba yote ambayo kwamba imelikiwa na watu binafsi, ya

chukuliwe na Serikali, Serikali, ya nchi ya Kenya napendekeza iwe ya majimbo, dini za Kikristo, tafadhali naomba ziwe mbili ili kutatua fujo Nchini.

**Com Paul:** Tafadhalini, tafadhalini, nini mnaweza kutulia, umemaliza?

**Mr Juma:** Nimemaliza.

**Com Paul:** Ya mwisho umesema dini ya kikristo ziwe mbili, moja iwe gani na ingine gani?

**Mr Juma:** Dini za Kikristo, mimi ninasozikia ni nyingi sana, najua moja tu Catholic pekee yake, hizo zingine kila mtu ataja kivyake, kwa hivyo ni ngeomba Catholic, na nyingine yoyote lakini ziwe mbili tu, ili kutatua ile fujo.

**Com Paul:** Asante sana tumesikia, Agnes Nyaro tafadhalini tulieni, tusikize wenzetu, Agnes yuko, Agnes, kuna Walter Botela, nilkuwa nimemuita hapo awali, ako, Walter Botela aje hapa mbele atoe maoni.

**Interjection:** (inaudible)

**Walter Botela:** Kama mnavyo ona nimepewa muda mfupi sana kusema, nitasema kwa ufupi nanyi, jambo ninalotaka kusema ni la umuhimu mkubwa sana, ni rahisi sana kuja hapa kukutana kutoa maoni Walter Botela, mimi ni Walter Botela, na ni mzee wa mtaa wa Sublocation ya Via Town na pia ndiye mwenye kiti wa chama kipya tulichokiunda kinachoitwa Via Town Resident Society. Nimeanza na ardhi, mamaliko na matatizo ya hawa watu ni mingi mno, na maoni tutatoa moja moja si vibaya, watu wote tukipewa nafasi ya kutoa maoni ni vizuri juu matatizo ni mingi, kwa hivo ukipata maoni mengi ndio mzuri.

Langu moja tu ni juu ya ardhi, hii tunaikalia, ardhi hii inafanya watu wa Coast wanateseka sana, kwasababu wakati hii Constitution ilipotengenezwa ya Kenya ama wakati uhuru ulipokuja, mara moja kulitengenezwa chama kimoja kinaitwa Land Ajudication something, ambayo kilikuwa kinatembea sehemu Zote kuangalia kwako ni wapi, ili kila mtu ajue mahali pake au masikani yake aijue, itengenezwe. Mbali huo mpango ulipokamilika kule Bara, uliteremka Pwani, ukifika Mariakani, hauwezi kuendelea mbele, jaribu mara mbili tatu watu wa Civic Education waenda Pwani, wakifika Mariakani hawawezi endelea mbele, na huku matatizo ya huku ni makubwa, na hii matatizo iko mikono ya watu wakubwa, basi ni Nchi ya washida. Kwa hivo twatakiwa tuwe na Constitution za kuangalia mambo ya Pwani, jambo la kwanza ni ardhi, ikiwa Constitution ni ya Kenya mzima, wacha iwe ni ya Kenya mzima, leo Constitution ya Kenya haiambatani na mambo ya hapa Pwani kabisa.

**Com Salome:** Kwanini haiambatani?

**Mr Walter:** Kuna sehemu nyingine za hapa Pwani pande za huko Kilifi huko mpaka Malindi, kuna watu ambao wanatawala

ardhi, mimi nilijua ile kingereza Squater ni lipokuwa Bara, jana. Squatter ni nani ? kumbe ni mwafrika anayekaa katika shamba la mzungu sio. Basi karibu idadi kubwa ya wafrika wa nchi ni wa Squatter kama pande za malindi, mpaka Kilifi kote huko ni mashamba ya watu wasio wa Kenya lakini ni mali zao. Ukienda pahali pote utapata pahali pa kukaa lakini wewe utakuwa Squatter, kwa hivo maisha yako yote wewe ni squatter, squatter katika nchi huru mambo gani haya.

Langu la mwisho, which is very important, nilipokuja hapa Town ni kakuta maskani ya Babu yangu, ninakakuta kuna watu ambao walipewa ardhi na vibaba zetu, yani ni wazungu waliokuwa Serikali ya wingereza kama acre 50, wakaambia wagawanye, na zilikatwa kado kado zikapewa watu mpaka leo wako, wakati Kenya walipewa uhuru in 1963, hiyo ndio ilikuwa mwisho wa vipande za ardhi,haijulikani ilikuwa aje na tukaambiwa hii ardhi tunakalia ni ya, Municipality mpaka wa leo, basi katika contribution ya ardhi, kuna marshati kama hayo ya, atakaye kuwa mmliki wa mwisho wa hii ardhi kabisa kabisa ni nani, hiyo inaitwa ultimate ownership, mpaka mufikirie ni nani atakayekuwa na mamlaka ya mwisho kabisa, kwasababu huyo mwenye mamlaka ya mwisho, anatakikana kabisa katika nchi hii, yeye ndiye mwenye uwezo wa kumuondoa. hata mwenye anauza viatu atoke hapa. Inatakikana Serikali inayoangalia ardhi kwa nchi mzima, ikupatie mahali pengine lakini iangalie ile mali ya nchi mzima sio kwa mtu mmoja.

**Com Paul:** Mzee Walter ni takukata.

**Mr Walter:** Na maliza.

**Com Paul:** Maliza tafadhali.

**Mr Walter:** lakini ultimate ownership inatakiwa, watu wanakubaliana, Serikali ni ya kuchunga haki ya watu, kwa hivo angalia mambo hayo.

**Com Paul:** Asante sana Mzee Walter, jiandikishe pande ile tafadhali, sasa tutampa nafasi muheshimiwa (inaudible) sababu yeye ni mjumbe wa Kisauni, sababu yuko nasi siku ya leo, watu ni wengi wanao taka kuongea muheshimiwa na tunawapatia tu dakika mbili mbili, lakini wewe tutakuongezea tukidogo, kwa hivo ufanye hima.

**Muheshimiwa wa Kisauni:** Hamjambo watu wa kisauni!

**Wananchi:** hatujambo.

**Muheshimiwa wa Kisauni:** Mimi sitaki kusema mingi kwa sababu, kesho wajumbe wote wa Pwani watakuwa na nafasi za kutoa memorandum zao kwa kamati ya kukusanya maoni ya Katiba Kenya mzima. Isitoshe ninayo nafasi nyingi saidi ya kutoa maoni yangu, kama mnavyojua Kisauni imebahatika kwamba katika ile kuu ya Bunge, mimi ni mmoja wa wale members, ni na

cheo kikubwa, sitaki kusema ni boss ya hawa, lakini Bunge likija tutauliza maswali. Kwa hivo leo nije ni kuwa kutoka asubuhi nisikize maoni ya watu wa Kisauni, imeenda old Town watu wamejaa wengi, na wanatoa maoni sawasawa na yenu, nani mekuja hapa na nimefurahishwa kwamba, maoani yenu ni ya kupendeza saidi.

Commissioners taabu niliyo nayo, ambao ni lazima ni lalamike ni kwanini mliwapa siku mbili Shangamwe na Mvita, na mimi Commissioner kama mkubwa wenu, na mnanipa siku moja na mnaona vile Wananchi ni wengi, kama manweza kukaa jiono na wale wataenda nyani kesho watakuwa wadogo mrudin hapa asubuhi at least msikize hawa Wananchit, hiyo ndio ombi langu. La mwisho kabisa kwa sababu Wananchi wenyewe wanataka kusema, yale yote utakayosikia hapa Commisssioners, kwasababu ninyi Commissioners mmetoka Bara ukweli ambao lazima muuchukue na muambia watu wakutoka Bara ni kwamba Pwani sio Kenya, and that is the truth.

Kwa sababu ushahidi tunao, na umetolewa na mtapata memorandum nyingi, tuko na ripoti ya Kenya postal street mwaka wa sitini na mbili ambapo inaelezwa wasiwasi, maana malalamiko haya yote unasikia ya ardhi, ni kuonyesha kwamba Katiba ya Kenya haikucover watu wa Pwani ilipokuwa ikipitishwa tuwe waKenya, kwasababu Katiba ya Kenya ya sasa inasema, you have the right to own land anywhere in Kenya that's right, Katiba ya Kenya ya sasa inasema, mwenye title deed ndio mwenye ardhi, lakini mmesahau ya kwamba, ordiners act ya 1908 ilipokuja hapa, sisi watu wa Pwani ambao tulikuwa tuko kwenye protectorate, Kenya zilikuwa mbili, kulikuwa na Kenya colony, na Kenya protectorate ambao ni sisi, sasa Kenya protectorate, tafadhalini ma Commissioner na Wananchi tusikizane hakuna haja ya kupigiana makofi, Kenya colony ilikuwa ni watu wa Bara.

Kwasababu mlikuwa mnaongozwa na mzungu, sisi hata siku moja hatujatawaliwa na mzungu, sisi tumetawaliwa na Sultan, kwanza tulitawaliwa na Mreno, akaondoka, akaja Portuguese akaenda, akaja British halafu akarudi tena wa Omani halafu kukawa na agreement mwaka wa 1886 kwamba sisi tuwe chini ya protectorate, na ordinors wakati ilipokuja ya 1908, mashamba yalipokuwa inagawanywa katika Kenya hii, that is the claim, sisi watu wa Pwani ambapo tulikuwa ni wa afrika weusi, haturuhusiwi kusema hii shamba ni yangu, kwasababu wakati ule, wa Arab walikuwa wameshida vita, na Mazrui waliokuwa wanaitwa Mujirishi, walikuwa wako pale Takaubwa, wamepewa ardhi, ndio walioruhusiwa peke yake kuota mashamba ya wa Arab na Mwafirka alikuwa akiota shamba wewe huruhusiwi, that is how we were displaced, as Africas.

Sasa tulipokuwa tunarejeshwa Kenya 1964, baada yake mnapata uhuru na mnaendelea na Sheria zenu za Kenya, mkasahau ya kwamba all free hold lands na iko agreement hata million moja ilitolewa, ambayo inasema wazi, kwamba free hold land zote, za wale tunaita Sultan decendants zilegeshwe hawa walio hapa wote, there is an agreement money was paid, why didn't the Government of Kenya give us that right. Pili Kenyatta kwasababu wakati ule alitaka hii yote beech plot, kwasababu siri ya hapa, wakati tuanpata uhuru Mwarabu hana title deed katika beech area, walikuwa wanaogopa majini, hawataki kukaa huko. So the first floor was clear, wakati ule Koinange akiwa Waziri wa Tourism, akamwambia Kenyatta aandike barua kwa Shamte, kwamba kwasababu watu wa hapa ni Waislamu, zile free holds zote zitakaa kwa Waislamu na twasoma madarasa, sawa sisi ni Waislamu weusi, wakati ule Shamte alikuwa ni Mwarabu.

Sasa kwanini tulegeshewe Uislamu na ardhi siende na watu weupe, that is the question you should ask yourself, you see, that is where we sailed, ndio sisi tunasema, katika Katiba hii maoni yake manayo kusanya katika Kenya, sisi watu wa Pwani tunataka Katiba maalumu yetu, ama msipokubali tutajitenga vile vile na tuwe

**Interjection inaudible**

**Mheshimiwa:** Na nina sema hivo kama mwakilishiwa hao kwasababu, I am not inciting everybody, na nimesema the same this morning, kwasababu hakuna Serikali yoyote ya Kenya kuanzia Kenyatta ya Moi imetutabua, imeendelea kutuua na kutupiga, kitu ambacho tuansema ni kitu moja, ningewaomba Commissioners msikize watu hawa, malalamiko yao, na muyasikize yakiwa ni malalamiko ya watu special, kwasababu Kisuani Constituency, ndio Coast Province, Coast Province ilianza hapa. Hapa ndio koti ya kwanza iko hapa mji wakale ambao ni Kisauni. Na pia kwa uchungu wa kupigania Katiba ya Kenya, sisi tumeeanza, kama mzee wa Via Town huyu, ardhi aliyo sema, huyu inahusiana na slaves walionunuliwa hapa, wamepokonywa ardhi hiyo na iko katika Katiba, walikuwa na Ward yao inaitwa Via Town, juzi tumepigania ndio hiyo imelegeshwa, ilikuwa imeondolewa na Serikali hii hata hawajui proto code nini.

Tumeanza kukataa hata kulipa kodi ya mashamba ili Serikali ijue ya kwamba, sisi tulidhurumiwa, bado wanasema apana, kwa vile wale wako na Title deed, wale wakina nani, na sisi we were transferred

**Mheshimiwa:** We were transferred, from the Sultanish to Kenyans, why don’t you recognize us, kama ninyi mliokuwa colony kule, wazungu, wakikuyu walipopigana, na wazungu wakafukuzwa wakaenda uraya, kwanini mliorganize yourselves mkanunua mashamba ya wazungu, why cann’t you organize us and buy the same land which was free holds. That is the biggest problem we have, na utakuta kila mtu ata complain land, as if it is the Constituion, because Constitution it means a wider range of says, tunataka utamaduni wetu,tunataka kuzungumzia mambo yetu, kama hatungekuwa na problem ya land, leo tungezungumzia hata mambo ya mijikenda, tabia zao kwa wanawake. Mmjikenda akikuta mwanamke amelala na bwana ingine anataka maru, kwa nini mwanamke asiruhusiwe naye akapige maru, yule bibi amelala na Bwana.

**Interjection inaudible:**

**Muheshimiwa:** Those are the things, hiyo ndiyo vitu ambao tungezungumza kama hatungekuwa na matatizo ya land. Ndio tunasema ya kwamba Wananchi hawa watatuliwe, lakini utakuta the whole Coast region, problem inayozungumzwa ni Constitution, wanataka land, you should see the difference why tumekuja Coast Province, kwanini mlienda kwingine hamkusikia. Tena hawa watu wanalia majimbo kwasababu gani, wajua wazi kwamba mtu anatoka Nairobi, na karatasi anakuja kumuondoa mtu hapa ni ardhini kwangu wanapewa Nairobi, ndio wanaamini kama Majimbo imekuja, mujaluo au mkikuyu hawezi kuja hapa. Sio ati juu wanaipenda,no there see the cure of that ni hiyo. Na hiyo ikiletwa katika Constitution is not a

good thing, but they have been brain washed, what we want, in the Constitution ni kwamba, kama Katiba ita gurantee kwamba mtu wa Pwani apewe ardhi yake na tuishi pamoja,

(inaudible) Kisauni tumejipigania tumeanza kugawanya hata settlement scheme, hatujafukuza Kikuyu, tukipata Kikuyu yuko pale tunampa Tile deed tukipata Jaluo yuko pale tunampa title deed, maanake yeye na Mpwani walikaa pamoja. Kwa hivo mimi sina mengi saidi, nitachukua wakati mwingi kesho ndio nitambomoa huku, lakini maombi yangu, kama mna nafasi mrudi hapa kesho, ili Wananchi wangu wapate siku mbili kama Mvita na Shangamwe, thank you very much

.

**Com Paul:** Asante sana Mheshimiwa, pengine ni sahihishe kitu kidogo tu, ijapokuwa, hapa mlipewa siku moja lakini vikao ni viwili, tuko hapa leo Mlaleo Primary School kuna kikudi kingine cha ma Commissioners kiko huko Barochi hall, kwa hivyo,

**Mheshimiwa:** No, in Mvita you gave two days,

**Com Paul:** Lakini tulikuwa kikao tofauti one panel.

**Mheshimiwa:** No,no, there were two panels.

**Com Paul:** It was not two I was there it was only one panel

**Mheshimiwa**: Two days?

**Com Paul:** One panel for two days, so there was two sittings

**Mheshimiwa:** Why don't add up, I am a member of your Commission, tutahonga kidogo.

**Com Paul:** tutapeleka ripoti halafu kesho, tutakueleza maana lazima tupange mpango wa kurudi, tumesikia, kama hatutamaliza kusikiza watu, ni lazima tufanye mpango wa kurudi hapa hiyo ni kawaida wale ambao hatutawasikia, msiwe na wasiwasi tutarudi hapa kuwasikiza juu hata tuko namajina yao. Lakini siku yenyewe hatutasema ni kesho, maana ake lazima tupeleke ripoti halafu tupewe naasi tena kutoka huko turudi hapa tena. Kwa hivo tutaendelea, tumemsikiza Mbunge wetu hapa Garisa Maitha. Kwa hivo tutawapatia Wananchi nafasi kama alivyosema, tumuite Masono Joseph, yuko hapa, aje hapa mbele tafadhali. Ufupishe maneno tafadhali kwa sababu watu ni wengi hapa, tuone kama tunaweza kuwapatia wengine nafasi, dakika ni tatu tu tafadhali.

**Masono Joseph**: Mimi kwa majina naitwa Joseph Masono.

**Interjection inaudible:**

**Mr Joseph:** Mengi yamezungumuzwa, yangu nitazungumzia mada mbili tu peke yake, ya kwanza nitazungumzia kuhusu Adminstration, yani utawala, ya pili nitazungumzia Judiciary Mahakama. Mimi yangu maoni ningependekeza kwamba Raisi awe na nguvu zile zile, lakini kuna kitengele Fulani, ni maoni yangu,

**Interjection inaudible:**

**Com Paul:** Tafadhalini tunaweza kutulia

**Interjection inaudible:**

**Com Paul:** Sasa wacha ni seme hivi, mmekosea, maana ake sisi tangu tuketi kutoka asubuhi, tunasikiza maoni ya kila mtu, hata yakiwa tunayapenda, akiwa hatuyapendi, kwa hivyo tupatie huiyu nafasi aseme ile anataka kusema, kwa hivyo ikiwa huyapendi ni maoni yake, sio ati itakuwa Katiba wacha aseme yale anayotaka kusema, endelea mzee.

**Mr Joseph:** Yangu ni kwamba Raisi awe na nguvu zile zile lakini vitengele Fulani zibadilike, kama moja ya kusema Raisi asiwe juu ya sheria, hiyo ibandilishwe, ili akikosea adhimbiwe kama wanaKenya wengine, na pia hawa Adminstrators kama kutoka PC kurudi chini wachaguliwe na Public Service Commission. Ili anapokosa na asibadilishwe akapelekwa sehemu ingine kama ilivyo sasa. Maana ilivyo sasa ni Machiefs na Manaibu wao peke yao ndio huchaguliwa na Public Service Commission na kwa hivyo anajali masilahi ya yule mtu aliyemteua. Pia ningependekeza kwamba nguvu za Chief sipunguzwe na wafanye kazi kama watumishi wengine wa Serikali, juu Chief huripoti ofisini saa tano, na saa sita ametoka. Pia ningependekeza kwamba Kenya ibaki nchi moja Unitary State, baada ya kuwa na majimbo, maana ake hapa Pwani kwetu,

**Com Paul:** Mupeni nafasi, apewe nafasi aseme yale anasema, tutampa nafasi azungumze maana kila mtu amepewa nafasi yake, kwa hivo endelea.

**Mr Joseph**: Hapa Pwani kwetu, tuko na port ambayo inaleta mapato, na kuna tourism na kuna sehemu zingine za Kenya kama North Eastern kule, hakuna chochote ya weza kuleta maendeleo ya ile Mkoa, kwa hivo tuseme ati Pwani ijitenge, kwa mfano kama Western wana miwa, sukari iko, samaki inatoka ziwani, Rift valley iko na pryrethrum, iko na majani, iko na wheat, Mkoa wa kati uko na majani na kahawa, je North Eastern watafanyia aje kujiendelesha.

**Com Paul:** Sasa tafadhalini, inaonekana hamtaki tuendelee, na kama hamtaki kweli tuendelee sisi tutafunga na ofisi na tutaenda, kwa hivo tumpatie nafasi azungumze yale ambayo anataka kusema halafu tuendelee, maoni yake ikiwa tofauti na yako mpe nafasi, maana ake hiyo ni haki yake.

**Mr Joseph:** Kuhusu Judiciary, ningependekeza majuges wachaguliwe na Bunge badala ya Raisi, kwa sababu wakichaguliwa na Raisi watakuwa wakijali maslahi ya yule aliyechagua sio maslahi ya Wananchi. Katika maongozi ya mashtaka, iwe ikitoka kwa mkuu wa sheria ambaye ni kiongozi wa mmpaka chini, pasiwe na polisi anayefanya ya prosecution, kuajiliwe watu ambao wana utaalamu hata angalau a trainewe katika nyaja hiyo hata kama ni certificate in law ili prosecute cases sio polisi. Na hii itasaidia kubuni kazi maana yake vijana wengi wa trainiwa katika hiyo nyaja, badala ya kutumia polisi ambayo tayari ana mshahara anapata.

**Com Paul:** Maliza

**Mr Joseph:** Nimemaliza, asante sana na shukuru.

**Com Paul:** Asante sana, kwa hivo jiandikishe huko, tumpatie nafasi Muhamed Ngumbi, jiandikishe hapo, tusikize Muhamed.

**Muhammed Ali Ngumbi:** Jina langu naitwa Muhammed Ali Ngumbi, na mimi ndiye Secretary wa Kisauni Lands Lobby Group, kwanza nasema Saalamu waleykumu.

**Wananchi :** Waleykumu saalamu.

**Mr Muhamed:** Muheshimiwa, Bwana Ma Commissioners, ningependa mnipatie muda wa kutosha ili kupresent kesi yangu kwa watu wetu wa kisauni.

**Com Paul:** Wa kutosha utakuwa ni dakika tano tu nitakuongezea mimi.
**Mr Muhammed:** Hasinitoshi kusema ukweli.

**Com Paul:** Ni hizo tu hakuna zingine

.

**Interjection inaudible**:

**Mr Joseph:** Mimi nitakupatia Historia tu kidogo halafu nitaendelea na resolutions zetu. Kwa vile tulikuwa under the British protectorate from 1888 na tukiingia katika Kenya colony 1895, sisi tumekuwacolonized miaka 67, Kwani mnavyo jua Kenya ilikuwa imegawanywa mara mbili, upande wa juu ambao ni wa Bara, na upande wa chini ambao pia ulikuwa colonized and at the same time ulikuwa chini wa utawala wa sultan.

**Com Paul:** Utusaidie kutupatie proposals maanake hiyo historia tumepewa.

**Mr Joseph:** Kama unavyoelewa ardhi hizi, zilikuwa chini ya utawala wa Sultanate, hicho ni kipande nilikuwa nataka kukueleza, kipande kifupi sana cha history katika zile proposal zangu ambazo nitaleta hapa zinafuatana na mambo kama hayo. Jambo la kwanza sisi watu wa Kisauni tunasema, zile title za kikoloni from 1908 zote ziwe newlified na subdivision siwze kufanyanyike kisawasawa katika area yetu ya Kisauni.

Namba ya pili, kuna ardhi ambazo zimekaa hazijatumika mpaka leo, tunasema ardhi hizo, kwasababu ya wingi ya watu walivyo Kisauni, zisichukuliwe mara moja na siweze kugawanywa kwa watu walioko, kwasababu ni ile ile lakini watu wanaongezeka kila siku. Tunataka ardhi ambazo hawa walitumia kitu kinaitwa trustee ili kupatia pesa nyingi nyingi kutoka kwa mabenki, ardhi kama hicho zichukuliwe na siweze kugawanyiwa watu vile vile vile, mara moja. Kwa sababu hizo ardhi zilipatikana wakati huo, kwa kuinua maisha ya wale decendants of the soldiers, kupitia Agriculture, leo hakuna ardhi tena ya kulima katika kiasuni hii, bali ilizoko ni majumba hapa hakuna tena kulima . Kwa hiyo ardhi ilioko hapa ambayo imejengwa, kila nyumba iliyo jengwa juu yake ipatiwe sub division na titile yake iweze kupatikana mara moja.

Tunapendelea vile vile kupatikane proper planning, kwasababu kisauni ni pahali ambapo palikuwa pamesahauliwa, kuweza kutoa BaraBara na mambo ya drainage katika kisauni. Ardhi ambazo wenyewe ni Warabu, wako katika Nchi nyingine za nje kama vile Mascat, London, Canada, America, ardhi kama hizo tungependa Serikali mara moja na tunaweza kuwafanyia sub division watu wetu hapa. Zingine ziko na madeni makubwa sana ya municipal kama 1 million outstanding rent, tunataka ardhi kama hizo kuchukuliwa vile vile na tugawanyiwe, ama sipatiwe 14 days na ikiwa hauwezi kusettle deni lake basi ardhi hiyo ipatiwe moja kwa moja ipatiwe watu wa kisauni waweze kujiganyia.

Government lands zichukuliwe na kupitishwa chini ya DC na kupitia sisi wana Lobby Group pamoja na Mbunge wetu ili tuweze kuwagawanyia watu wanaoishi katika ardhi hizo. Ardhi ambazo wenyewe hawajitokezi, either kwa kujificha kwasababu wako ngambo lakini wameaachia mawakiri na ma agent wa ardhi, kwasababu ya kutoza kodi kwa watu, ardhi kama hizo tafadhali tunaomba Serikali iweze kutukubalia sisi, kumuita mwenyewe haswa tuweze kumuona, ama sivyo kama hatajitokeza basi siweze kuchukulia na sisi tugawanyiwe.

Kuna ardhi ambazo sinaitwa warp Lands, Warp ni kitu ambacho ni cha jamii, kinanufaisha kila anayekaa katika ardhi hiyo, kwa hivo ardhi ziko nyingi sana hapa Kisauni na Mkoa wa Pwani kwa jumla, tungependelea ardhi kama hizo vile vile ziweze kuchukuliwa na kugawanyiwa watu mara moja. Kwa vile umiliki wa shamba katika Kisauni hii ni mchache katika subdivision itakayoendelea, tungependelea kila mmoja aweze kupata angalau karobo acre, ili kuweza kumasaidia kujenga makao yake na kumsaidia katika familia yake.

Political boundaries, ningependelea kusema hivi, watu wa Kisauni wamekata kwamba, political bound ya Kisauni ianzia Nyari bridge main land north, mpaka kikabala ambayo ni mpaka wake wa zamani, kwa hivyo iwe ni Constituency ya peke yake, na

kule ambako ni mjini basi wanaweza kuingiza kadokado wa Sharif Nassir huko Central, na sisi tujisimamie wenyewe.

**Com Paul:** Malizia tafadhali.

**Mr Joseph:** Sawa sawa, tukiwa na Mbunge wetu na macouncillor wetu na kila kitu, mambo ya maji ya maji tungependelea tuwe na flat rates ya shillingi mia 200 kila nyumba, hata kama unatumia maji hayo kivipi iwe flat rated kamavile Bara inavyo fanyika. Mambo ya stima kila nyumba ichargiwe shillingi mia nne, na ikiwa kuna home industries ifike kama shillingi 1000 na ikiwa kuna industries inategemea na ile Idara Power and Lightening kuwacharge kisawasawa.

Upande wa uvuvi watu wengi wameeleza, na nimesema hapa kwamba uvuvi watu wa hapa Pwani wanaonea,kwavile watu wetu wanatumia madao, na foreigners wanatumia trollers na inakuwa tofauti kubwa sana, kwa hivyo wavuvi wetu wa hapa wapeewe nafasi wafanye vile wanavyotaka kwasababu hata samaki wale wanaovua baharini ni kidogo kidogo, na hiyo ndiyo wanafanya ili watoto wao wasome.

Habari ya city council resources, kwa vile Pwani imebahatika na kuwa na makampuni yote makubwa yakokatika area ya Pwani e.g Bamburi, Oil refineries, Kenya pipeline na mengineo mengi, tungependelea kwamba makampuni kama hayo yawe yanatoshwa ada maalumulya kusaidia City Council yetu, ili kuondosha matatizo ya mishahara na kutengeneza Barabara na kadhalika. Vile vile watu wa kisauni wanapendelea mambo yachakula, price control, irudi kama zamani. Kama chakula muhimu kama unga wa ngano, unga wa mahindi,

**Com Paul:** Dakika niliyo kupatia zimeisha.

**Mr Muhamed:** Mchele na kadahalika, nipatie dakika mbili.

**Com Paul:** Hiyo sasa utachelewesha kidogo.

**Mr Muhammed:** Dakika mbili tu.

**Com Paul:** Memorandum tutaisoma,

**Mr Muhammed:** Ni sawa lakini dakika mbili nimeomba.

**Com Paul:** Kwa hivo nitakupatia nusu dakika umalize, tafadhali.

**Mr Muhamamed:** Haya, tunakwenda kwa Adminstration leaders, tunapendelea kwamba, Administration leaders wote, katika

Mkoa wetu hapa wawe wanatoka area yetu yenyewe hapa Mombasa hatutaki kuletewa Administration Leaders kutoka nje. Habari ya health kidogo, sababu ya hali ya madawa yamekuwa Ghali sana na vile vile hospitali hazilalliki siku hizi, tukipendelea kama watu wakisauni tuongezewe kujengewe mahospitali, na yale yalioko hapa yaweze kupanuliwa ili tuweze kusaidika. Citizenship, mtoto akizaliwa nayeye ni mKenya halisi, na hakuna maana ya kumnyima vibali ya uraiya hapa kwa hiyo aweze kupata Birth Certificate yake, ID card yake na Pass port yake on the sport, ili akitaka kuitumia iwe ni urahisi kwake.

Jambo la mwisho, ni upande wa dini, wale ambao ni waislamu wakiingia ukristoni, ni lazima majina yao yaweze kutengezwa according to their documents, na wale walio wakristo wakiingia upande wa waislamu vile vile zile karatasi zao zinatakikana zitengenezwe mara moja, juu hii inaleta fujo, wakati mtu akifariki wakati wa madhishi ikiwa ni muislamu mtu anakosa haki yake ya kusikwa kislamu na kama ni mkristo vile vile. madawa ya kulevya, yameharibu sehemu zetu hizi, nimapendeleo yetu kwamba rehibilatation centers zinjegwe kila Constituency. Mwisho kabisa, ni juu ya Human rights, polisi wa be friend ordionary citizens ili kuweza kupatikana uhaki wakati ikiwa wataweza kukamata mtu yeyote, na evidence ya kutosha iwe itatolewa ndio mtu huyo aweze kupatikana hukumu yake ya kisawasawa, kwa hayo machache ni tapeeana memorandum.

**Com Paul:** Asante sana, ngoja tu, hii Warp lands simesema iwe redistributed kwa Wananchi si hiyo ni mali ya waislamu unataka wapewe akina nani.?

**Mr Muhammed:** Sisi Bwana Commissioner tunaishi katika Pwani hii kwa utengamano, hatubagui baina ya Bara wala Mpwani, ikiwa umeshajenga hapa na hiyo shambaiwe ni ya warp lands basi kila mmoja agawanyiwe pahali pake aweze kujipatia kitile chake, asante.

**Com Paul:** Jiandikishe hapo tafadhali, Muhammed Asuman, uko, endelea mzee, mzee ametumia wakati mwingi, kwa hivo tutakupa dakika mbili tu useme ile ya muhimu, tuendelee. Tumpatie mzee Asumani nafasi tafadhali azungumze.

**Muhammed Asuman:** Jina langu naitwa Sheikh Muhammed Asuman Todoo:
(**in venacular)**

**Muhammed Asuman:** Mimi maelezo yangu nishaandika yote kamili hapa, isipokuwa tu najieleza jina langu, basi, nitawapa hii memorandum yangu, mtasoma mtakavyo yote, isipokuwa tu nataja sehemu mbili, lakini nasiongezea kusiu (inaudible)

Kuhusu majimbo, mimi nikiwa kama Professor au Imam wa jimbo hili la Mombasa, Coast Province, ni haki yetu sisi kupata majimbo yetu tuweza kuipeleka kisawasawa. Pili utaona religion yetu ya kislamu imeaanza kutoka bali kama vile Bwana Maitha alivyoeleza, si leo si jana, kwa hiyo ile asiri iko vile vile, lazima kupatikana heshima ya kutunzwa na kujulikanwa na kupewa nafasi yake bila matatizo, sasa ukitiliwa vikwazo vikwazo vikwazo ndio Serikali inaleta yenyewe matatizo na wale waislamu, ambapo waislamu ni watu wazuri sana, kama walivyosema Serikali kwamba waislamu ni watu wabaya, hii ni siasa ya kikoloni

ya kiubaguzi wao wenyewe, mimi ni kiwa kama professor nimesoma Koran sharifu naninajua ilivyo, kwa hiyo hakuna haya yakusema kwamba waislamu ufanye ubaya kwa mtu mwingine hakuna, na ikiwa yuko, aje mbele yangu tufanye challenge juu ya Koran, na ile Katiba yao au Bibilia tutazungumza, kuonyesha kwamba uislamu ni kitu kizuri kina amani cha penda amani kwa watu wote hiyo ni sehemu ya kwanza.

Sehemu ya pili ni kwamba mmekuja lakini mpeleke ripoti ya heshima kubwa kwa hao wazee wetu walioko huko, kwamba tuptiwe nafasi ya heshima ya ofisi yetu ya Kadhi, office yetu ya Ukadhi imebanwa banwa sana, haina hata mpangilio wowote inabakia kuoza kuacha basi niwie radhi, ambapo ziko hukumu nyingi sana kulingamana na Historia na Koran ni (inaudible) hukumu kushida za kizungu, mimi nimesoma sheria katika chuo kikuu cha Lazaraus Chariot Misiri, halafu nimesoma sheria zote mbili, koti inavyofanya hapa ni kinyume kwa makoti mengine, ni me kwenda Misiri, Uraya, German mpaka Vetican nimefika kwenda kufanya kireligion, vetican nimekaa mwaka mmoja na nusu. Waislamu si wabaya, ni yale matendo mabaya yaliyofanyiwa waislamu na wao wakawa wanalipisha au ni kwamba wao nao wanaona uchungu hali wanaofanywa, kwa hivyo naona office yetu ya kadhi iweze kupewa nafasi mzuri, ifanye kazi kwa ukamilivu na watu wahudumikiwe kisawasawa. Kwa hiyo naomba memorandum iko hapa, hayo yote yako dani na mengineyo, kwa hiyo namaliza ili nipatie wenzangu nao nafasi, sitaki niseme mengi sana kwa hiyo nawaambia,
**(in venacular)**

**Com Paul:** Asante sana Sheikh Muhammed Asuman, jiandikishe hapo na utuachie memorandum tutaisoma kwa makini sana, nimesikia maneno yako. Nitamuita Bwana S O Miroto.

**Interjection inaudible**

**S O Miroto:** Mimi yangu ni machache,

**Com Salome:** Majina yako tafadhali, aanza na majina yako.

**Mr Miroto:** Mimi yangu ni machache, kwa jina yangu naitwa Sammy Onyango Miroto, lakini nimeshukuru sana kwasababu wengi wetu wamechangia kuhusu ardhi ambapo kule kwetu Nyanza ile ninaoana hapa haiko huko, sasa nimewaunga mikono kabisa kwa maaana Kenya ni moja lakini kule hata kama ukiweka shamba lako utaikuta tu, lakini hapa wale Wananchi hapa hawana shamba hiyo ni makosa sana.

Sasa mimi yangu kabisa nitaanzia na education, najua gharama ya malipo ya karo imeenda juu sana, sasa nimeomba Serikali yetu tukufu iweke hii gharama wamewekewa hii malipo watu wanaenda chuo kikuu, ninzuri sana, lakini wale wanaenda polytechnic, pia wamepita mtihani na wazazi wanasumbuliwa na malipo na kuna pesa imewekwa mingi kwa office ya President, ili that budget should be reduced, halafu hii pesa iwekwe kwa Ministry of education isaidie wazazi kwa kulipa karo ya watoto

wao kwa polytecnic.

On top of that mimi ningependa, the appointment of BOG kwa shule na PTA waangalie kabisa, kwa maana wale watu ndiowanaongeza karo, kwa maana wengi wao hawana watoto kwa hizo mashule na wakiongeza karo, ingine inaenda kwa allowance yao, sasa hapao wazazi wanaumia sana. On the employment act, iko Cap 226 kuna cross in surbodination hii imeua watu wengi sana kwa employment, jamani nigeomba Serikali tukufu, hii mabadiliko ya Katiba hii insubdination nini hata ukikosana na Manager nje unafutwa kazi.

Mambo ya matatu, matatu imesaidia sana kuhusu transport hapa Kenya, lakini wafanyaji kazi wa matatu driver wanatumika kama Slave Trade, maana ake mwenye gari anataka apelike pesa, na hajui hiyo pesa inatoka wapi, sasa mimi nataka hii Katiba mpya aangalie watu wa matatu watawekwa upande gani. Sana sana mimi nataka kwa maana wale pia wamekuwa employed kama watu wanafanya kwa transport ingine, wawe wanakatiwa NSSF, wawe wanakatiwa kila kitu, heri badala ya kuacha kazi wawe kama wafanyaji kazi wengine, sio eti wazee na vijana wawe kama watumishi wa watu.

Ingine inahusu huyu Mbunge wetu, atapeleka hii hata kabla hujampeleka. Mwaka sitini na tatu wakati tulipata uhuru, tulikuwa na wa Bunge wachache huko Bungeni ikawa column iliwekwa watu 30, mpaka dakika hii wanatuabisha sana, wanaweka pale kiwaja tumewatuma kwa hall kama vile tumejaa na hawapo, na there are over 200, na hata wametuabisha kwa maana there are not debating, sasa wanasema column ni 30 people lakini there don't go there, na huku wana draw a very big challenge it is a shame, to the contributors ambapo ni Wananchi wa Kenya, so my MP I respect you very much because naona jina lako kila siku nikisoma gazeti you are there, lakini tell wale Ministers we don't need them, because wanakula mshahara yetu bure, this is tax payers money.

**Com Paul:** Tupatie Maoni tafadhali

.

**Mr Samuel:** Ya mwisho ni mshahara ya Councillors, wajua wa Councillors wamekuwa wezi sana, na wamekuwa wezi kwa shida moja, shida ni allowance yao saa ingine imechelewa kwa ajili ile refenue haipatikani kwa rahisi, sasa kwa hivyo ni ngeomba hii Tume mpya mshahara ya wale watu itoke kwa tressary heri mtu akiingia hapo aende kama mtu ameenda kufanya kazi sio mwizi tena, maana ake anapigwa kura na influence watu, lakini kule baada ya mwaka moja amekuwa tajiri.

Yangu ya mwisho ni power ya President, mimi ningeomba hivi, Parastal Heads, Judiciary na watu wote, wawe vetted na Parliament mwanzo. Wale wajumbe baada ya kuandika barua hii barua iende kwa Clerk to the National Assembly, halafu awe vetted na Parliament kisha ndio majina itumwe kwa President, heri achague walewatu anawapenda, maana ake tumeona mara nyingi kama vibanda hii mnalia hapa it has come wameprepare kwa ajili ya wrong appointments. People who are not qualified wamekuwa chairman, wamekuwa Managing Directors mpaka hata Posta imesorota. Asanteni sana.

**Com Paul:** Asante kwa maoni yako, jiandikishe hapo tafadhali, halafu nitamuita Muhammed Abdul, Muhammed yuko, Muhammed yuko, Muhammed Bashuara, Muhammed Bashuara, tafadhali tumia dakika mbili tu uguzie yale muhimu.

**Muhammed Bashuara**: Niongezee ya tatu maana ake mambo yangu ni matatu tu nayo ni mafupi mafupi sana, Asalamu waleykumu.

**Wananchi :** Waleykumu salamu

**Com Salome:** Sema jina lako.

**Muhammed Bashuara:** Jina langu ni Muhammed Bue Bashuara, na sina mengi yangu sana ya kusema ni matatu paeke yake, langu la kwanza hasa kuhusu Katiba, ningependelea Katiba ya Kenya, inapomalizwa, lakini iwe ni mfumo wa elimu wa watoto kutoka darasa la kwanza mpaka kufikia darasa la mwisho, na nikishangia kwa sababu, ni kwamba Katiba inasema (inaudible) na Mwananchi wa kawainda wa Kenya hajui chochote kile, natunyanyazwa sana na mambo hayo ya Katiba kama vile hivi leo tunavyozungumza hapa, tuanapata ardhi ya ulongo na ni ardhi yako na unanyanyaswa nayo tena. Juu huna kibali na Katiba ya Kenya huijui Mwananchi, kwa hivyo mimi naonelea ifundushwe dani ya skuli kama kawaida ya masomo mengine yale yote ya Kenya.

Ningependelea ardhi igawanywe kwa muafrika mwenyewe halisi ambaye kwamba ako na asili ya mahali alipotoka, tusikae tu kikoloni kutoka tulipoanza wakoloni mpaka hivi leo tuko chini ya ukoloni wakiarab, wakizungu na wakimatajiri na wakibebebari kama sisi hapa tulipo hapa afrika, tunanyanganya tena wafrika wenzetu, kwa hivyo jambo hili, katika Katiba ya Kenya itiliwe mkazo kwamba Mwananchi ambaye atapata ardhi , agawanyiwe na Wananchi wenyewe hasa wanaohusika katika makao au katika eneo hilo wanaloishi. Iandikishwe ama apewe Title Deed yakena hasa sehemu ambazo hazina title deeds watu wapewe titile deeds zao wanapo gawanyiwa mashamba yao kwa njia ya haki na ya ukweli.

Nikimalizia sehemu yangu ya tatu, nitazungumzia kuhusu uislamu, nigependelea katika Katiba ya Kenya, isibadilishe tabia na mila na desturi za kislamu, kutokana na office ya Chief Kadhi, kuwe na mgawanyiko au na mpangilio kutoka juu ya kwa office ya Chief Kadhi mkuu wa Kenya itelemka kila sehemu mpaka wilaya, na watu hawa pia, walipwe malipo kulingana na sheria za kikadhi ama za kislamu kwasababu yeye ni mwisl;amu lakini mambo anayofanya ni ya sheria za hapa nchini kwetu Kenya kwa hivyo huyu mtu anastahili naye kupata chochote kutokana na uongozi wake ama na umutumishi wake wa umma anaotumikia Waislamu. Pia Katiba hii ibakishe haki ya muislamu hasa kuhusu kama mwanamke, mwanamke ni mtawala wa mwanamume kulingana na sheria za kislamu. Kwa hivyo Katiba ya Kenya iweke wazi kwamba muislamu ana Katiba yake maalumu ambayo inatoka katika kitabu tukufu cha Koran ambayo ana haki kuhusu uridhi, na ndoa na tarakakwa hivyo napenda sana kuchangia jambo hili la Waislamu saidi kwamba Katiba iangalie sana masilahi ya Waislamu hapa Nchini Kenya. **(in venacular)**

**Com Paul:** Asante sana Muhammed Bashua, jiandikishe hapo tafadhali, nitawauliza akina mama wawili, watatu hivi, lakini kabla ya hapo, nitamuita Abubakra ni takupatia nafasi kwa maanake ulikuwa unataka kwenda kumuona Daktari, lakini tafadhari dakika nitakupatia ni mbili tu, kama una memorandum utuachie tusome, halafu uguzie yale muhimu.

**Interjection inaudible.**

**Abubakra Awali : ( in venacular**) Kwa majina naitwa Abubakra Awali, na maoni yangu ni kama yafuatavyo, ningependelea na system ya Government ifuatayo, tuwe na National Parliament na pia tuwe na Jimbo Parliament, kwenye National Parliament, yule atakayepigania uRaisi , awe atakuwa ki Katiba amewajibika kutangaza Mawaziri wake ambao atakuwa nao kwenye Serikali yake peke yake wakati wa campaign, halafu naibu wa Waziri watateuliwa katika wale waBunge kulingana na Political Consideration, isiwe waziri amewekwa kwasababu ya kisiasa, iwe ni kwasababu ya kuendesha nchi kikamilivu, mkubwa wa Jimbo pia naye atateuliwa na ile jimbo ambayo inahusika nawe ataisomea, na wale ma Councillor wote watakaa pamoja waunde sheria za jimbo lao katika mambo Fulani, na mambo Fulani yataendeshwa na Serikali kuu, Serikali kuu itahusika tu na mambo ya foreign policy, military policy, na physical policies na Nation budget, mengine yaachiwe Serikali za Mkoa. Mali yanayopatikana katika mikoa, Yawe yatashikwa na mikoa ile ila tu 30% zipelekwe kwa Serikali kuu ambayo itaendeshwa mambo ya nchi nzima.

Kwa upande wa Mwananchi wa Kenya, Mwananchi wa Kenya iwe ni wakusaliwa, hata kama Mwananchi ule amezaliwa na mgeni maadamu amezaliwa katika Nchi ya Kenya, awe ni Mkenya. Na Mkenya akiwa amesafiri na amezaa mtoto nje ya Kenya lakini maadamu ule mzee ni Mkenya, basi mtoto ule pia awe Mkenya. Pia dual citizenship ikubalike katika sheria. Na ikiwa kuna mgeni ambaye amekaa Kenya kwa muda wa miaka mitano na amejulikana mambo yake ni ya kisawasawa, basi jimbo liweze kurecommend kwamba Mwananchi yule apewe uraia wa Kenya.

Jambo lingine, ningependa kusema kwa kifungo cha Sheria ambayo kianaitwa right to recall, kwamba mfanyi kazi wa Serikali yoyote au mtu ambaye anayechaguliwa akiwa ni Mbunge ma ni Councillor awe ataitwa arudi kwa Raia ikiwa amefanya makosa, na kiti chake kichukuliwe na kipigiwa kura mara ingine. Indipendent Candidates wakubalike, kwa sababu Wananchi wanapata taabu wanaona vyama vingi haviendi kimivumo ya kiphilosophia mbali ni mivumo ya kijambazi. Kuwe na kifungo cha sheria kinachosema katika Katiba zote mbili, iwe ya jimbo ama iwe ni ya Serikali kuu, kwamba kusiwe na sheria ambayo itakwenda zidi na imani na matumaini ya Mwananchi yoyote, yani Mwananchi asilazimizwe, kufuata jambo ambayo ni kinyume na dini yake ama ni kinyume na utamaduni wake.

Jambo jingine ni ardhi, ardhi imepigiwa kelele sana, ningeomba kuwe na sheria maalumu, kwamba ardhi zote ambazo zimetoka kwa unyanganyivu, zirudi katika mikono ya Serikali, Serikali ya majimbo iwe na sehemu yake na Serikali kuu iwe na sehemu yake. Kasha kupangwe sheria kupitia kwa Serikali za majimbo, na Serikali za nchi kuu iangalie ardhi ile itatumika namna gani kwa masilaha ya Wananchi wanaohusika na area zile. Jambo jingine ni Kadhis Court, napendekeza kwamba juridicing yake iongezwe iwe kuanzia low court, high court, mpaka court of appeal kufuatia sheria za kislamu, isiwe mtu ameenda kwa kadhi na

ameona hakuridhika anakwenda high court ambayo haihukumu kislamu, inakuwa ile ni ku undermine the institution of Islamic affairs. Kwa hivo mambo yote ya kislamu yapitie kwa kadhi kutoka nyaja ya chini mpaka ya juu.

**Interjection Inaudible.**

**Mr Abubakra**: Parliament, iwe itakuwa na time table yake maalumu, both, Jimbo Parliament na Nation Parliament, isiwe tarehe ya election itakuwa lini, Bunge ikianza tu inajulikana tarehe Fulani kula sitakuweko, na ikiwa Bunge litavujwa mapema basi kuwe na masala muhimu, kuna crisis katika policies, vyama za kisiasa vinasosana, mpaka kwamba Serikali haiwezi kuendelea basi ifunjwe. Sio eti ule ako kwa utawala anaweza fuja sasa nikiita kula naweza kushida.

Jambo jingine, tumepitia historia ya kutokuwa na uaminivu na Serikali yetu, Commissioners nyingi sana zimechaguliwa, lakini mapendekezo yake hayakusikika wala haijulikani, ningeomba kwamba tunaimani, ijapokuwa si kubwa kwamba Commission hii itamaliza kazi yake na Katiba mpya itapatikana, na ndani hii mpya kuwe kuna kifungo maalumu kwamba all Commissioners, ziliopita nyuma kuanzia uhuru mpaka sasa, mapendekezo yake yote yarudishwe na yasomwe na Wananchi , na kila jimbo ambalo la husika na jambo kama lile lichukue hatua kulingana na jimbo lake na kulingana na Serikali , ndipo tupate kujua dhambi zote zilifanywa na waliopita, siwe sitahukumiwa Kisheria.

Mwanadamu hawezi kuwa juu ya sheria lazima awe under the law, ikiwa ni President ikiwa ni Prime Minister, ikiwa ni Mayor wa Jimbo akifanya makosa anachukuliwa hatua immediately, wakati pale pale yuko kwenye wadhifa. Ombi langu la mwisho, na this is my observation Commissioners, mtaona kwamba ndugu zetu wengi wamekuja hapa wamelalamika badala ya kutoa proposals, this is to say that civic education haikufanywa kisawasawa, mimi nawaomba sasa yale malalamiko yale watu wameitoa, based on that muform Constitution matters (inaudible) asanteni sana.

**Com Paul:** Asante sana tumesikia yako tafadhali jiandikishe hapa, sasa tutamuita, naona hapa kuna jina tulikuwa tumelitaja lakini wewe hukujibu maanake tulikuita, je na kama Omar S Yahi ni wewe, tafadhali jina lako halionekani pahali popote hapa nalitafuta, lakini tutakupatia nafasi.ngoja kidogo hapa, nilisema nitamuita mama kwanza, jina lako haliko asubuhi, lakini nitakupatia nafasi, maana ake nimekuona tangu asubuhi.
**Speaker:** ee nimeregister.

**Com Paul:** ee kweli, Riziki Hamisi yuko, Riziki, mama kuja hapa uzungumze.

**Riziki Hamisi**: Hamjambo akina mama na akina baba, mimi kwa jina naitwa Riziki Hamisi, mimi katika vile Katiba ambapo nilikuwa nikitaka kidogo igeuzwe, ilikuwa katika Kadhi wa kislamu achaguliwe na waislamu wenyewe, tena awe ajua sheria zile za kislamu na asome elimu ya kislamu na elimu ya sheria. Tena basi tuwe na koti ya rufani ya kislamu ambapo maswala yote yatashidwa, muislamu yule yule akate rufani katika koti ya kislamu ikiwa swala ni la kislamu.

Halafu tulikuwa tunataka tuwe na mwanamke, ambaye atakuwa na meza yake ya kislamu, ambaye mama yule ikiwa mimi kama mama nina kasoro na mume wangu nisiende moja kwa moja mpaka kwa mwanamume nikamuelezee yale matatizo yangu, kwasababu matatizo mengine ni ya ndani. Tena, huyu Rais sipendi awe na vyeo chungu nzima yeye awe ni amri mkuu wa jeshi, ama ni nani ama nani yani vyeo chungu nzima anavyo yeye, awe atapunguziwa mamlaka ya vyeo. Akina mama wapewe nafasi ya Mbunge maalumu katika Bunge ama achaguliwe

**Com Paul:** Tupatie mama nafasi tafadhali, kuna kelele nyingi hapo,

**Ms Riziki:** Awe achaguliwe Councillor maalumu wapewe nafasi akina mama, achaguliwe Mbunge maalumu ama Councillor maalumu. Jambo jingine nikuhusiana na watoto, kuna pesa ambazo pengine huwa za tengewa watoto, kama bursary hivi, ambazo huwa zaingia mahali ambazo hasitahili, kwa mfano tuliambiwa kuna pesa zilikuja ziko Mombasa zilipewa Councillor ambaye atasimamia Busary ya watoto ama mambo ya elimu, sasa hizi pesa hazifikii yule mama mnyonge na atashidwa kusomesha watoto yake, kwa maoni yangu mimi ilikuwa napendelea Serikali iweke kiwango Fulani cha katwa kuwekewa mtoto ule ako tumboni, mpaka atakapozaliwa, mpaka atakapofikia umri ya kwenda skuli. Hiyo ndiyo nilikuwa nayo. Asanteni sana.

**Com Paul:** Asante sana mama jiandikishe hapo tafadhali sasa nitampatia nafasi Omari Salimini, kwanini hata jina lako limeandikwa,

**Omari Salimini:** Ndio hiyo taabu hiyo sasa twa taka majimbo kwasababu ya taabu hiyo.

**Com Paul:** Endelea, na unatoa maoni kama individual, pia kisha kama mwakilishi wa Baraza la maimamu kwa upande huu, nitakupatia dakika tatu kwasababu umekaa dakika tatu

**Omari Salimini: (in venacular)** Twamshukuru mwenyezi mungu kwa kupata fursa hii ya leo, mimi maoni yangu yalikuwa kwanza nizingumzie habari ya Kadhis court, akina mama wamejaribu vyakutosha kwa sababu ni uwanda wangu upande huu, ma Commissioners nawaombea mungu awabariki muweko katika hii kazi.

**Com Paul:** Kidogo kidogo ebu tafadhali Bwana Omari, wale ambao wako na simu za mikono tafadhali simeni, there are interfering with the recording of this hearing. Endelea mzee.

**Mr Omari:** Ma Commissioners nawaombea mungu awabariki kwa uvumilivu moja mnaopata, kwasababu natoa hekaya moja iliotokea kakamega, mama mmoja alitoa maoni yake kuhusu haki za kibinadamu na hakuisoma hii Katiba, maana neno Katiba ni baina ya mtawala na mtawaliwa, ndio ni mkataba wa baina anayetawala na aliyetawaliwa, yule mama Commissioners, mimi

maoni yangu, wale kuku ambao nawafuga sitaki Chief wala mzee waje wanichukulie hiyo ndio Katiba yangu. Kumbe katika Katiba kuna act cap 1974 ya kumlinda mtu mali yake na hakuisoma wala hajui, so more civic education yatakikana yalemishwa raia.

Sasa naja katika maoni kuhusu office ya Chief Kadhi nataka kuifafanua kwa upana, Chief Kadhis office, hivi sasa inavyokuwa ama ilivyo, sivyo vile ambavyo sasa twatoa maoni, kama Council of Imaam na wahubiri, twataka Kadhis Office iwe kama makoti mengine, waheshimiwa Commissioners ndugu zangu, kwanza kuanzia surbodinate courts, zile ngazi cha chini wawe watu wanahukumiwa kupitia kitabu cha mwenyezi mungu ambayo ni Koran Karim na hadithi za Bwana mtume muhammed, kisha kuna court ya appeal, iwe ni ya kislamu. Sio leo case za waislamu zatoka kwa Kadhi wamezidikana kuelewana kesho wanarudi katika secrularism hatuwezi kwenda huko, kwasababu kitabu chetu kimekamilika, isalamu is the way of  the life.

Tukija katika akina mama, tukienda katika ma Court hivi sasa utachangaa, hakuna nafasi ya mama zetu kukaa kama vile court zingine tunasiona za secrularism ama court zingine za ki Serikali, utulie anapohukumiwa, anapata taabu pengine ni mja mzito, tunataka zile facilities ziwafikirie na wao kama wale wengine. Kisha kuwe na uhuru waweze kuwa na mkalimani baina ya mama mke ambao wamesoma, tunao wengi wamesoma.  Tuje katika qualification, mama yule ameelimika, akiwa ameelimika, kitabu chetu kinatuambia baina ya mke na mume ni kutangamana ni fitina, kwa hivyo ni lazima kuna siri zingine. Hata wakati mtume na masaaba, ilikuwa Bwana Mtume katika sera yake hata kuoa wake aliopewa na mungu amri, ni kwasababu mambo mengine wanawake kwa wanawake wazungumza na yeye. Kwa hivyo hii tunataka muiandike na iwepo, ili wapate kuwambiana yale shida zao walizo nazo. Baina ya mama na baba huwa mambo mengine hufichana, amasivyo ndugu zangu?

Qualification ya Chief Kadhi, kwanza twataka awe na elimu ya Islamic sheria, kisha awe na (inaudible) ya kidunia, awe ni msoevu katika makazi yake ya ukadhi na awe na usoevu ya uwakiri Lawyer, kisha awe na experience, ya miaka aliofanyia kazi kuzunguka mikoa yote minane, tena wachaguliwe na muslimu scholars waliohittimu kisawasawa katika Magistrate zura. Wakicha fanya hivo sasa ndio hao makadhi hao wengine, nao wanakwenda sababa kulingana na amri ya chief kadhi alivyo chaguliwa, na umri tunaotaka ni kuanzia 35, mimi nishapata niko 38, kwa huyo Mtume alipopewa utume alikuwa na miaka 40, kwasababu bongo limekomaa, utotoni hayuko, na ubarobaroni hayuko.

Tukija upande wa women state, tunataka akina mama pia wawe na majela yao kama vile leo watu wanavyo jela, siwe na heshima jela zile ikiwa katika hukumu za kuhukumiana na wawe  watu wanaangalio kiutamaduni ya vile walivyo.  Upande wa mapolisi wawe na polisi wao kwasababu leo akina mama wachukiwa na mapolisi ya wakina baba.  Sasa hii system itakuwa imechunga amani, ule uharibifu, sasa twasikia tuna ma case ngapi za rape, polisi mume akiamua atafanya vile atakavyo, lakini akiwa ni polisi mke kwa mke hakuna raping. Bwana Commissioner asante kwa nipa muda saidi, natural resource naja nakatakata, mambo yangu yalikuwa tangu asubuhi

**Com Paul:** Nimeongezea tu dakika ingine moja.

**Mr Omari:** Natural resource, kwanza hapo klitajwa kuhusu upande wa elimu sisi tumefanya utafiti, mimi nimmoja aliyekwenda Mombasa Polytecnic, mimi najiita jina la zamani Miyome, maanake ni Muslim education Muslim Instition of welfare, ile ijegwa na dururu kuanzia msingi wa ardhi mpaka kusimamam dururu wa islamu wenyewe. Leo kwa hivi sasa wako wanafunzi 6500, 500 peke yake ndio wa Pwani, sio waislamu wa Pwani, ninayo research naweza kukuletea, 500 why twataka kujua. Tuje katika Chanzo Teachers College waliochukuliwa Pwani nzima ni 774 more than 8000 Kenya mzima na yenyewe resource yenyewe iko hapa.

Maoni yangu kisiasa kama mwenyewe ninavyotaka kuzungumza, Mbunge lazima tukimuandika kazi tuandikiane mkataba, tumemtaja hapa na nilikuwa aweko asikie, wamekuwa na malaki wanaopata hapa, Mbunge yule tutampa kazi, tuandikiana mkataba mambo hayo moja kwa moja na utie sahihi ya kwamba utaweza kufanya hayo mambo, twakupeleka Mbunge, ukikataa hapa hapa hatukupe kazi tunakufuta kazi. Na Diwani vile vile

Angalia vile jaa imejaa hapa, na leo ni maradhi yametuenea, Barabara haipitiki, kazi hazifanyiki, matinga tinga hakuna, why twa taka kujua, ndio twandikiane maktaba hapa.

**Com Paul:** Sasa ile dakika moja imeisha.

**Mr Omwari:** Basi nipe nusu dakika nimalize, maanake nimekaa nionee imani ndugu yangu, sasa maoni yangu, Mbunge na Councillor waandikwe mkataba hakuna tena ile horera. Kisha hayo yote yamalizikia katika Majimbo system. Lakini nataka historia moja 1885 mkutano uliokuwa Berlin, wazungu walikaa chini kuigawanya Africa, Kenya haikuwa inajulikana Kenya, imejulikana Kenya baada ya 1920 ndio ikajulikana Kenya Tanzania Uganda, lakini kuanzia nyuma 1885 wazungu walikaa chini German, akasema tuwezeje kuichukua Africa wakaigawanya vipande vipande, ndio hii mipaka iliyo tuko nayo. Kenya boundary Tanzania boundary hakaweza kuweka total zao, wakatunyonya kiasi cha kutunyonya, Kenyatta alipoingia katika ufalme wake kama Raisi, aligeuka ile mikataba akaja akatia mambo yake ndio leo tuko na taabu namna hii, kwa hivo tuanataka tena yale majimbo yetu yarudi kama zamani

**Com Paul:** Sasa Mzee (inaudible)

**Mr Omwari**: Salamu waleikumu

**Com Paul:** Asante sana kwa maoni yako Bwana Salimini, sasa tutamuita mama mmoja kama Bibi Saidi, aje hapa na kuna huyu Abannus Kioko yuko, na wewe nikama ulitoa maoni huko Shangamwe.

**Interjection inaudible**:

**Com Paul:** upatie mama nafasi aongee atoe maoni yake.

**Hamisi Saidi:** Mimi nilikuwa na shukuru sana kuhusu haya majimbo.

**Com Salome**: Sema jina lako

**Hamisi Saidi:** Jina langu mwana Hamisi Saidi, natoka Michomoroni, sasa wakina mama wananyanyaswa sana, jambo la kwanza wakifanya biashara, watoto hawana fees za skuli, wakifanya biashara wanaambiwa kwanini unafanya biashara na wao hufukuzwa, kwa hivyo wazee mnao toka juu muangalie wakina mama wananyanganywa sana, na wengine mababa zao walikufa, sina mengi.

**Com Paul:** Lakini mama jina hili ni lako kweli

**Ms Hamisi**: Ni langu nimeandika,

**Com Paul**: Na mimi naona miaka 27 kweli

**Ms Hamisi:** Walioandika wameandika kimakosa.

**Com Paul:** Na unatoka shirika linaitwa jana si leo

**Ms Hamisi:** Walio andika wameandika kimakosa.

**Com Paul**: Hapo mama kunaonekan kumetokea makosa kidogo lakini tutajaribu tuandike jina lako pahali kwa maana tumeyapokea maoni yako na yameingia kwa ukada tayari, ujiandikishe hapo, sasa tutamuita Tesa Omar,

**Speaker:** Bona mmetusahau, unaitana tu na bona hutuiti?

**Com Paul:** Sijawasahau, hata sasa wale nawaita wako nyuma kidogo, najaribu kurekebisha kidogo maana majina yenu yameandikwa huko nyuma nyuma na nitajaribu kuwaita. Tesa Omari Yuko, kuna mwingine anayeitwa Nassir Zam Zam, three minutes.

**Muhammed Zam Zam:** Jina langu naitwa Muhammed Zam Zam, nataka kuzungumzia mambo ya house without land, sijawahi kuona nyumba ambayo haina ardhi, labda imejegwa baharin, wenzangu wamezungumzia (inaudible) lakini nataka kuzungumzia act 295, ningependelea iwe abolished kabisa, kwa vile ndiyo nuisance katika Kisauni, wengi hawa wanao levi distress

hawapitii katika mahakama wanapitia through Lawyers and auctioneers.

**(inaudible)** …ni vile vile, diwani ni vile vile. Diwani akija hapa hakuna kutanga, angalia njaa lilivyojaa hapo. Lo! Nini maradhi yametuenea, barabara haipitiki. Kazi hazifanyiki, matingatinga hakuna, why? Twataka kujua, twamwandika kazi kwa mkataba, twaandikiana naye. Twaandikiana, si mmesikia mmesema je hapa, wakuta malaki mangapi? Majuzi 150 walikuwa Whitesands hapa, walikuwa Whitesands. Mimi nina homa nawaangalia kwa runinga, wako Whitesands hapo, mmoja akiwa hapo, akina nani? Akina Orengo kina nani wako hapo. Sisi baraza la Maimamu kila utafiti, hatuja hatulali, usiku na mchana. Pia Moi anajua. Sasa, twataka hii ki ngo…

**Com. Wambua:** Sasa, pengine dakika moja imeisha.

**Speaker:** Ngoja kwanza. Nipe tena nusu dakika nimalize maanake nimekaa nionee imani ndugu yangu.

**Com. Wambua:** Basi maliza.

**Speaker:** Haya asante, haya. Sasa hiyo maoni yangu kwa mimi kama hivyo Mbunge na Councillor waandikwe mkataba ndugu zangu nawaambia. Hakuna tena ile holela, mkataba, ni kama mkataba ule tunaopika wajua wa kuhusu ki kuchukua ardhi na hii vilevile mkataba. Kisha nitamalizia la mwisho. Na diwani pia vilevile tumwandikie mkataba tumemaliza kisha tumesema hayo yote yamalizikia katika Majimbo system na hayo yote yamalizikia katika Majimbo system. Sasa nitaka kuwapa historia moja, 1885 mkutano uliokuwa Bahrnin, nawapa historia kidogo. Mkutano ulikuwa Bahrnin, walikaa chini wazungu, waingereza na kila mahala kuigawanya Afrika. Kenya ilikuwa haijulikani Kenya, nawapa historia. Kenya imejulikana Kenya baada ya 1920, ndio ikajulikana Kenya, Tanzania, Uganda. Lakini kuanzia nyuma 1885, wazungu walikaa chini mkutano wa Bahrnin ndani ya chama wakasema tuwezeje kuichukua Afrika? Wakaigawanya vipande vipande. Ndio hii mipaka ndio tuko nayo, Kenya border hii, ndiyo ya Tanzania border hii, Afrika nzima. Wakaweza kuchukua vipande wakaweza kuweka title deed zao, wakatunyonya kiasi cha kutunyonya. Kenyatta alipoingia katika ufalme wake au kama Rais, aliigeuka ile mikataba, akaja akatia mambo yake ndio leo tuko wastaabu namna hii. Kwa hivyo twataka tena yale Majimbo yetu yarudi kama pale…

**Com. Wambua:** Mzee,--------------------(inaudible) kwa hivyo---------(inaudible) utanisadiki hapo…

**Speaker:** Salaam Aleikum.

**Com. Wambua:** Asante sana kwa maoni yako Bwana Salimin na sasa tutamuita mama mmoja hivi, kama huyu Binti Saidi, yuko? Binti Saidi yuko? Binti Saidi?

**Speaker:** Binti yuko wapi?

**Com. Wambua:** Aje hapa. Na huyu Urbanus Kioko, Urbanus Kioko? Na wewe ni kama ulitoa maoni ooh, Changamwe?

**Binti Saidi:** Wakina mama na wakina baba salaam aleikum?

**Wote:** Aleikum salaam.

**Com. Wambua:** Tumpatie mama nafasi aongee, atoe maoni yake.

**Binti Saidi:** Mimi, nilikuwa nashukuru sana kuhusu haya majibu. Jina langu Mwana Hamisi Saidi, natoka Mishomoroni. Sasa wakina mama wanyanyaswa sana. Jambo la kwanza wakifanya biashara, vatoto hawana fees za skuli, vakifanya biashara vaambiwa kwa nini mwafanya biashara. Maan…kuto wakuza akina mama. Kwa hivyo, wazee mnaotoka huko juu muwaangalie wakina mama, vanyanyaswa sana mabarabarani. Vatoto hawana karo za fee, vatoto hawana uniform, twapata taabu sana si tukifanya biashara. Vengine hawana wakina baba wamekufa, kwa hivyo sina langu. Sina zaidi, zaidi ni hilo, twanyanyaswa sana.

**Com. Wambua:** Lakini mama, hizo ni zako kweli?

**Binti Saidi:** Ni langu nimeandika.

**Com. Wambua:** Umekua nazo miaka ishirini na saba, kweli? Basi, walioandika waliandika vibaya, waliandika kimakosa.

**Binti Saidi:** Walioandika wameandika kimakosa.

**Com. Wambua:** Mmmh?

**Binti Saidi:** Eeeeh.

**Com. Wambua:** Na ulikuwa umetuahidi-------(inaudible) jana si leo? Si ndiyo?

**Binti Saidi:** Aa aah.

**Com. Wambua:** Haya basi, nafikiria………(inaudible). Mimi naona mama hapo kumetokea makosa kidogo lakini tutajaribu tuandike jina lako pahali maanake tumeyapokea maoni yako na yameingia kwa official diary. Kwa hivyo jiandikishe hapo. Sasa tutamuita Pesa Omar.

**Speaker:** Mbona wakina mama umewasahau?

**Com. Wambua:** Sijasahau, hata sasa wale ninaita nawako wako nyuma najaribu kurekebisha kidogo maanake majina yenu yameandikwa huko nyuma nyuma lakini nitaendelea kuwaita tu. Pesa Omari yuko? Haya yuko. Kuna mwingine anaitwa Najib Shamfa, yuko wapi? Haya, three minutes Bwana.

**Najib Mohammed Shamsan:** Jina langu Najib Mohammed Shamsan.

**Speaker:** Sauti kidogo.

**Najib:** Jina, Najib Mohammed Shamsan. Aah, nataka kuzungumzia mambo ya house without land. Sijawahi kuona nyumba ambayo haina ardhi, labda imejengwa baharini. At the moment, wenzangu wamezungumzia mambo ya ground rent. But mimi nataka kuzungumzia zaidi kuhusu hii distress of rent Act number 295. Act hino ningependelea iwe abolished kabisa kwa vile ndiyo news nest katika Kisauni. Wengi hawa wanaolevy distress hawapitii kupita mahakama. Wanapitia through their lawyers and auctioneers, which is very wrong. Maanake wale ambao wadaiwa kwa njia ambayo si ya halali hawapewi nafasi wakasikilizwa. Kwa hivyo Act hino ambayo ni 293, ningependelea sana iondolewe katika katiba yetu kabisa.
Ma-auctioneers wamepewa power nyingi sana ya kuuza vitu na thamani value wanaiweka wao wenyewe. Itakuwaje nyama umpe fisi ajihukumu kama yeye fisi mwenyewe atakula nini mbeleni? Kwa hivyo ningependelea anything of sheria anayoifanya lazima iwe valued by independent valuer, registered one ambaye both parties anayedaiwa anayedai watakubaliana na hiyo value na ikiwa value hazijalingana, waende kortini kwa kusikilizwa kuhusu valuation.
Watu wamezungumzia kuhusu price control. Ningependelea Price Control Act irudishwe sababu unyanyasaji wa chakula umezidi kuendelea. Hivi juzi tu, gram za mkate zimepunguzwa lakini bei imebakia pale pale. So, ingewezekana Price Control Act irudi vyakula vicontroliwe na ikiwezekana the government should subsidize atleast 60% ya chakula ya mwananchi because mnaposema haki ya mwananchi ni basic need ambayo ni vungu, mnatarajia chakula kitoke wapi kama wakati watu hawana kazi? So, serikali yenyewe ifanye bidii, itoe 60% ilipe mafactory ya chakula wananchi watoe 40% ya tofauti. Otherwise, the name basic need ya mwananchi haijaingia kwa katiba yetu. Mpaka iwe ya 60% ya chakula.

Kuhusu councilors – Councillors, we could prefer mambo ya miaka mitano is too much for them. Wanakwenda council, wanakaa five years they are doing nothing. Tungependelea waweze kupewa miaka mitatu peke yake, three years is enough. From after three years tuwaangalie tena wanaweza kuendelea ama sivyo tuwang'oe. So, electorally tuwapige kura after every three years. Mayor to be elected by Wananchi themselves.

Kuhusu disabled, walemavu – Bwana Commissioner, hii classroom tuliyokaa leo ni ya walemavu. Iangalie hali yake ilivyo, look at it. Ma-desk haya ni ya kuomba, haina umeme. Walemavu hawa kutoka wazaliwe hasa hawa wa mental disturbance,

mentally wa kichwa, kutokea wazaliwe mpaka kifo chao wanatumia madawa. Wazazi wao ni masikini, serikali haiwaangalii kwa namna yoyote ile walemavu hawa wa kichwa. Serikali haijui kama hawa walemavu wanaishi na sisi. Tutaishi na hawa watu wa namna gani kama hawawezi kusaidiwa? So, the government should, must waambiwe kwamba ni lazima wawapatie madawa ya bure walemavu hawa. Neno lazima liwe litatumiwa pale sababu hawana njia nyingine.

Kuhusu walemavu wale wanaotumia magari kama hizi za nonino, wakipanda basi kwenda Nairobi ama transportation yoyote wanalipa tikiti mara mbili kuliko sisi wenyewe. Analipia gari yake, analipia mwenyewe. Public Service Vehicles zifahamishwe kwamba mlemavu ni haki yake kusafiri kwa hivyo gari zao za ulemavu zisilipishwe hata kidogo. Kuhusu tena walemavu, walemavu maofisi ya serikali zote hawana njia ya kupanda juu kumuona P.C ama D.C. Hawajatengenezewa namna yoyote wao waweze kwenda kuona wale maofisa D.C na P.C otherwise wateremshwe chini na serikali ama sivyo walemavu watengenezewe njia za kwenda juu. Walemavu, watoto wao ndio wanawategemea. Walemavu wenyewe hawana njia ya kufanya kazi mbili. Kwa hivyo ningependa watoto wa walemavu wapewe bursaries kutoka Ministry of Education waweze kuelimika. Walemavu, ikiwa watapewa madawa ya bure hawa wa kichwa na hawa ambao wana ulemavu wa aina nyingine yeyote, waweze ku-cost only 50% katika mahospitali.

Kuhusu Police Cells – Hizi police zetu saa hii mkiziangalia Nyanyani, Bamburi na kwingineko, ni polisi ambayo binadamu hafai kuingizwa ndani. Kuna dirisha size ya exercise book kule juu. Je, mimi ambaye sina makosa tayari ninahukumiwa ninawekwa cell, korti inaponipata mimi tayari sina makosa, je, yule polisi aliyenitia cell nina njia ya kumuadhibu? Kwa hivyo ningeomba, we should not be charged unless found guilty. Going to cells tayari ni njia ni ishara kwamba mimi tayari ninakosa. Kwa hivyo, what we would prefer is, “not guilty, until found guilty”. Kwa hivyo mapolisi wetu wafahamishwe kwamba torturing is a crime, wakiwa mtu amepigwa polisi anafaa kushtakiwa. Kwa hivyo torturing is not a way of getting information from somebody. Torturing should be treated as a crime.

On top of that, ningeomba tena ma-Commissioners, mimi ikiwa ni mwakilishi wa Kisauni Constitution Committee kama vile Bwana Mesad alivyozungumza, kama mtakuwa na nafasi mje mara ya pili. Wananchi wanalalamika kwamba hawawezi kupata nafasi, nawaombeni. Asante.

**Com. Wambua:** Kabla hatujawaita akina mama tena, nitampa nafasi one minute, Maurice, dakika moja tu halafu, one minute nasema one minute.

**Speaker:** Mimi naitwa…

**Com. Wambua:** Akina mama mambo yenu sasa itashughulikiwa tafadhali. Mpatieni nafasi.

**Maurice Amakoya Stevenson:** Okay, mimi naitwa Maurice Amakoya Stevenson na haswa nitazungumzia mfumo wa serikali

ambayo ningependa tuwe nayo na uwekwe katika Katiba mpya.

**Speaker:** Ongeza sauti.

**Maurice:** Okay, my name is Maurice Amakoya Stevenson and I am going to talk specifically about system of government. I wish to propose as follows that Kenya should have a Parliamentary System of government in which the Head of State is separate from the Head of Government.

**Com. Wambua:** Apeye nafasi tafadhali.

**Maurice:** Raisi katika mvumo wa serikali ambaya napendekeza kwa tume ya katiba leo ni kwamba rais pamoja na makamu wake wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. pili, wadhifa wa rais wa jamhuri uwe na msingi wa kuongoza Kenya katika sherehe pengine za kitaifa ama kuweka sahihi mswada baada ya kujadiliwa na bunge na mamlaka makubwa ambayo katiba ya sasa inampa raisi wa jamhuri yanapaswa kupunguzwa; kwa mfano, rais kutangaza hali ya hatari, kuweka sahihi mikataba na nchi bila kupata kibali cha bunge, kuwasamehe watu ambao kuna ushahidi wa dhahiri kwamba wameuwa na mambo kama hayo unapasa kupunguzwa. Tatu, rais wa jamhuri wa Kenya hapaswi kuwa juu ya sheria, the President of the republic of Kenya shold not be above the law kwa sababu hali kama hii inamfanya rais wa jamhuri kukiuka sheria za nchi na hata kukiuka haki za kibinadamu za wakenya vile anavyotaka. Kwa hivyo, ikiwa raisi wa jamhuri kutakuwa na ushahidi wa kuonyesha kwamba ametenda hatia zifuatavyo, kwa mfano kutumia ofisi yake vibaya, kutumia uwezo wake vibaya, kujihusisha katika vitendo vya uhaini na ufisadi, anapaswa kufunguliwa mashtaka na kupatana na hatia aondolewe mamlakani. Nne, ijapokuwa napendekeza hapa kwamba rais wa jamhuri katika mvumo huu, yaani parliamentary system awe na uwezo wa kuteuwa pengine majaji na ma-ofisa wengine wa uma, mabalozi, lakini utozi huo unapaswa kupasishwa na bunge ili kuhakikisha ya kwamba wakenya wanaofaa ndio wanaochaguliwa kuchukua nyathifa hizo. Tano, bunge linapaswa kubaki na mamlaka ambayo liko nayo ya kupiga kura ya kutokuwa na imani na rais. Pia, rais uwezo ambao yuko nao katika katiba ya sasa ya kuweza kuita, kuhairisha na kuvunja bunge uondolewe kutoka kwake. Badala yake, bunge linapaswa kuwa na ratiba yake ya matokeo yake. Sita, ningependa kupendekeza kwa tume ya katiba kwamba uwezo ambao rais yuko nao katika katiba ya sasa ya kukataa kwa mfano kuweka sahihi mswada ambao umejadiliwa na bunge, kwa mfano ile donde bill

**Speaker**:...............................................(inaudible)

**Maurice:** kunapaswa kuwa na kifungu ambacho kitamlazimisha raisi wa jamhuri aweke sahihi kifungu hicho ili iwe sheria. Mwisho, katiba ya Kenya ambayo wakenya wangependa kuwa nayo, iwe na should provide for the post of the leader of opposition na kazi za kiongozi wa upinzani itakuwa ni to keep checks and balances of the government of the day to ensure that there is probity, transparency, accountability, good governance and sound economic management to foster national development. To ensure that there is equitable distribution of natural resources by the government in power, to provide an

alternative government for the people of Kenya when the government of the ruling party looses the legitimacy. Mwisho kabisa, viama vya upinzani vinapaswa kupewa haki zifuatazo za katiba ili viweze kufanya kazi yake vizuri; kwanza wawe na radio yao na television yao ili kuendeleza sera zao. Pili, wawe wanaweza kufanya mikutano ya kisiasa katika sehemu yoyote ya Kenya bila kutatizwa na polisi na kunyanyaswa kwa njia yoyote. Asanteni sana.

**Com. Wambua:** Asante, tupatie memorandum na ujiandikishe pande hio. Sasa tutampatia nafasi....................(inaudible) jina lakini ungojee tu. nitamwita mama mmoja Nuru Said. Huko wapi Nuru, kuja hapa mama tafadhali, chukua muda wa dakika mbili tu utupatie maoni yako halafu tuendele

**Nuru Said:** Hamjambo nyote, mimi Nuru Said natoko Kongoea. Maoni yangu kuhusu kina mama wapewe haki zao. Kina mama sisi twanyanyaswa sana kuhusu pahali popote tunapokwenda kuwa hatuna uwezo wa kuzungumza jambo lolote na kuhusu kama polisi pale, lazima tuwe na meza yetu kina mama. Jambo jingine ni kuhusu hapa pwana; pwani sisi watu wa pwani twanyanyaswa ingawa pwani ni yetu, lakini twanyanyaswa sana. tukitaka kwenda maskuli kama hii polytechnic, mimi nina watoto wangu wengi karibu watatu, tungienda kwenye polytechnic twambia tungojee advertisement. Na wengi sana ni watu wa kutoka juu. Twataka sisi, 90% kutoka hapa pwani wachukuliwe na hilo ilobakia 10% wachukuliwe watu wa kwengine. Na kuhusu port pia, sisi leo watoto wetu wanakaa vikundi vikundi, hakuna watoto wanaokwenda kule port kupata kazi kwa sababu watu wa bara ndio wao wakubwa kule. Watu wa bara ndio wachukuliwe, mtu yuko bara kule atakaa miaka yote, akija akimaliza skuli moja kwa moja yuangia wapi, kazini. Sisi watoto wetu wakaa magarden halafu ambao watoto wa pwani wavivu, watoto wetu hawasomi, hawaendi university. Hawana nafasi university kabisa, pwani hii yetu haina university hata moja na ambayo ni city sasa. Kuna city itakosa university? Kwani watoto wetu hawasomi? Watoto wetu wasoma sana, tena werevu sana lakini sasa kuanzia sasa, mimi maoni yangu nataka watoto wetu, mitihani yao zifanyiwe hapa hapa, zisiende juu. Kwa sababu kule kule juu ndiko wanakoangushwa. Wakija hapa, watoto wetu ambao waseja hawana university. Kuna watoto hawapata grade za A wakienda kule wa pewa business. Mtoto anasoma hapa anapata grade A halafu aende university bara, apewe business tena si kwa kutaka yeye mwenyewe, yeye ataka kama doctor, nini lakini akifika hapa, akifika kule abadilishiwa moja kwa moja. Na hio iko, nishaona hapa hapa ambapo ni mtoto wetu, ni mmoja katika.. Mimi kila ninalozungumza ananipata mimi mwenyewe. Kuhusu COast General, Coast General hapa, watoto wetu wakiandikisha form, wasichana wetu wawe ma-nurse, wakienda kule wabaguliwa, zao zawekwa kando, ishajulikana Mariamu, Fatuma wao, sisi twataka hapa hapa mkoa wetu uwe hapa hapa, majina ya watoto wetu yachaguliwe hapa hapa. Na kuhusu hizi beach, beach hizi zote wafanyikazi wote ni watu wa bara. Wote kwanzia Manager mpaka wa chini, mpake watchmen wa nje mlangoni ni watu kutoka juu. Utakuta Mohamad na Salim wawili. Mimi leo nitazungumza mambo mengi manake yaniumiza roho yangu. Na kuhusu polisi kushika shika watu ovyo ovyo, pia hatutaki

**Com. Wambua**: Tafadhalini tufanye heshima kwa mama, tumpatie nafasi atoe maoni yake

**Nuru Said:** Kuhusu mapolisi, mtu mama kama mimi mtu mzima nikiota, pengine natoka harusini au natoka kwa watoto

wangu, wanisindikiza wanipeleka kwenye matatu, nikishuka nyumbani tu nashikwa. Msako, mama mimi mtu mzima pengine naitwa usiku, mjukuu wangu mgonja, narudi. Au ninasahau kitu dukani naenda nunua, ninashikwa. Nashikwa na msako mtu mzima mimi natafuta nini usiku huu nje hata nishikwa na msako. Hata nikimwambia, we mama wewe huna ID. Nitatokaje na ID mimi saa zote nitembee na ID, ikipotea? Na kuhusu vitambulisho watoto wetu, watoto wakizaliwa wawe na vitambulisho vitatu. Passport, birth na ID card. Hizo vitu vitatu lazima watoto, mimi maoni yangu, mtoto anapozaliwa. Na utakuta sisi wananchi wa hapa hatupati vitambulisho, watoto wetu wanyanyaswa, mtu ana leaving, ana certificate, mimi nina certificate nimemzaa, amesoma kutoka standard one mpaka form four, ambiwa mtoto yule bado si mkenya. Nakuhusu mzazi mmoja, mtu aweza kuzaa, mama aweza kuzaa, pengine baba mwenyewe hayuko au baba mwenyewe ashikanta gwara zake halafu mama akashika mimba. Akizaa yule mtoto anamlea mpaka anakuwa mtu mzima hata kumtolea ID mtoto huwa ni shida, amsumbua bababe; babake yuko wapi? utamptafuta wapi naye ashashika njia alikwenda zake?

**Com. Wambua**: Asante, asante mama

**Nuru Said:** Mimi nina maneno mengi

**Com. Wambua**: Ndio nina ona mambo sasa yamechemka, lakini wacha nikuulize swali mama. Mama unasema mtoto akizaliwa, apatiwe ID, apatiwe birth certificate, apatiwe passport. Mama unajua, passport utapataje mtoto aliye zaliwa jana na ambaye hawezi kuweka sahihi?

**Nuru Said:** Mzazi wake anaweka

**Com. Wambua**: Kweli atawekaje, kwa ID ataweka aje kidole na aweke na sign yake, katoto kaliko zaliwa? Au unataka kumaanisha hivi, mtoto akizaliwa, ndio birth certificate anaweza kupewa kwa maana ni ya baba na mama lakini hivyo vitu vingine akimaliza miaka yake ile kumi na nane, apewe. Lakini kusema akizaliwa apewe hivyo vitu, mimi ninaona unauliza ambacho hakiwezekani.

**Nuru Said:** Right, haiwezekani, lakini twaomba

**Speaker:** Mwambia ni sawa

**Nuru Said:** Ni sawa lakini tusisumbuliwe sisi, manake hasa rangi hii mimi nasema wazi, tunasumbuliwa sana na ID na passport. Vitu hivi viwili vinatuumiza sana, mimi nina mtoto wangu 27, mpaka leo hajapata ID.

**Com. Wambua:** Mama, haya ni maoni yako. Ikiwezenaka, mtoto akizaliwa apewe birth certificate, passpot na ID pamoja. Haya ni maoni yako. Asante sana mama, jiandikishe hapo tafadhali. Kwa hivyo tutamuita hapa kabla hatujaita mama

mwingine, tumuite Urbanus Kioko. Lakini, utumie two minutes, dakika mbili tu.

**Urbanus Kioko**: Asante sana, mimi ni Bwana Urbanus Kioko na napigania u-councillor......................(inaudible) town ward. Kitu cha kwanza muhimu sana kuja hapa ni juu ya elimu. Nimeshangaa sana kuenda sana kufika mahali nikakuta kwamba watoto hawako maskuli, wako barabarani, wanaendesha

**Speaker:** usikule mic

**Urbanus Kioko**: Sawa sawa, wanaendesha magari barabarani na hawa watoto wote hawasomi. Kwa hivyo tunaomba kwamba elimu kuanzia January iwe ni ya bure, hakuna mwanafunzi kulipishwa lolote, hapa mnajua juzi walifanya..........................(inaudible) yaani elimu ni ya bure kuanzia mtoto wa nursery mpaka standard eight. Basic education mtu awe anasoma bure, hivyo inasaidia kuelimisha upumbavu ambayo ukitia sahihi haina haja mtu kutia na kidole, lazima awe amesoma vizuri. Halafu kuhusu skuli zetu za...........................(inaudible) iko hapa kweny skuli ya Kisauni, hakuna hata mtoto mmoja kutoka Kisauni anasomea pale. Ni kwa sababu gani? Kwa sababu akina mwenzetu wanatu.....................(inaudible) starehe, kutupikia viazi, utalipaa fee ama utaangalia mambo ya donor ya kununua unga?

**Speaker:** Utanunua unga

**Urbanus Kioko**: Angalia mambo ya unga, kwa hivyo tunaomba kwamba commissioner, wakati koti linapofunga mwezi wa siti waalimu wapatiwe choki za bure, andika hiyo. Waalimu wapatiwe choki za bure, hatutaki waalimu waanze kugoma na mwalimu kama amekubali mshahara wa elfu nane, asianze kugoma, kama hawezi huo mshaara, aache. Sisi tuchukuwe huyu mshahara tufanye kazi, si kuanza kusema anataka kuongezewa, aongezewe kitu gani? Mambo kama ile ya juzi mliona hapa mnajua, ma- head master wanaleta gadhabu hapa, wataka kuongeja madarasa, kuna madarasa hapa yameongezwa? Pesa tumetoa mfukoni na baado twaitishwa tena pesa, mambo kama haya ndio hatutaki. PTA ni wazazi ambao watoto wanasoma katika hii skuli kwa hivyo by January tafadhali, hatutaki miaka kumi na tano. Serikali imesema miaka kumi na tano ndio elimu itakuwa bure, la, January elimu iwe bure. Asante sana.

**Com. Wambua:** Namwita Kazungu, Kazungu ako wapi, Kazungu.

**Kazungu:** Mimi ni kusamilia, lakini ambaye nita............................................(inaudible) yuko hapa. Kwa hivyo mimi nimekuja kutoka asubuhi mzee wangu na nimesalimia watu wote. Maram yetu itasomwa na huyu mzee nimemwambia nini.

**Speaker:** Ni sawa

**Com. Wambua:** Ninataka yule ambaye atazungumza kutoa maoni.

**Kazungu:** Ndiye huyu mzee wangu

**Com. Wambua:** Basi aketi hapo atoe maoni. Mzee nitakupatia dakika mbili tuu kwa kifupi utoe maoni yake halafu utupatie hiyo maandi, tutaenda kuyasoma halafu tu................................(inaudible)

**Ali Hamisi:** Kwa jina naitwa Ali Hamisi. Katika maoni ya watu wa Bombo Kassan, ambao wamenipa nije niwakilishe hapa Bombo Kassan, wamesema kuwa kuwe na serikali ya majimbo. Watu wa huko wamesisitiza sana serikali ya majimbo ili kila jimbo liweze kujitawala hilo lenyewe. Jambo la pili, kila mwana kenya aliyezaliwa jimbo hilo au ambaye anaishi katika jimbo hili au ambaye amezaliwa katika jimbo hili aishi jimbo hilo hilo kwa sheria ya jimbo. Jambo la tatu, zile manifesto ya viama vya kisiasa viwe na muongozo wa majimbo, ziwe na maongozo ya majimbo. Hivi ndivyo wato wa Kassani wamenieleza kuwa nije nitoe hayo manifesto, zile sheria za kisiasa, vile vitabu vyao waweke sheria za majimbo. Sikuwa yeye ana chama kina kile kitabu chao cha manifesto na hakina majimbo. Huyo asipatiwe licence ya kupigia kura katika Kenya. Lazima manifesto yake iwe ina mwongozo wa majimbo. Jambo la elimu, watu wa Bombo Kassani wamepitisha au wametoa mawazo yao kuwa elimu, kwa vile watu ni maskini zaidi na watoto wanaendelea kuzurura ovyo ovyo, iwe ya bure mpaka form four. Hapa ndio patakua hana uwezo wa kujitafutia kazi yeye mwenyewe hata kama hakuendelea. Kuhusu wabunge, mbunge kawaida zao ni kuwanyanyasa wananchi. yeye anasimamisha wananchi mlolongo kupigiwa kura halafu akisha pata basi, hawajui wananchi. kwa hivyo, mbunge kama huyo ambayo hashugulishani na wale matajiri wao waliowaandika, hawatizamiwa kiasi cha miaka miwili. Ikiwa hakutimiza masharti ya wananchi, atolewe, aje hapa nyumbani arudishwe mtu mwingine. Kuhusu waislamu, muislamu ana haki ya kupewa dhima yake na sheria zake na hukumu zake ziliko katika kitabu cha Koran tukufu. Muislamu kwa kifupi, katika sheria ya kislamu, mwizi akiiba hukatwa mkono. Tunaomba katiba nayo itupe uwezo huu ili tupunguze haya matatizo ya wizi. Katika muislamu, mtu katika sheria ya kislamu, mtu akishikwa na bibi ya mwenziwe ni apigwe mawe hadharani mpaka afe. Hii ni sheria iko katika kwa waislamu. Katika sheria za kislamu, zipewe uwezo wa kuweza ku........................(inaudible) kwa ufupi

**Com. Wambua:** tafadhali, malizia tafadhali

**Speaker:** Malizia

**Ali Hamisi:** Kwa hivyo ninamalizia kwa kusema kuwa, katika sheria ya kislamu, mtu akiua mwenziwe ni auawe, akiuwa mwenziwe na auawe na akimjuruhu mwenziwe, akimkata kisu ipimwe kiasi cha vile alivyokatwa na yeye akatwe.

**Com. Wambua:** Asante sana mzee, kwa hivyo jiandikishe hapo tafadhali...................................................................(inaudible

**Ali Hamisi:** Salaam Aleikum

**People:** Aleikum salaam

**Com. Wambua**: nawaita sasa, pengine tutawasikia watu wengine hufanya hivi, kabla hatujakiahirisha hiki kikao na kwanza, tusikize hapa kwanza tuangalia nani yuko hapa. Hii page ndio tutaanzia. Tutamwita mama Irene Randu, yuko? Mama huyu tutamsika halafu tu, wacha tuangalie, Said Adul yuko

**Speaker:** Yuko hapo

**Com. Wambua:** Haya, Nyiva .................(inaudible) yuko, hayuko

**Nyiva:** Niko hapa

**Com. Wambua:** .........................(inaudible) yuko,

**Speaker:** Ngoja kwanza

**Com. Wambua**: Hayuko, Tume Shukari yuko, hayuko

**Irene Randu**: Kwa majina naitwa Irene Randu na niko hapa kwa niaba ya maendeleo ya wanawake, YWCA na vikundi vyote vya kina mama wa Kisauni. Katika kaiba yetu tumeona haina utangulizi wowote kwa hivyo haijulikani ni kina nani wenye kuishi katika hiyo nchi. Kwa hivyo tungeomba katiba iwe na utangulizi, ijulikana kama hapo ndani kuna wakenya na tu watu wa iana gani na wingi wetu na mila zetu na kadhalika. Na tumelia mama, tumesema msichana akiwa ameshikishwa mimba skulini, kuna tabia ya yule msichania kuadhibiwa, kufukuzwa. Tungeomba wote, msichana na mvulana waadhibiwe na pia msichana akisha zaa aweze kurudishwa skuli mara moja akiwa ana afya nzuri. Mateso kwa wakina mama kutokana kwa nyumba zao hasa katika hali ya brutality, tumeona yamezidi na kutungwe sheria ya kuweza kumlinda mama.

Mama akifiliwa na mume wake wa halali, apewe uridhi asomeshe watoto aliowachiwa. Uridhi usichukuliwe na mashemeji au jamii ya mume wake, pia asichukuliwe ufa, maradhi yamezidi sana. Kuundwe wizara ya wakina mama pamoja na watoto na tuweze kuwa na waziri wetu wa kike. Vikongwe wajengewe makao pamoja na watoto wanao randa randa pia watengezwe makao

**Com. Wambua**: Kelele nyingi.................................(inaudible) tafadhalini

**Irene Randu**: Na ikiwa wataondoka katika hayo makao warudi mabarabarani wachukuliwe hatia. Sheria iruhusu wakina mama nafasi ya kuamua ni watoto wangapi wanataka kuwazaa kulingana na afya zao sio kushurutishwa ataje majina mbari nzima. Lazima waislamu wapewe wakina mama wakili wao ambaye atakaye simamia haki za watoto na wakina mama ambao wamemchagua wao wenyewe.

Uandikishaji wa kupiga kura uwe ni wa kuendelea kwa sababu mda ya kujiandikisha kura hujulikani, kuwe na ofisi maalum za kujiandikisha. Wananchi wanaofikisha umri wa kujiandikisha waweze kujiandikisha mahali popote wakati wowote. Kuwe na women desk katika ma-police station na hospitali zetu tumesema ziwe bure kwa sababu hali ya vifo na maradhi ni mengi sana, imeweza kutuadhiri sana ki uchumi. Uradhi, siku bwana akimwacha mkewe, mali yao yagawanywe nusu kwa nusu manake bibi pia amechangia katika kujenga hio nyumba. Mwanamume akinajisi mtoto mdogo, sehemu zake za siri ziweze kuwa castrated manake hukumu anayopewa ni ndogo sana ndio maana wanaendelea kila siku. Baba akimruka mama kuwa mtoto si wake, kuwe na sheria za kupimwa damu ili mzee huyo aweze kusimamia malezi ya huyo mtoto. Kuwe na koti ya uamuzi ya wakina mama, mila ya kuridhi mwanamke ikomeshwe, miji Kenda nao pia wanalia sana pamoja na mila zingine ambazo zinazidi kuleta mateso, mila ndogo ndogo za mama ameolewa, siku akiachwa anaambiwa arudishe mahari na yule bwana hawezi kumrudishia uzuri wake na usichana wake. Bibi na bwana wakiachana, mke na nume wakiachana, watoto wakiwa wako chini ya umri wa miaka kumi na nane waachiwe mama yao katika nyumba ile ile walio lelewa. Yule mume akiwa amepata mke mpya, aende akaanze boma jipya. Kuwe na tume speciali katika hospitali ambazo zitaangalia malalamiko ambayo tuko nayo, unaeza kwenda mama kuzaa hospitali na mtoto wako akadhuriwa kwa sababu ya ujeuri ulioko katika mahospitali, mtoto akaangushwa, akawa mlemavu na hakuna mahali tunaweza kupeleka hayo mashtaka. Na tabia ya wazazi, ikiwa ni baba au mama kuingilia ndoa za watoto wao zikomeshwe kwasababu hao ndio wanazidisha talaka na watoto wengi wanaadhirika kwa sababu ya ndoa kuvunjika ovyo ovyo.

**People:** ...................................................(inaudible)

**Irene Randu:** Na baba wa kambo na mama wa kambo pia waulizwe wazi wazi ikiwa hawawezi, mzazi wowote kulea mtoto wa mwenziwe aseme wazi wazi kuliko kumfanyia mateso. Tumesema natural resources ziweze kusaidia katika province zinakotoka kwa hivyo zitatusaidia kutokana kwa upande wa elimu, hospitali na mambo mengine. Ukatili katika majela hasa hizi juvenile courts za watoto wetu

**Com. Wambua:** Summarize tafadhali, nimekupatia muda

**Irene Randu:** sisi tumeketi kutoka asubuhi na kina mama tumedhulumiwa na mumetuonyesha wazi hapa. Ukatili undolewe katika jela za watoto wetu

**Com. Wambua:** Mama................................(inaudible) tafadhali mama

**Irene Randu:** Nishamaliza

**Com. Wambua:** Nimekuita hata kabla ya watu wengine ambao walijiandikisha mbele na nilifanya heshima shauri wakina mama walingojea, kwa hivyo

**Irene Randu:** Bakia dakika ngapi

**Com. Wambua:** Nimekupatia nusu dakika umalize

**Irene Randu:** Asante, ningeomba kuwe na family support kwa familia zilozo na watoto walemavu kwa sababu malezi yao yako ghali sana. na kuwe na board za vitu kama hiyo minazi, korosho na kadhalika kuweza kurudisha uchumi wa watu wa hapa pwani. Na mbunge akiwa amechaguliwa katika tikiti ya DP au katika chama chochote, akirudi ku-defect akienda mbungeni atolewe kwa sababu atakuwa si wale watu waliompeleka huko, arudi angoje tena mwaka mwingine ndio aweze kusimama. Asanteni

**Com. Wambua**: Asante mama, jiandikishe hapo tafadhali....................................(inaudible) sana lakini, sasa nitamwita Ali Omari Majimbo. Ako wapi?

**Ali Omari**: Niko Bwana

**Com. Wambua:** Dakika zako ni mbili mzee, umalize yale unataka kusema..........................(inaudible) na tutawapatia nafasi hapa tuko na ndugu zetu ambao...................................(inaudible)

**Speaker:** ngoja nikalie sasa

**Com. Wambua:** Kwa hivyo

**Speaker:**......................................(inaudible)

**Com. Wambua:** Wapewe nafasi hapo mtaelezewa..................................(inaudible)

**Speaker:** .......................................................(inaudible)

**Com. Wambua:** Maliza hapo mzee.

**Ali Omari Majimbo:** Asante. Mimi sina mengi, yangu ni machache

**Speaker:** Jina yako tafadhali

**Ali Omari Majimbo:** Jina langu ni Ali Omari Majimbo, hilo jina maarufu sana hilo. Mimi nazungumza kwanza mambo ya ardhi. Hii mambo ya ardhi ni mambo moja ambayo tulidhulumiwa na hao waliotudhulumi mpaka dakika hii tunao. Kwa hivyo, ningeomba mambo ya ardhi haya yachukuliwe haraka sana ili ardhi hii irudi kwa wananchi wenyewe. Kwa sababu, hapa tuna ushahidi kamili kwa sababu sitaki kusema neno holela. Huyu, bi Sultani, huyu Sultani aliyekuja hapa kutoka Yemen na watu wake na akanyakua aridhi yote akawapa watu wake. Hawa kununua, sasa leo sisi wananchi kwa nini tununue ardhi hii?

**Speaker:** Kweli

**Ali Omari Majimbo:** Ikiwa hawa hawa kununua huyu ndiye angekuja kuwapatia watu wake? Ndiye alitawala hapa na kwa nini ha kununua na sisi leo twambiwa tuuziwe. Tuuziwe na nani? Ukweli ni kwamba, ikiwa wewe umenunua, si kusema eti ni tajiri sana, hakuna jina la kuwa karibu na............................(inaudible) ardhi wala suma neno la ardhi, wala mwakio ni nani, hakuna. Kwa hivyo walinyakuwa, kwa hivyo ni haki yetu ardhi hii tupate, hilo ni jambo la kwanza. Jambo la pili, mweheshimiwa ni mambo ya hii majimbo. Tunataka majimbo na tunaona ni aibu sana katika nchi za kiafrica, leo hii pwani peke yake. Nisha tembea Tanzania, Uganda, wapi, sikuona mtu yeyote squatter. Nimetembea Kakamega, Western kule wapi, bara nzima. Kenya nimetembea, sikuona squatters, ajabu squatter ni hapa. Kwa hivyo hii mambo nataka tukomeshe. Kama serikali haiwezi kukomesha, tutakomesha wenyewe kwa sababu imefika wakate. Mimi sitasema zaidi maanake naambiwa wasemaji ni wengi na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

**Com. Wambua:** hizi ..............................(inaudible) za mwisho ni zako kabisa

**Ali Omari Majimbo:** Tena ninakuletea kitambulisho sasa hivi hapo

**Com. Wambua:** Jina lenyewe ni Majimbo

**Ali Omari Majimbo:** Hilo ndilo linajulikana sana hilo

**Com. Wambua:** Na wewe unataka serikali ya majimbo

**Ali Omari Majimbo:** Serikali ya majimbo manake ndio italeta amani katika nchi nzime

**Com. Wambua:** Asante sana mzee, jiandikishe hapo.

**Ali Omari Majimbo:** Asante, kidogo tu, neno moja, neno moja tu babangu tafadhali. Kwa sababu ukaona nchi za kiafrica, vita.......................(inaudible) haviishi sababu hakuna majimbo na majimbo inaleta haki kwa wananchi. kwa hivyo naiomba tafadhali serikali ya majimbo kila watu jimbo lao. Lakini kitu nataka ni kwamba, serikali kuu lazima mjue iko. Na serikali kuu tunataka iwe raisi awe ni mthamini wa nchi juu, pesa zikija kwa wafadhili, kila jimbo wagawanyiwe zao ili waweze kutumia, wakitaka kulipa walipe, sisi hatutaki celi kama hii. Pesa zaja zaingia mfukoni kwa watu, utaona watu wa Kakamega walipa, watu wa Kisumu walipa, watu wa Pwani wa lipa, lakini twalipa kitu ambacho hakutumia sisi. Hii ni dhambi kabisa. Ndio maana tunasema tunataka majimbo. Asanteni.

**Com. Wambua**: Asante sana Mzee, kabla hatujawaita ndugu zetu ambao wameingia sasa, tutamsikiza mwingine mmoja, Said Abdul, dakika chache tu, mbili ndio tuwapatie nafasi wengine. Excuse me, who is the translating ................................(inaudible)

**Speaker:** He will do it.

**Said Abdul:** Asante sana ma-commissioners na watu wote waliohudhuria hapa. Kwa majini naitwa Said Abdul Athman, leader of youth, Kisauni...........................(inaudible). Asalaam Maleikum. Langu haswa ni kuzungumzia habari ya ardhi kwanza. Makao ni muhimu na mimi ni mzaliwa wa hapa na tangu nizaliwe mpaka sasa nimesoma sehemu nyingi lakini najikuta niko katika hali moja ya unyonge kwamba jina langu ni squatter. Na nikitoka huko nikirudi hapa mpaka sasa sina makao kwa hiyo makao ni muhimu sana. Tunaomba kila mtu apatiwe haki yake, apate tittle deed yake ajisikie naye pia ni mtu wa hapa Kisauni. Nikija katika upande wa kazi, vijana wengi hapa Kisauni hawana kazi na hii ni constituency. Naongea kwa niaba yao kwasababu nimefanya research na nina statistics kwamba vijana elfu 30-hapa Kisauni hawana kazi. Hii ni idadi kubwa sana kwa hivyo ningependa asli mia 75% ya kazi zote hapa pwani ikiwa Bamburi, ikiwa ni beaches, ikiwa ni KPA wawafikirie hawa vijana. Ama kama sio hivyo, mimi pamoja na vijana wenzangu tutaunga hata kama ni kutumia nguvu ili sisi tuweze kujiendeleza.

Upande wa afya, tunasema kwamba huduma za afya lazima ziwe bure kwa sababu sasa ukiangalia kama Kisauni, vijana hawana kazi, utapata wapi mapeni ya kuwasaidia wazazi wao au ndugu zao katika chochote? Kwa hivyo afya iwe bure. elimu vile vile tunaomba iwe bure na upande wa polisi. Upande wa polisi tumeona kwamba hiyo kazi wanaofanya ni kama ule muda wao wako training sio wa kutosha, kwa hivyo kama ilikuwa ni miezi tisa, labda waongezewe miaka moja u nusu manake wajidumishe vizuri kwa sababu hawajifundishi jinsi ya kuishi vizuri na vijana wenzao. Wakishika vijana hapa, hauna hatia, wewe ni shida moja kwa moja na ukifika kule wewe huna kazi lakini utaulizwa utoe.................(inaudible) utazitoa wapi? la pili, tunaona kwamba kuna watu wengi ambao serikali yetu imepate ma-rais wawili tangu ijinyakulie uhuru ambao ni Bwana Kenyatta na vile vile Bwana Moi, hatujui atakaye kuja sasa. Hii tabia ya kubadilisha pesa, tunaomba kwamba ikome. Pesa zote ziwe na sura ya kiongozi wa kwanza kabisa ili iwe ni historia kila mwananchi ambaye atakuwa pia hakumwona aweze

kujua raisi wake aliyetu kombolea nchi hii ni nani kuliko kuingia kwa hasara ya kutengeza pesa sijui Kibaki pesa zake, kijana pesa zake, hii ni kuharibu mali ya uma sana. Halafu mishahara, kazi zote, kazi zote zifikiriwe mishahara maalum, wabunge mishahara yao ipunguzwe na hata ma-commssioners pia mishahara yao tunaona ni mingi sana. Ikiwa sisi hapa tumeshinda kutoka asubuhi hatujakula, na tumefanya kazi hii kuhakikisha kwamba nini, hiyo ni haki gani? Asanteni kwa hayo machache, asante.

**Com. Wambua:** Asante sana, jiandikishe hapo, tume sikia maneno yako kwa hivyo wamepokelewa. Sasa, tutawauliza tu watu wengine wawili watu hivi halafu tutafunga kikao. Wale ambao wamebakia, bila kutoa maoni ni watu wengi na ni arobaini na watano, nimewahesabu tayari. Kwa hivyo inaonekana lazma tutafanya mpango turudi hapa ndio maoni ya wale ambao wamebaki yatapokelewa. Hata tukiketi hapa mpaka kesho asubuhi, pengine hatutamaliza kwa hivyo lazima tutamaliza. Tutawapatia nafasi mzee tu hapa aliyefika hapa wakati huu na wawili wao ndio wataongea peke yao. Tutamwita mmoja, Peter Musiko

**Peter Msiko:** Peter Umano

**Com. Wambua**: Sasa wewe tutakupatia nafasi dakika mbili utupatie maoni yako halafu yule atakayefuata ni John Nyangate, ndiye atakaye fuata halafu kumalizia kabisa baada ya hawa wawili kutoa maoni yao, tutamwita huyu Bwana Khumala, nilimtaja, ako wapi halafu wewe ndiyo sasa utamalizia. Halafu tufunge kikao. Endela hapo Peter Musiko

**Peter Msiko**: Mimi naitwa Peter Msiko na sioni, jambo la kwanza. Ningependa kuzungumza kuhusu hasa sisi watu ambao kwa jumla walemavu na vipofu kwa sababu sisi huwa tunapata shida sana katika hii serikali yetu ya wakati huu. Kwa sababu sisi bado hatujajulikana ama sisi tuko watu. Ingawaje sisi tunajiona tuko watu, bado hatujatambulika kama sisi tu watu. Nikasema hivyo kwa nini, sababu utakuja ona hata kama kwenye parliament, wakati inasemekana parliament inafanya vikao vyao, hutasikia habari wa walemavu ikigusiwa, wala eti walemavu wafanyiwe hivi, hiyo ni kitu tunafaa kuzungumza just verbally. Na inafaa kusemekana tu basi, walemavu watapata kitu fulani na hio kitu inaishia pale pale hata hiyo kitu hatutaiona, inaisha vile vile. Na jambo lingine, watoto walemavu hata sisi walemavu, elimu yetu kama tungepewa elimu ya bure, kidogo ingesaidia walemavu kwa njia nyingine. Kwa sababu sasa ikiwa mzazi wa mlemavu anaambia atoe shilling elfu ishirini ama thelathini alipie mtoto wake mlemavu, na zile pesa hana, atafanya nini? Yule mlemavu itabidi akae nyumbani bila kusoma na utakuja kuona pia katika hivyo pia, mtu ambaye haoni shida ni hio hio. Kwa sababu utakuja kuona kama wewe huoni na kama haukusoma, uko hali yako pengine na mwenzako. Na utakuja ukipita mbele ya watu wengine pia wanauliza, ‘eh, na huyu mtu, namna gani huyu mtu, ana tembea ki vipi huyu mtu?’ kuna wale wana roho ya imani, watakushika mkono akuambie, ‘ eh, mzee ama mama, hapa utagongwa na kitu, pita hapa hivi’. Lakini kuna wale wanakuangalia tu, wewe unapita lakini kama una elimu kidogo na uko na idea ya kutembea, unatembea. Tatu, sisi walemavu tunataka wakati tumeajiriwa, tupate kuajiriwa na ma kampuni, tusifanyiwe ubaguzi. Katika ma kampuni mengi utakuta walemavu hatupendwi sana kwa sababu wanafikiria pengine huyu hata akiandikwa, atafanya kazi gani huyu? Pengine huyu mlemavu hata akiwekwa hapa, atafanya kazi gani huyu? Hakuna kazi yoyote atafanya.

Kwa hivyo ninaomba serikali ijaribu sana kutufikiria sisi walemavu. Lingine, huu wakati ukifika wa kura, serikali ijaribu kutuweka karibu walemavu kama watano hivi kwenye bunge. Kidogo tutajisikia pia nasi ni watu. Sababu wale ndio watakao kuwa wakijua shida zetu, tutakuwa tukienda kwao, tunazungumza nao, tunawambia sisi bwana shida yetu ni hii na hii na kwa kuwa ni walemavu kama sisi, watatusikia, watatuelewa. Lakini saa hii hata ukienda kwa bunge useme ah basi kule walemavu hata, hata kwanza hawatakuelewa unazungumza kitu gani. Kwa sababu hakuna mlemavu pale ambaye anajua shida ya mlemavu. Lingine, katika hizi, tunaitaje hizi, hii mahospitali na, ma hospitali sana sana, tunataka tuwe na free, matibabu ya bure. kwa sababu walemavu wengin wakati huu kusema ule ukweli hawana uwezo. Na mlemavu aweza kuenda hospitali, ni mgonjwa kabisa na unamwona huyu mtu ni mgonjwa, lakini inabidi aambiwe atoe pesa. Hizo pesa atapata wapi na ni mlemavu? Na hana kazi yoyote yule mlemavu ukimfikiria hivi? Unamwambia atoe pesa, atatoa wapi hio pesa? Inabidi yule mlemavu apate msamaria mwema, asipo pata msamaria mwema, basi yake yanaisha na Mungu. Lingine ni kwa kuwa tujaribu kuangalia

**Com. Wambua:** Tafadhali

**Peter Msiko:** Kidogo nimalize

**Com. Wambua**: Malizia tafadhali

**Peter Msiko**: Lingine ni habari ya usafiri. Usafiri, serikali ijaribu kuangalia njia nyingine la kutengezea magari ambayo mlemavu anaweza kuingia bila matatizo. Hiyo nafikiri itatusaidia kwa njia nyingine. Asanteni sana

**Com. Wambua**: Asante sana Peter Msiko. Jiandikishe hapo tafadhali, maneno yako yamepokelewa, tutayaangalia vilivyo. Tutamwita John Nyagaka na yeye pia atoe maoni yake na kwa sasa wale ambao wako na maandishi ama memorandum na walikuwa wamejiandikisha kutoa maoni, nawauliza walete hiyo memorandum hapa ama maandishi, tutaenda nayo na kabla ya kurudi hapa kupokea maoni. Kwa hivyo usiende na memorandum kama ulikuja nayo hapa kutupatia. Kwa hivyo kama kuna mtu yeyote ako na maandishi, alijiandikisha kutoa maoni atoe hapa halafu tutatangaza siku ya kurudi hapa kisauni. Endelea nanii, John.

**John Nyagaka**: Wenzangu, habari ya jioni, kwa hakika ni furaha yetu

**Speaker:** Sema majina

**John Nyagaka:** Ya kwanza, majina yangu vile mumesikia naitwa Johnstone Nyagaka na ninafanya kazi huko Bombolulu workshops. Wengi wenu mnaijua na ningependa kuchukua hii fursa hakika kwanza kushukuru huu muda ambapo tumepewa sisi ili tupate kutoa maoni yetu kama walemavu. Na sijui kwa hakika hapa, vile tume kaa hiki kikao, ni mzazi ama ni wazazi

wangapi ambao wana watoto walemavu ama kuna jamii ambayo ina mlemavu. Mlemavu katika jamii tangu kitambo ni mtu ambaye amedharauliwa sana na huwa ni kama laana katika jamii. Na hio kweli imekuwa ni

**Com. Wambua**: Tumsikize mwenzetu hapa tafadhali. Excuse me, can you organize yourself so that you dont disrupt the proceding, we cannot have two or three at a time or maybe.................(inaudible) to record the .................(inaudible) outside there. I think it will be better. Nendeni nje hapo tafadhali mujiandikishe

**John Nyagaka:** Venye nilikuwa nasema, mlemavu katika jamii tangu kitambo amekuwa ni kama laana. Na utapata kwa muda mwingi huyu mlemavu hapewi nafasi na hata kwa serikali yetu, ni ajabu sana serikali yetu ilikuwa inadharau mtu mlemavu sana mpaka wakati wa multi-party ilipo ingia ndio kidogo imeanza kutambua umuhimu wa yule mlemavu. Kitambo haungeweza kupata mlemavu bunge na ni kitu cha kushangaza kwamba mlemavu ni binadamu, anataka huduma kama yule mwingine lakini serikali haimtambui. Ningependa kutoa maoni yangu na yangekuwa ni kama sheria ipitishwe katika bunge ambayo itamuwezesha yule mlemavu kuonekana kama mtu yeyote yule. Ya kwanza ningependa mtu mlemavu akipata elimu yake, iwe ni ya bure. elimu wengi wetu ambao ni walemavu kama mimi nimepata elimu kupitia wa-missionari. Kama si missionari singepata elimu na kwa sasa hivi wamisionari wamejiondoa katika serikali yetu. Watoto walemavu wanapata shida sana. Serikali haioni hivyo, vituo vingi vya walemavu vimefungwa, serikali ikisema haina pesa, kumaanisha kwamba bila wale misionari wamejitoa, serikali haiendelezi elimu wa walemavu. Utapata mlemavu amewekwa kwa kiwango kile kile cha yule ambaye si mlemavu. Kwa hivyo ningependa serikali iangalie upande wa mtoto mlemavu kuwa hata yeye anahitaji elimu, anahitaji afya nzuri na iwe ni sheria kwamba yule mlemavu aangaliwe kabisa. Kitu cha pili, akisha maliza shule, anaweza kuwa amefaulu vizuri sana. Ni ajabu kwamba mlemavu ukituma application kwa kampuni yoyote ile, yule mwajiri hatajua kwamba wewe ni mlemavu wakati umetupa application hajakuona. Utakapo itwa kwa intervew, na kweli una qualifications za kutosha, utakapo kwenda kwa ile interview na mwajiri aone wewe ni mlemavu, huwezi kutembea, haoni, husikii, ile kitu atafanya, pengine atakupa shilingi elfu moja akwambie, ‘am sorry, ile kazi iko hapa wewe huwezani nao’. Lakini kulingana na qualifications zako, unaweza ile kazi. Sasa hio opportunity ambayo, I mean, kutuonea huruma hatutaki. Tunataka opportunity, nina elimu ya kutosha, nipe ile opportunity kama umeamua kuniajiri, niajiri uone kazi yangu, uone outcome yangu. Wacha kunionea huruma kwamba mimi siwezi, ninaweza. Kwa hivyo ningependa serikali ilitie mkazo kupitia parliament, kwamba kila kampuni ipeane percentage fulani ya kuajiri mtu mlemavu. Atleast kama pale Bamburi kungekuwa na walemavu ambao wanafanya kazi pale. Kuna watu wengi sana walemavu wamesoma, lakini ukienda bamburi pale pengine huwezi kupata mlemavu, kwa nini, hawezi kazi lakini qualifications, certificates, anazo. Kwa hivyo tungependelea iwe ni mjadala bunge ipitishe iwe ni sheria kwamba kila kampuni ipate kupeana nafasi kwa mtu ambaye ni mlemavu. Kitu kingine, kuna hizi funds zinakuwa managed, nizawalemavu ndio kama zile wakati mwingine serikali imechanga funds za walemavu. Lakini utapata wale wanazi manage si mtu mlemavu. Utapata mtu anazi manage ni mtu ambaye anatembea vizuri, hajui shida za mlemavu, uki apply ile fund, hupati na unashangaa sasa ile fund ni ya nini. Haikufikii wewe, ukitaka huipati, sasa unashindwa hii fund basi haja gani ikachangwa kwa kutumia jina lako na hauipati. Kwa hivyo tungependa parliment iangaliwe, iwe ni sheria ya kwamba ile kitu iwe governed na mtu ambaye ni mlemavu. Hata pahali, institutions kama Bombolulu, iwe walemavu wamepewa

**Com. Wambua**: ........................(inaudible) tafadhali, maliza sasa

**John Nyagaka:** Kwa kufupisha, nina memorandum nimeandika nafikiri nitapeana

**Com. Wambua**: Hiyo ndio tutahitaji sana zaidi kushinda.........manake tutaichunguza vilivyo, tujue ni maneno gani yalioko.

**John Nyagaka:** Asante sana

**Com. Wambua**: Kwa hivo kama kuna memorandum tupatie ndio twende tukasome na tutaichukua kama representative opinion. Kwa hivyo hiyo hata itafaa sana. Kwa hivyo kama kuna memorandum tafadhali tupatie. Lakini nitakupatia half a minute umalizie

**John Nyagaka:** Haya, kumalizia, pia tungependa mambo ya retrenchment isi affect mtu mlemavu. Mtu mlemavu ametegemea ile kazi ambaye amebahatika kupata katika kampuni fulani ile. Utapata ile retrenchment, mtu wa kwanza kuwa affected ni mtu mlemavu. Sasa unashindwa, akiachiswa ile kazi, ataenda kufanya kazi wapi na pale ndio alikuwa anategemea kuelimisha watoto wake, kujipatia riziki yake ya kila siku na amesimamishwa. Itabidi huyu mtu tena arudi kuomba omba pale town ama pahali popote pale ambapo sio picha nzuri. Kwa hivo asante mwenye kiti kwa nafasi hii.

**Com. Wambua**: Asante sana, utatupatia hiyo memorandum, tafadhali jiandikishe hapo. Mwisho kabisa, mtu wa sabini ambaye atakuwa ni wa mwisho ni Bwana Kumala, kwa hivyo nitakupatia two minutes halafu tutafunga hiki kikao, kwa hivyo usipitishe muda wa dakika mbili, useme yale ya muhimu halafu ufunge.

**Juma Athmani:** Jina langu naitwa Juma Athmani Kumala, bwana commissioner mimi sina mengi, mengi yamezungumzwa. Lakini langu ni kulitilia mkazo swala la majimbo kwamba sisi wakaazi wa pwani ni lazima tujitawale sisi wenyewe. Utakuta sehemu kama vile Kenya Port, Bamburi Portland Cement ni ma kampuni ambayo yako katika maeneo yetu na wajibu wetu wakaaji wa pwani tuwe tutapewa nafasi ipasavyo. Sio watu kutoka sehemu za bara wanaingia na kuchukua nafasi kama hizo. Kwa hivyo swala la majimbo, mimi maoni yangu kama Bwana Kumala naliunga mkono sana. na serikali ulichukuwe na ulitilie maanani zaidi. Lingine, kuna mzee wangu amezungumzia kuhusu dini ya kislamu. Kama tunavyo fahamu, mimi ni muislamu na dini ya kislamu inakataza zinaa kabisa. Na mimi maoni yangu ningelipenda, kuwekwe sheria, mtu anapo patikana akizini, kuwekwe sheria mtu yule afunguliwe mashtaka na astakiwe mahakamani. Kwa sababu hata dini ya kislamu inakataza zini, kwa hivyo hili ni jambo na maoni yangu ningelipenda litiliwe mkazo. La mwisho ni kuhusu hawa viongozo ambao miaka yao imezidi. Itakuta mtu ametumikia serikali kwa muda mrefu na ame retire. Na amesikia kwamba uchaguzi unaingia, yeye anataka kupigania uongozi; either wa udiwani au wa ubunge na miaka amepita miaka mingi. Kwa hivyo, kuwe na miaka kadhaa mtu atapaswa apiganie, either miaka sabini mtu kama huyu asiruhuwise kupigania uongozi wa aina yoyote, either udiwani au ubunge,

aachie vijana majukumu hao wao waongoze nchi. Kwa hayo machache, asanteni sana.

**Com. Wambua:** Basi asante Bwana Kumala, sasa tumefika mwisho wa kikao hiki. Tuta muita mtu moja atuombee ndipo tufunge kikao lakini kwa wale ambao hawajatoa maoni, msiwe na shaka kama nilivyo sema, tutarudi hapa. Majina tuko nayo na tutarudi hapa kupokea maoni yenu. Kama nilivyosema wale ambao nimehesabu, wale ambao wametoa maoni ni sabini sasa, wale walio bakia ni arobaini na watano hivi. Kw hivyo tutakuja hapa tupokee maoni yenu, msiwe na shaka eti kwa kuwa hamjazungumza, maoni yenu yamepotea, hapana, tutarudi hapa. Lakini siku ya kurudi hatuijui, mpaka turudi Nairobi, turudishe Secretariat ndio wapange siku ya kurudi hapa na kutuma kikao. Lakini hiyo ni lazima ifanyike. Kule kwingine tulipo kwenda ambapo hatukumaliza, walitupatia muda kurudi, kwa hivyo hiyo itafanyika. Mtu mmoja tafadhali, dini ya kislamu, tafadhali tuombee leo

**Speaker:** Kwa jina la mwenyezi Mungu..........................................................(inaudible) E mwenyezi Mungu utuongoze pamoja na walio ongoza, utusamehe pamoja na waliosamehe, utubarikie katika ulicho tupa, utukinge na maovu ulio hukumu. Akaewa hukumu mwenyezi Mungu wale hukumiwe, hakika hathaliki yule mthuru, wala hatukuki Mola wetu uliyempiga vita. Umetukuka Mola wetu na ukujua kila kitu, shukrani zote ni zako.......................(inaudible) kutupa. Kwako twaomba rabi inayotoka kwako kwa ..........................................................................................(inaudible).

**Com. Wambua:** Tulianza na maombi ya Kislamu na ya Kikristu, sijui kama kuna mmoja wetu mkristo anataka kuomba kama yuko, kama hayuko basi tumefika mwisho, kwa hivyo nendeni salama salamini.

Meeting ended at 6.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&**